**28 JANUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Pili – Tarehe 28 Januari, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Watu wenye ulemavu. Ninamwahidi, sitamwangusha.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria,

Sura ya Kwanza na Kanuni ya 46 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha:

Nakala za Matoleo ya Magazeti, pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa baada ya Toleo Na. 14 la Tarehe 04 Aprili, 2025, kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 15 la tarehe 11 Aprili, 2025;
2. Toleo Na. 16 la tarehe 18 Aprili, 2025;
3. Toleo Na. 17 la tarehe 25 Aprili, 2025;
4. Toleo Na. 18 la tarehe 02 Mei, 2025;
5. Toleo Na. 19 la tarehe 09 Mei, 2025;
6. Toleo Na. 20 la tarehe 16 Mei, 2025;
7. Toleo Na. 21 la tarehe 23 Mei, 2025;
8. Toleo Na. 22 la tarehe 30 Mei, 2025;
9. Toleo Na. 23 la tarehe 06 Juni, 2025;
10. Toleo Na. 24 la tarehe 13 Juni, 2025;
11. Toleo Na. 25 la tarehe 20 Juni, 2025;
12. Toleo Na. 26 la tarehe 27 Juni, 2025;
13. Toleo Na. 27 la tarehe 04 Julai, 2025;
14. Toleo Na. 28 la tarehe 11 Julai, 2025;
15. Toleo Na. 29 la tarehe 18 Julai, 2025;
16. Toleo Na. 30 la tarehe 25 Julai, 2025;
17. Toleo Na. 31 la tarehe 01 Agosti, 2025;
18. Toleo Na. 32 la tarehe 08 Agosti, 2025;
19. Toleo Na. 33 la tarehe 15 Agosti, 2025;
20. Toleo Na. 34 la tarehe 22 Agosti, 2025;
21. Toleo Na. 35 la tarehe 29 Agosti, 2025;
22. Toleo Na. 36 la tarehe 05 Septemba, 2025;
23. Toleo Na. 37 la tarehe 12 Septemba, 2025;
24. Toleo Na. 38 la tarehe 19 Septemba, 2025;
25. Toleo Na. 39 la tarehe 26 Septemba, 2025;
26. Toleo Na. 40 la tarehe 03 Oktoba, 2025;
27. Toleo Na. 41 la tarehe 10 Oktoba, 2025;
28. Toleo Na. 42 la tarehe 17 Oktoba, 2025;
29. Toleo Na. 43 la tarehe 24 Oktoba, 2025;
30. Toleo Na. 44 la tarehe 31 Oktoba, 2025;

31. Toleo Na. 45 la tarehe 07 Novemba, 2025;
32. Toleo Na. 46 la tarehe 14 Novemba, 2025;
33. Toleo Na. 47 la tarehe 21 Novemba, 2025;
34. Toleo Na. 48 la tarehe 28 Novemba, 2025;
35. Toleo Na. 49 la tarehe 05 Disemba, 2025;
36. Toleo Na. 50 la tarehe 12 Disemba, 2025;
37. Toleo Na. 51 la tarehe 19 Disemba, 2025;
38. Toleo Na. 52 la tarehe 26 Disemba, 2025;
39. Toleo Na. 01 la tarehe 02 Januari, 2026;
40. Toleo Na. 02 la tarehe 09 Januari, 2026; na
41. Toleo Na. 03 la tarehe 16 Januari, 2026.

**SPIKA:** Ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali. Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo.

Na. 21

### Ujenzi wa Daraja la Isakalilo – Kitwiru

**MHE. FADHILI F. NGAJILO** aliuliza:-

Je, lini Daraja la Isakalilo – Kitwiru litajengwa, ili kufungua Utalii wa Mbuga ya Wanyama Ruaha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Fadhili Fabian Ngajilo, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Isakalilo – Kitwiru lipo katika Barabara ya Isakalilo – Kitwiru yenye urefu wa kilomita tatu, ambayo inaunganisha kati ya Barabara ya *TANZAM* na Iringa kwenda Msembe. Daraja hili ni kiunganishi muhimu kuifikia Mbuga ya Wanyama ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa *TACTIC,* Awamu ya Pili, imefanya usanifu wa mradi. Baada ya kukamilika kwa usanifu, mradi huu unaojumuisha ujenzi wa daraja pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita taru utaanza kutekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngajilo.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu, daraja hilo, wananchi wamekuwa wakiahidiwa muda mrefu zaidi ya miaka 20 iliyopita na sasa Serikali imetoa kauli yake. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja, nataka kujua, na wananchi wa Iringa Mjini wanataka kufahamu vizuri, ni lini hasa sasa mradi huu utaenda kukamilishwa na fedha zitatoka?

Mheshimiwa Spika, pili, wananchi wanataka kujua je, mradi huu utatekelezwa kama *full package*? Kwamba, daraja la mita 40 pamoja na kipande cha lami cha kilomita tatu, kama alivyopendekeza msanifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, kwenye huu Mradi wa *TACTIC,* Awamu ya Pili, ndani ya

Manispaa ya Iringa Mjini, Serikali haina tatizo la fedha. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan ametenga shilingi bilioni 20, kwa ajili ya huu Mradi wa *TACTIC*.

Mheshimiwa Spika, mradi huu tunautekeleza kwa awamu mbili, kama nilivyoeleza. Tayari tumeshaanza awamu ya kwanza kwa kujenga Soko la Kihesa, kujenga barabara za Mkimbizi – Bima, Mtwivila, Viziwi na Bontank.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ndiyo ujenzi wa daraja hili, pamoja na barabara za maingilio kwenye daraja hilo. Siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Mradi wa *RISE* kwenye hii Manispaa ya Iringa Mjini anajenga barabara kwa kiwango cha lami, kilomita 37, kutoka Ipogolo kwenda Kilolo. Mradi huu tunautekeleza kwa pamoja na wenzetu wa *TANROADS*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wilson Mahera.

**MHE. DKT. CHARLES W. MAHERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Busegwe – Kitaramanka, yenye urefu wa kilomita 18 inapita katika kata tano za Busegwe – Mliaza – Buhemba na Mirwa, pamoja na Sirorisimba. Barabara hii ni muhimu sana kwenye shughuli za kiuchumi katika Jimbo la Butiama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja Butiama tulimwomba aweze kuipatia lami barabara hii akaridhia na kwa umuhimu wa barabara hii, ni Barabara ya *TARURA,* lakini inasimamiwa na *TANROAD*. Sasa swali la msingi, je, ni lini usanifu utaanza wa barabara hii, ili kusudi tuweze kupata lami katika Jimbo la Butiama?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi wetu wakuu wa nchi na hususan Mheshimiwa Rais, ni maelekezo kwetu sisi wasaidizi wake ndani ya Serikali. Namwahidi Mheshimiwa Mbunge Mahera kwamba, tunaendelea na utaratibu wa kupitia ahadi zote za viongozi wetu wakuu kwa nchi nzima na tumekuwa tukitekeleza kwa kadiri ambavyo fedha zinapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Daraja la Ipanzya – Isalalo limekuwa ni kero ya muda mrefu sana. Ni lini Serikali itaanza kulijenga daraja hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa *RISE,* tunajenga madaraja kwenye halmashauri 130 nchi nzima. Awamu ijayo na kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana tutatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda.

Na. 22

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Kitangiri – Newala**

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA** aliuliza:-

Je, lini Stendi ya Mabasi ya Mji wa Kitangari, Newala, itajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina stendi ya mabasi iliyopo katika Mji wa Kitangari, ambayo imepangwa kutengewa fedha katika Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia mapato ya ndani ya halmashauri. Kutokana na stendi hiyo kutokidhi mahitaji ya sasa ya usafiri, halmashauri imepanga kufanya maboresho ya awali kwa kiwango cha changarawe ili kuboresha utoaji wa huduma za wananchi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maboresho hayo halmashauri imeanza kutafuta eneo mahsusi, kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa itakayokidhi mahitaji ya Mji wa Kitangari na maeneo ya jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara zote zilizopo katika Mji wa Kitangari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara za lami kutoka katika Kijiji cha Maputi hadi Ndanda, na pia, katika Kijiji cha Chiwonga, Pacha Nne, hadi Nanganga? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshaanza kujenga barabara zilizopo katika Mji

wa Kitangari. Tumeanza na barabara ya kutoka kwa Mzee Lada mpaka kwa Mzee Twalibu, ambayo ina urefu wa kilomita moja, na siyo tu kwamba tumeishia kuijenga, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amehakikisha barabara hiyo imewekewa taa pia, na inatumika.

Mheshimiwa Spika, kadiri fedha zitakavyoendelea kupatikana tutaendelea na ujenzi wa barabara za mji huo. Barabara ya kutoka Msikiti Mkubwa kwenda kituo cha afya karibu na stendi, na vilevile Barabara ya Mnakute hadi Halmashauri na Barabara ya *VETA* hadi Nachirindima.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Barabara ya Maputi – Ndanda, Chuonga – Pacha Nne kwenda Mkongi hadi Nanganga njia panda ya kwenda Ruangwa, Serikali itatekeleza kama ilivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025/2030. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara hizi kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa hapo, jitambulishe kwa jina. Haa, *I see,* Issaay. Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Serikali ilikusudia kujenga stendi ya mabasi, soko, dampo na machinjio katika Mji wa Mbulu kwa kupitia Mradi wa *TACTIC*. Hadi sasa Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza mradi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi katika Mji wa Mbulu ni sehemu ya Miradi ya *TACTIC* tutakayoitekeleza katika awamu ya tatu. Hivi sasa Serikali inaendelea na ukamilishaji wa Usanifu wa miradi yote 18, kwa maana ya miji yote 18 iliyomo kwenye awamu ya tatu. Mara tu baada ya usanifu kukamilika, taarifa zote tutazikusanya na

tutakwenda hatua inayofuata ya kutangaza zabuni kumpata mjenzi, pamoja na mkandarasi mshauri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima.

Na. 23

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Iwondo - Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Iwondo ili wananchi waanze kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2021 mpaka 2022 Serikali ilitoa shilingi milioni 500, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Iwondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Fedha hizo zilitumika kujenga Jengo la Huduma za Wagonjwa wa Ne *(OPD),* maabara na kichomea taka, ambayo yamekamilika na yanatumika. Jengo la huduma za uzazi na upasuaji, ujenzi upo hatua ya plasta na jengo la kufulia hatua ya kupaka rangi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imetenga jumla ya shilingi milioni 50 katika mwaka wa fedha 2025/2026. Mwaka 2026/2027 itatenga jumla ya shilingi milioni 50, kwa ajili ya kukamilisha majengo yaliyosalia katika Kituo cha Afya Iwondo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Waziri na Naibu Waziri katika Wizara hii wote ni wageni natamani sana wapate fursa ya kufika kuona ujenzi unavyoendelea. Je, ni lini Waziri ataandamana nami kufika katika Kituo cha Iwondo cha Afya, ili aweze kuona ujenzi unavyoondelea pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Natany Malima. Sisi Wizara tunafanyakazi ya kuzitembelea halmashauri zote nchini na tumekwishaanza zoezi hilo. Namhakikishia tu Mheshimiwa Natany Malima, baada ya Bunge hili tunaweza kuongozana kwenda Jimbo la Mpwapwa katika halmashauri hii na kukitembelea kituo hiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Halmashauri ya Mji wa Bunda tunajenga hospitali yetu ambayo iko Kata ya Bunda Stoo. Serikali imetupatia fedha, lakini tangu mwaka juzi, 2024, kuna shilingi milioni 800 zilirudi na hazijarudishwa bado, huo mradi umesimama. Ni lini mtaturudishia fedha zetu shilingi milioni 800 tuweze kukamilisha hospitali ya Wilaya ambayo ina mchango mkubwa kwenye Jimbo la Bunda Mjini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, Serikali imejipambanua katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi wote. Nawahakikishia wananchi wa Jimbo la

Bunda, fedha zao zipo na tutazielekeza kuendelea na shughuli ambazo Serikali ilikuwa imezielekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsekela.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali hili la nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia wahudumu 58 katika dirisha hili la ajira za afya kwa Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Nkwenda ni kikubwa na kinatoa huduma zaidi ya Kata 19 na *sometime* kinatoa huduma nje ya Wilaya ya Kyerwa, lakini kituo hiki hakina gari ya uhakika ya wagonjwa *(ambulance),* je, ni lini Serikali itatupatia gari la uhakika kwa ajili ya kutoa huduma safi kwa kituo hicho? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT.JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, tunakumbuka sote humu ndani katika kipindi cha miaka mitano Serikali imenunua jumla ya magari ya kubebea wagonjwa 316, pamoja na magari ya wakaguzi 212 na *ambulance* za awamu ya kwanza tumeshazigawa katika Halmashauri ambazo ziliainishwa. Nimhakikishie kuwa, awamu ya pili kituo hiki kitakuwa wanufaika wa gari la *ambulance*.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Chacha Mwita Wambura.

Na. 24

**Ujenzi wa Uwanja wa Mpira Manispaa ya Geita**

**MHE. ENG. CHACHA M. WAMBURA** aliuliza:-

Je, hatua gani zimefikiwa katika kuandaa mpango wa kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu - Manispaa ya Geita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, uwanja wa mpira wa miguu - Geita ulianza kujengwa mwaka 2021 kwa kutumia fedha za uwajibikaji wa kijamii wa mashirika *(CSR)* kwa gharama ya shilingi bilioni 5.46 kupitia mgodi wa *Geita Gold Mine*. Hata hivyo, ujenzi ulisimama mwaka 2023 ukiwa 71%, baada ya Mkandarasi *EFQ Co. Ltd* kusitishiwa mkataba kutokana na mabadiliko ya kanuni ya miradi ya *CSR*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na mgodi wa *Geita Mine Ltd* imepata mkandarasi mshauri *NORPLAN* ambaye amefanya mapitio ya gharama halisi za kukamilisha ujenzi wa uwanja huo na kiasi cha shilingi bilioni tano zinahitajika. Aidha, Serikali inaendelea na mapitio ya gharama zilizowasilishwa na mkandarasi mshauri ili kuweza kuendelea na ujenzi kupitia fedha za *CSR* zitakazotengwa katika mwaka 2026/2027.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha.

**MHE. ENG. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amesema kwamba mapitio yanaendelea. Ninaomba kufahamu kwamba je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio haya kwa haraka ili basi uwanja ule uweze kukamilika na ikiwezekana ukamilike kabla ya mwakani ambapo tunaenda kuwa na mashindano ya *AFCON* ambayo yataenda kufanyika katika nchi zetu tatu za Afrika Mashariki na ambapo tunaamini Geita ni *centre* ya Kenya, Tanzania na Uganda?

Mheshimiwa Spika, kama tutaweza kukamilisha uwanja huu kwa wakati basi zile timu zinaweza zikafanya mazoezi au kutumia vile viwanja wakati wa mashindano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali katika sehemu nyingine tumekuwa tukishirikiana na tukifanya vizuri sana, na tunavyoshirikiana na *private sector,* je, katika suala hili la viwanja hapa Tanzania, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi ya ku-*engage private sector* ili kushirikiana nao na kuwa-*support* ili tuweze kupata viwanja vingi zaidi ili tuendeleze michezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura kwa kufuatilia ujenzi wa uwanja huu. Pia ninaupongeza uongozi wa Mkoa wa Geita kwa kuwa karibu na wawekezaji hawa hadi kufikia kuweka fedha hizi kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumpata mkandarasi mshauri, tayari kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 3.4 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa jukwaa juu, majukwaa ya watazamaji na sehemu ya kuchezea mpira *(pitch)* ambapo inakadiriwa kuwa ujenzi utakamilika ifikapo Oktoba, 2026.

Mheshimiwa Spika, kulingana na idadi ya wakazi wa Mkoa wa Geita inayokadiriwa kufikia milioni tatu kutokana na sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022, uwanja huu Serikali inauona kama ni sehemu ya kuleta tabasamu kwa Watanzania walioko katika Mkoa wetu wa Geita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kumwahisha mkandarasi kuweza kukamilisha ujenzi wa uwanja huu, tunao uhakika kabisa kwamba uwanja huu wenzetu wa Wizara ya Michezo wanaweza wakauona kama ni sehemu ya *AFCON* ya mwaka huu kama utakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inamhakikishia Mheshimiwa Mwita kuendelea kufuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha uwanja huu unaweza kutoa huduma hii ya michezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula Magangila.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni mpango upi wa Serikali wa kujenga kiwanja kikubwa cha kisasa katika Mji wa Kahama ambao unakua kwa kasi sana sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mipango hii ya kuhakikisha vile viwanja ambavyo vipo chini ya Halmashauri vinajengwa kulingana na vipaumbele vya Halmashauri na jinsi wataalam wetu wanavyoweza kuibua miradi katika maeneo yao. Kama kitakuwa kipo ndani ya Halmashauri kiwanja hicho, tutaweza kuhakikisha kinajengwa kwa wakati, na kama kipo kwa wenzetu Wizara ya Michezo wataweza kutolea majibu katika swali hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Malleko.

Na. 25

**Ufanisi Katika Ufikishaji Fedha kwa Walengwa**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha fedha za *TASAF* zinawafikia walengwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ahadi yangu kwake ni kuendelea kufanya kazi kwa bidii kwa kujituma, na kwa uzalendo, ili malengo yaliyopangwa yafikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Esther Malleko, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *program* ya *TASAF,* imeweka mkakati mahususi wa kuhakikisha fedha/ruzuku zinawafikia walengwa kupitia matumizi ya mfumo wa malipo ya kielektroniki *(e-payments)* unaolenga kuongeza uwazi, usalama na ufanisi katika utoaji wa ruzuku kwa walengwa. Mkakati huo unatekelezwa kwa kutumia watoa huduma za kifedha walioidhinishwa ambao hulipa fedha moja kwa moja kwenda kwa walengwa kupitia akaunti zao za benki na mitandao ya simu.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu huondoa utaratibu wa kutuma fedha taslimu, na hivyo kupunguza mianya ya upotevu, ucheleweshaji au matumizi yasiyo sahihi ya fedha. Pili, malipo yote hufanyika kwa kuzingatia taarifa za walengwa zilizohakikiwa katika mfumo wa usimamizi wa walengwa, *Management Information System (MIS),* ambapo kila mlengwa hulipwa kulingana na utambulisho wake wa kipekee, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa *TASAF* imelenga kuwasaidia kaya maskini katika kupunguza umaskini katika hizo kaya, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inawapatia wale watoto waliotoka kwenye kaya maskini mkopo wa elimu ya juu 100% ili na wao waweze kupata masomo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni namna gani bora mnayoitumia kwenye zile ajira zenu za muda, kwa sababu tumeona mara nyingi wanaoenda kufanya hizo kazi ni wazee na hawawezi kuzifanya kwa ufanisi? Mnafanya namna gani kuweza kuwapata ambao wanaenda kuzifanya hizo kazi za muda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Swali lake la kwanza, Serikali kupitia *TASAF* imeweka mkakati wa kuhakikisha watoto wanaotoka katika kaya maskini wanapewa kipaumbele kwa maana wanapewa mikopo kwa 100%, na kwa utaratibu huo *TASAF* imefanya makubaliano na imesaini hati ya makubaliano kati ya *TASAF* pamoja na Bodi ya Mikopo ili kuhakikisha kwamba wale watoto wanapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia hati ya makubaliano, *TASAF* imeendelea kuwapa kipaumbele wale watoto ambao wanatoka katika kaya maskini ili Bodi ya Mikopo iendelee kuwaona na kuwazingatia ili waweze kupata mikopo kwa 100%. Kupitia katika makubaliano hayo, *TASAF* pamoja na Bodi ya Mikopo imesaini makubaliano na katika makubaliano hayo, wamekubaliana na kuunganisha taarifa zao ili taarifa za *TASAF* ziunganishwe pamoja na taarifa ya Bodi ya Mikopo ili Bodi ya Mikopo waweze kuwapata kirahisi hawa watoto ambao wanatoka katika kaya maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, taarifa ni kwamba, mwaka wa fedha 2025/2026 takribani watoto 5,958 wameweza kupata mikopo ya elimu ya juu, jumla ikifikia watoto 18,000

wameweza kufanikiwa kupata mikopo ya elimu ya juu ili waweze kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kazi au ajira za muda. Serikali kwa kupitia *TASAF* imeweza kuweka mkakati mzuri namna ya kutoa ajira za muda kwa walengwa, hasa wale ambao tayari wako kwenye mfumo, na kwa kupitia hivyo, Serikali imeendelea kusisitiza walengwa ambao tayari wameshasajiliwa katika kaya maskini waweze kupata kazi hizo za kujitolea au kazi za ajira za muda na hizi zinazotolewa ni mpango shiriki, kwamba jamii husika inashirikishwa ili kuwapata walengwa haswa ambao tayari wameshasajiliwa kwenye mfumo na tayari wanapatikana katika kaya maskini waweze kufanya kazi zile za ajira za muda.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia huko *TASAF* imeweka vigezo ambavyo vinatumika ili kuwapata wale washiriki. Kigezo mojawapo ni kuhakikisha kwamba washiriki wazingatie umri kuanzia miaka 18 mpaka 65, lakini kwa kuzingatia pia washiriki wale wanaoshiriki katika ajira za muda wawe na uwezo wa kufanya kazi kwa maana ya kuwa na afya njema na kigezo kingine ni kuhakikisha kwamba, wale washiriki ni wale ambao tayari waliosajiliwa kwenye mpango wa *TASAF,* ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itazindua mpango wa tatu wa kaya maskini?

**SPIKA:** Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, je ni lini Serikali itazindua mpango wa awamu ya tatu wa kaya maskini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa sasa tayari imeshaweka mkakati wa kwenda kuanzisha mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya tatu baada ya kukamilisha ule mpango wa awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, mpango wetu wa awamu ya tatu ni kuhakikisha kwamba, tunaenda kuangalia yale mafanikio yaliyopatikana kwenye mpango wa utekelezaji awamu ya pili, lakini kuangalia changamoto iliyojitokeza kwenye awamu ya pili na kuenda kutafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali iko kwenye maandalizi ya kutekeleza kuanzishwa kwa awamu ya tatu ya mpango, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba.

Na. 26

**Kigezo cha Mikopo kwa Wanafunzi wanaotoka Shule Binafsi**

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha kigezo kinachowapunguzia fursa wanafunzi wa shule binafsi kupata mikopo ya elimu ya juu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upangaji na utoaji mikopo ya elimu ya juu unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (Sura 178) ambayo inabainisha sifa za msingi za mwombaji, zikiwepo sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu kwa waombaji waliothibitika kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaotoka katika kaya maskini bila kujali mwombaji ametoka shule za Serikali au shule binafsi. Kwa msingi huo, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo imeweka utaratibu wa kuzingatiwa kwa waombaji wote, bila kujali shule aliyosoma ilimradi mwombaji amekidhi vigezo vilivyowekwa ikiwemo ujazaji wa taarifa sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha.

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye sekta ya elimu. Pia naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Je, ni lini Serikali itaondoa vigezo hivi ili kuweza kuweka usawa kwa shule hizi za sekta binafsi, kwani tunafahamu kabisa kwamba wanafunzi hawa wanaosoma sekta binafsi wanasaidiwa na wazazi ambao wanajikwamua kwenye kipato cha chini, yaani wanajinyima, pia wanasaidiwa na marafiki, ndugu, jamaa na watu mbalimbali kutoa misaada hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, ni lini Serikali itaondoa vigezo hivi ili kuwatia moyo wazazi hawa ambao wameweza kujinyima kuwalipia ada na watu mbalimbali wanaochangia hizi ada, ili kupunguza msongamano kwenye shule za umma kwa maana ya shule za Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu hauhitaji kigezo cha aina ya shule aliyosoma mwombaji, iwe ya Serikali ama iwe ya binafsi. Hivyo, wanafunzi wote sifa za kupata mkopo wa elimu ya juu hupatiwa mkopo huo kwa mujibu wa utaratibu wa vigezo vilivyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Sura 178, imeweka vigezo mahsusi ambavyo mwanafunzi mlengwa hutakiwa awe navyo. Vigezo hivyo ni pamoja na; awe Mtanzania mhitaji, awe amepata udahili katika taasisi zinazotambulika, pia awe amejaza fomu hizo kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi na swali la nyongeza, ni kwamba hakuna kigezo kinachowapunguzia fursa wanafunzi wa shule binafsi kupata mikopo.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

Na. 27

**Ujenzi wa Barabara ya Mombo – Soni – Lushoto**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mombo – Soni – Lushoto km 36 kama ilivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mombo hadi Lushoto yenye urefu wa kilometa 36. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kutoka Serikalini, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inao upana wa mita saba ambazo kwa kweli ni viwango vya zamani sana. Nataka kufahamu kwamba je, huu upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umezingatia viwango vya sasa vya upana wa barabara ili watakapoanza kuijenga magari yaweze kupishana bila usumbufu kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Barabara ya kutoka Mlalo kwenda Lushoto kipande cha kutoka Nyasa kwenda Majulai kilomita tatu, sasa ni takribani mwaka mmoja mkandarasi ameshasaini mkataba, lakini bado hajapewa barua ya uthibitisho kutoka Serikalini. Je, ni lini Serikali itatimiza jukumu hili ili mkandarasi yule aweze kuendelea na kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba usanifu ambao umefanyika umezingatia viwango vya sasa vya upana wa barabara na *carriageway* ya barabara zetu huwa ni mita tatu na nusu kwa kila upande. Kwa hiyo upana wa barabara unakuwa ni mita saba ambao unaruhusu magari kuweza kupishana. Kilichoongezeka hapo ni kwamba tutapanua sasa yale mabega ya barabara *(shoulders)* kila upande mita moja na nusu. Kwa hiyo, barabara hiyo itakuwa na upana wa mita 10 kwa maana ya barabara ambayo itakuwa inaweza kutumika tofauti na ilivyokuwa zamani, mita saba na nusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipande alichokisema, ni kwamba tayari tumekwishasaini mkataba na mkandarasi, muda wowote tukishamlipa fedha za awali ataanza kufanya kazi hiyo na tutaanza na kilometa tatu kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Suma Ikenda. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya kuanzia Katumba – Suma – Mwakaleli – Ruangwa kutokea Tukuyu Mjini ni ya muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Bararaba hiyo inajengwa kwa kusuasua sana. Sasa, ninaomba kujua na wananchi wa Wilaya ya Rungwe wasikie, je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hiyo barabara mkandarasi ameshaanza kazi, na bahati nzuri mara baada ya kuteuliwa ni kati ya barabara ambazo niliweza kuzitembelea. Kinacholeta changamoto kubwa, moja ni kwamba eneo alilolitaja ni moja ya maeneo ambayo yanapata mvua nyingi sana. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo kwa sasa hawezi kufanya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kusuasua kwake, tumetoa maelekezo, na mkandarasi huyu ameshakutana na viongozi wa *TANROAD* Makao Makuu, kwa maana ya viongozi wao wa juu kuhakikisha kwamba zile kazi ambazo zinaweza kufanyika zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ni muhimu zaidi pia kwa sababu barabara iliyokuwa inatumika, nyingine ameshaivuruga. Kwa hiyo, tumemhimiza ili aweze kuhakikisha kwamba zile *diversion* zote zinapitika na barabara iweze kukamilika kwa muda kama ilivyo kwenye mkataba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chomete, Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Barabara ya Musoma – Makojo – Busekera ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Je, ni lini sasa ujenzi huu utaendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ilishapata kibali cha kuanza kujengwa na tuko kwenye hatua za mwisho kabisa za manunuzi ili barabara hiyo iweze kuanza kujengwa.

**SPIKA:** Ahsante; Mheshimiwa Arif Premji.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara kwa kiwango cha lami Barabara ya Ziwani – Madimba – Msimbati – Madimba – Tangazo – Kilambo, kwani kupitia Kikao cha *RCC* jukumu hilo walipewa watu wa *TANROADS,* na ukizingatia *feasibility study* pia ilishafanyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge. Tunajua umuhimu wa barabara hiyo ambayo inaenda huko Msimbati. Sisi kama *TANROADS* tulishafanya upembuzi, tulishafanya usanifu na tulishapeleka maombi Wizara ya Fedha, ambao ninajua wanaandaa malipo, ili tuweze kupata kibali cha kuitangaza barabara hiyo. Hii pia ni barabara ambayo inakwenda Daraja la Kilambo ambalo tunashirikiana na wenzetu wa *Mozambique,* na vile vile wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Bajeti ya Mwaka 2025/2026 tulipitisha Barabara ya kutoka Kibaya – Kisima kilometa 50 zijengwe. Je, ni lini barabara hii inaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii tunategemea kupatikana kwa fedha. Tayari sisi tumeshaomba

fedha za awali ili mkandarasi aweze kulipwa, na akishalipwa, basi kazi hiyo ya kuanza kuzijenga hizo kilometa 50 itaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa upande wa Kanda ya Kaskazini kuanzia Tanga mpaka Singida, kipande korofi cha barabara ambacho kimerekebishwa mara nyingi zaidi ni kipande cha Dareda – Gehandu, kutoka Jimbo la Babati Vijijini kupitia Jimbo la Hanang – Singida. Barabara hii imeshakarabatiwa kwa muda mrefu na bado imekuwa ni sehemu korofi.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuanza upya kukwangua kipande kile cha barabara na kujenga lami mpya ili kusaidia uchumi wa Kanda ya Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kipande hiki cha Dareda – Gehandu ni kipande ambacho kiko kati ya Kateshi na Singida. Sisi kama Wizara tumeiangalia kama ni barabara ambayo imechoka, yaani imeshafika mwisho. Si hiyo tu, ni barabara ambayo sasa hivi baada ya kuwa na maboresho makubwa ya Bandari ya Tanga, magari yanayopita ni makubwa sana. Kwa hiyo, tumeiweka kuwa ni kati ya barabara ambazo zimewekwa kwenye mpango wa kuzitengeneza kwa matengenezo makubwa, kikiwepo hicho kipande cha Kateshi – Singida, ambapo kipande hicho alichokisema kipo hapo katikati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya Utegi – Shirati – Kirongwe yenye kilometa 56, kwa bahati nzuri kilometa 27 za Utegi – Shirati zilitangazwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Ninataka nipate *status, so far*

barabara ile sasa imefikia wapi kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hiyo barabara inasubiri tu kufanya *signing* tutakapokuwa tumekamilisha taratibu zote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Wilaya ya Liwale katika Mkoa wa Lindi wanatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha za ujenzi wa barabara ya kilometa 10 kwa Barabara ya Liwale – Nangurukuru. Barabara hii ina jumla ya kilometa 231. Pia barabra hii ndiyo kitega uchumi kikubwa sana kwa wanachi wa Liwale pamoja na wa Wilaya ya Kilwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais sifa moja kubwa aliyokuwa nayo ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa zaidi ya 100%, je, ni lini sasa tutafuta kilio cha wananchi wa Wilaya ya Liwale kwa kutukamilishia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ili sasa Wilaya ya Liwale iweze kuunganishwa na wilaya nyingine kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Lengo la Wizara, na kama alivyosema Awamu ya Sita ni kujenga barabara zote na hasa zinazounganisha barabara kuu na makao makuu ya wilaya ama makao makuu ya wilaya na makao makuu ya mkoa, ikiwepo hiyo Barabara ya Nangurukuru – Liwale kilometa 231.

Mheshimiwa Spika, tumeshaanza kutoa hizo kilometa 10, lakini kikubwa zaidi katika hiyo barabara Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami, kulikuwa na changamoto kubwa sana za madaraja. Sasa tumejenga madaraja mengi sana katika huu mpango wa dharura ambao unaendelea kukamilisha ili kuhakikisha kwamba wakati tunatafuta fedha ya kujenga barabara yote wananchi hawa wawe na uwezo wa kupita kipindi chote cha mwaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Barabara ya Katoma – Gera – Bukabuye – Kanyigo – Bukwali – Kashenyei imekuwa ikijengwa kwa meta mia mbili mia mbili, na sasa hivi ni miaka 10 tuko kilometa tano. Ninaishukuru Serikali imeshafanyia usanifu na upembuzi yakinifu, Mheshimiwa Naibu Waziri ameitembelea, na nimeshafikisha ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri. Je, ni lini angalau nitapata bajeti ya kutosha angalau kilometa 15 hadi 20 barabara hii ianze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko kwenye kipindi cha bajeti, kwa hiyo, tuombe bajeti itakapokuwa imepitishwa, nina hakika tutaongeza kilometa kutoka hizo meta 200 tutakwenda kwenye kilometa nyingi zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo. Waheshimiwa ninawapa muda mwingi kwa sababu ninajua umuhimu wa barabara, lakini siyo wote tutaweza kupata nafasi. Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Barabara ya Mbande – Kisewe – Msongola, je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hii barabara ilikuwa inasuasua na kimsingi ni kama ilikuwa imesimama. Mkandarasi tumeshamlipa na hatudai sasa hivi, na nina hakika tutahakikisha tunamsimamia ili aweze kukamilisha hizo kilometa ninadhani ni 3.8 kwa muda wa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwelekeze tu Meneja wa Mkoa wa Dar es Salaam aweze kuisimamia hiyo barabara ili tuweze kumaliza, maana yake ndiyo iliyokuwa imebaki kuwa na kipande cha barabara ambayo ni vumbi katika hiyo barabara kuja Chanika.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 28

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nane Kibaha – Chalinze**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza: -

Je, ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kibaha Maili Moja hadi Chalinze umefikia katika hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya kutoka Kibaha Maili Moja hadi Chalinze umegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ya kutoka Maili Moja – Picha ya Ndege yenye urefu wa kilometa 3.6 kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa sehemu hiyo ipo katika hatua za mwisho. Usanifu utakapokamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sehemu iliyobaki ya kutoka Picha ya Ndege – Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9 itatekelezwa kwa njia ya

ubia kati ya Serikali na sekta binafsi *(PPP)*. Kwa sasa taratibu za manunuzi ya kumpata mbia zinaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri, ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze imekuwa na foleni kubwa sana isiyomithilika, tena ni ya mara kwa mara. Je, ni upi mkakati wa muda mfupi wa Serikali kuhakikisha tunamaliza kadhia hiyo ya foleni?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Fursa ya mageuzi makubwa ya Bandari yetu ya Dar es Salaam imesababisha usafirishaji wa mizigo mingi kupitia Barabara hii ya Morogoro na kusababisha foleni kubwa sana. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa *Chalinze – Morogoro Express Way*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali mawili ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, mhusika.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye swali la kwanza na katika swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Pwani linalohusu Kibaha – Chalinze.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu mkakati wetu wa muda mfupi, tumekubaliana katika Wizara ya Ujenzi kwamba, tunayo

barabara ya zamani ambayo mara baada ya kutengeneza barabara mpya tuliiacha. Tumepata fedha Serikalini tunaitengeneza kuwa ni barabara mbadala ili kusudi barabara kuu inapofunga, watu wawe na uwezo wa kupita katika barabara ile ya zamani inayoanzia Kibaha Maili Moja – Tumbi inakuja kutokea mpaka Mlandizi na kusonga mbele. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tunashirikiana vyema na wenzetu wa Jeshi la Polisi, tumeweka vikosi maalumu kabisa, kwa sababu barabara hii changamoto yake kubwa ni gari zinapoharibika ambazo zinaleta msongamano mkubwa. Kwa hiyo, vikosi vyetu vya *TANROADS* na Polisi vinashirikiana kwa pamoja, na hivi sasa kila linapotokea tatizo la namna hiyo, mara moja vikosi vile vinafanyia kazi na kuondoa lile gari lililoharibika na hatimaye kuruhusu barabara kuweza kupita.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu ni lini tutafanya sasa kazi ile ya Barabara ya *Kibaha – Chalinze – Morogoro Express Way*, tunashukuru sana kwa miongozo mikubwa na mizuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hivi ninavyokwambia tulichelewa hatua ya kwanza kwa sababu ya mkandarasi ambaye tuliingianaye katika mazungumzo, *terms* zake zilionekana kuwa hazina maslahi mapana kwa Taifa letu. Kwa hiyo, tumetangaza upya, na habari njema ni kwamba tumepata mpaka mashirika yetu ya ndani ikiwemo *NSSF*, *TPA*, walioonesha nia ya kuingia katika mradi huu mkubwa wa kielelezo na wa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, timu za wataalamu wa Serikali, wako kazini wakichambua ikiwa ni pamoja na haya mashirika ya nje. Muda siyo mrefu tutakuwa tumepata atayekwenda kutekeleza kazi ile.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Cornel Magembe.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b). Kwanza ninapenda kujua Barabara ya kutoka

Nyamirembe – Ichwankima – Kasenga – Biharamulo yenye zaidi ya kilometa 50, itaanza kujengwa lini, kwa sababu imekuwa ikiwekwa kwenye mpango wa ujenzi, lakini utekelezaji wake umekuwa haufanyiki?

Mheshimiwa Spika, la pili, ...

**SPIKA:** Ah, ah, swali ni moja tu.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari ameshafika ofisini kwa ajili ya kuulizia hiyo barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulishafanya usanifu, na katika mwaka wa fedha uliopita ilikuwepo kwenye bajeti. Nimhakikishie kwamba barabara hii tutaiweka kwenye bajeti kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, kwa sababu tayari pia wenzetu wa uchukuzi wameshajenga bandari pale Nyamirembe ambayo sasa bila hiyo barabara itakuwa haina maana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ibrahim Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Barabara ya Maili Sita – Kiboriloni ujenzi wa njia nne utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tupo kwenye hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kuianza hiyo barabara, kwa sababu ni barabara ambayo inaanzia Tengeru inakwenda Kikafu – Maili Moja – Kiboriloni kwa njia nne. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko kwenye hatua za mwisho kabisa ili barabara hiyo ianze kujengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nuru Issa.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza linalohusiana na lini Serikali itajenga Daraja la Mto Malagarasi kule Ilagala? Pia ni lini Serikali itajenga Barabara kutoka Simbo – Kalya ili kuwanusuru wananchi wa Sunuka, Herembe, Mwakizega, na Buhingu?

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu pale tuna Hifadhi ya Mahale, kwa hiyo, inasababisha watalii kupata usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba jibu kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Malagarasi maarufu kama Malagarasi Chini ambalo liko kwenye Barabara ya Simbo – Ilagala – Kalya ni daraja ambalo tumeshakamilisha usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo daraja lipo, tutalihamisha, tutalipandisha kwa juu. Tumeshakamilisha usanifu, tupo tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa *World Bank* kupitia utaratibu wa *CRW* ili tuweze kulijenga daraja hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Kakulu Kakulu.

Na. 29

**Upanuzi wa Barabara ya Kilwa**

**MHE. KAKULU B. KAKULU** aliuliza: -

Je, lini upanuzi wa Barabara ya Kilwa kuanzia Mbagala Rangi Tatu – Kongowe unatarajiwa kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* iliingia mkataba na Mkandarasi *M/S STECOL Corporation* kwa ajili ya upanuzi wa Barabara ya Kilwa kuanzia Mbagala Rangi Tatu – Kongowe yenye urefu wa kilometa 3.8. Mkataba ulisainiwa tarehe 19 Agosti, 2025 na utatekelezwa kwa muda wa miezi 15. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika mwezi Novemba mwaka huu 2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakulu.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwanza kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbagala kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali anayoiongoza kwa kutusaidia kujenga ile barabara. Kwa kweli ilikuwa ni changamoto kubwa, ilisababisha msongamano mkubwa na ajali nyingi katika Kilima kile cha Mto Kizinga. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri, swali moja tu la nyongeza. Ninafahamu na wote tunajua umuhimu wa barabara inayounganisha pale Kongowe kutoka Kongowe kuelekea Kivukoni katika Jimbo la jirani la Kigamboni, na umuhimu wake hasa katika kulisha viwanda vilivyopo Kigamboni katika eneo la *Kisarawe II* na viwanda vilivyopo katika eneo la Mwandege pamoja na eneo la Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inaona umuhimu pia wa kupanua hii barabara kutoka Kongowe kwenda Kigamboni ili kusaidia kuhudumia hivi viwanda na shughuli nyingine za wananchi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, kwa kutambua kazi kubwa ambayo anaifanya na hasa kuondoa changamoto ya msongamano wa barabara kwenye eneo hilo ikiwa ni pamoja na kulijenga hilo daraja la Mzinga ambalo muda siyo mrefu tunaanza kulijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, hii barabara ya Kongowe kwenda Kivukoni ipo kwenye mpango wa kuondoa misongamano *(decongestion)* ya miji ikiwepo Mji wa Dar es Salaam ikiwepo pamoja na hiyo barabara ya Kongowe – Kivukoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali inaenda kupanua barabara ya Tanga – Segera - Chalinze na hasa ukizingatia sasa hivi kumekuwa na msongamano mkubwa wa malori kwenye barabara hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Kaskazini ambayo ni *T-2*, kuanzia Chalinze kwenda Segera – Tanga, lakini hata kwenda Korogwe ni barabara ambazo zilijengwa zamani na ni finyu.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa hivi ni kuifanyia usanifu ili iweze kufanyiwa matengenezo ama ukarabati mkubwa ikiwa ni pamoja na kuipanua na tunatambua kwa kweli kulingana na kazi zinazofanyika sasa hivi na Awamu ya Sita, magari yameongezeka na magari makubwa sana yanapita kwenye hizo barabara. Kwa hiyo, tuna kila wajibu wa kufanyia marekebisho barabara zetu ikiwepo na hiyo barabara ya Segera - Tanga.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Afya, Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme.

Na. 30

**Huduma kwa Watoto Njiti**

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua wigo wa huduma za Watoto Njiti katika Vituo vya Afya vya Mkoa wa Tabora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya kibali alichonipatia kusimama mbele hapa. Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua ili niweze kumsaidia katika nafasi hii ya Unaibu Waziri. Pia, niwashukuru wananchi wa Muhambwe kwa kuendelea kuniamini ili niweze kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho siyo kwa umuhimu, ninaishukuru familia yangu ambayo imeendelea kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote cha safari yangu ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Mndeme, Mbunge Viti Maalum, kutokea Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za watoto njiti kwa Mkoa wa Tabora ambapo Hospitali ya Kitete imetengewa shilingi bilioni 4.5, Nzega *TC* shilingi milioni 460, Urambo *DC* shilingi milioni 460, na ujenzi huu unatarajiwa kuanza mapema Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imepanua wigo wa huduma za watoto njiti katika Mkoa wa Tabora kwa kutenga

vyumba maalum katika vituo vya kutolea huduma za afya, ambavyo vimewekewa vifaa kwa ajili ya kutoa huduma za watoto njiti kutoka vituo sifuri mwaka 2018 hadi kufikia vituo 33 mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuboresha Sekta ya Afya. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zimekuwepo changamoto ambazo huwapata baadhi ya wakinamama ambao baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali kukosa uelewa thabiti wa kuendelea na malezi ya mtoto njiti mara wanaporudi nyumbani. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya malezi kwa wakinamama wanapokuwa wamerudi nyumbani ili aendelee kumlea vizuri mtoto anapokuwa nyumbani ili kupunguza uwezekano wa kutokea vifo vya mtoto njiti anapokuwa nyumbani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, kuna utafiti wowote umefanyika ili kupunguza hili tatizo la watoto kuzaliwa kabla ya muda na kama utafiti huo umefanyika, je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu hii kwa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kutoka Tabora kwa jinsi ambavyo anawapigania wanawake wa Tabora ili waendelee kupata watoto waliozaliwa njiti na kuwa salama. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imeweka mwongozo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakinamama hawa wanapokwenda nyumbani ili elimu hii itolewe kwa mtiririko.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wanaozaliwa njiti ikumbukwe kwamba viungo vyao ambavyo vinawasaidia wao kuishi ikiwemo ini, mifupa, Ngozi, vyote navyo vimezaliwa vikiwa havijakomaa. Hivyo, msingi wa elimu hii ni kuwasaidia waweze kujua jinsi ya kuwakinga, waweze kuwalinda na wale watoto wawe salama ikiwemo kwanza kabisa, kuwasaidia kuwapatia joto.

Mheshimiwa Spika, elimu tunayowapatia ni kuendelea kufanya mamakangaroo ambapo mama huyu anatakiwa kumlea huyu mtoto wakati wote huku amemweka kifuani na akiendelea kupata joto la mama kwa kushikana ngozi kwa ngozi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunaendelea kumfundisha huyu mama umuhimu wa kumnyonyesha ziwa la mama ambalo lina faida zaidi ya chakula. Mtoto huyu amezaliwa akiwa kinga yake pia ipo chini. Kwa hiyo, kwa kumnyonyesha ziwa la mama inamsaidia pia huyu mtoto aweze kupata kinga ili aepukane na magonjwa. Pia, kwa vile huyu mtoto njiti amezaliwa bila ya kuwa na kinga, tunamfundisha mama aendelee kumtenga huyu mtoto na watu wengine ili asiweze kupata maambukizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunamfundisha huyu mama jinsi ya kuendelea kumpatia huyu mtoto chanjo pale muda utakapofika ili asiweze kupata maambukizi. Tunaendelea kumwambia huyu mama amlete mtoto kliniki kwa kufuata tarehe tulizompangia ili tuweze kuendelea kumpa elimu zaidi, na vile vile kuendelea kumpatia huyu mtoto huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho siyo kwa umuhimu, tunamfundisha dalili zote hatarishi ikiwemo kama kubadilika rangi mtoto, kuwa manjano, maana ini pia halijakomaa ikiwepo dalili ya mtoto kushindwa kupumua kwa sababu mapafu pia hayajakomaa na dalili yoyote ya hatari ambayo akiiona tu basi afike hospitalini haraka ili aweze kupata ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua kama kuna utafiti wowote umefanyika. Zipo tafiti nyingi

zimefanyika Kitaifa na Kimataifa, lakini pia Shirika la Afya Duniani, limefanya tafiti na kuona kwamba watoto wanaozaliwa njiti wanaongezeka kila mwaka na tafiti zimeonesha kwamba watoto hawa wanaongezeka kila mwaka kwa 10% mpaka 15% kwa watoto wanaozaliwa. Mfano, watoto wanaozaliwa Tanzania kwa mwaka ni kati ya watoto 1,900,000 mpaka 2,200,000. Kwa hiyo, tuna watoto 250,000 mpaka watoto 300,000 kwa mwaka ambao ni njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la (b) kwamba kama tumefanya tafiti, je tumetoa elimu? Serikali kupitia Wizara ya Afya, tumeendelea kutoa elimu kwa wamama wote wajawazito pale wanapofika kliniki. Maana matatizo yanayosababisha watoto kuzaliwa kabla ya wakati, yapo ambayo yanaweza kuzuilika ikiwemo maambukizi ambayo yanaweza kuleta homa kama vile Malaria, *UTI*, *Pneumonia* na mengine ikiwemo kiasi kidogo cha damu kwa mama mjamzito kinaweza kuleta kuzaliwa mtoto njiti, magonjwa sugu kama vile kisukari na shinikizo la damu kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni visababishi ambavyo mama akifika mapema, basi tunampa elimu ili tumtibu vizuri ili asiweze kujifungua mtoto ambaye hajatimia. Vipo visababishi ambavyo huwezi kuvizuia kama vile kuwa na mimba ya watoto mapacha. Tunawashauri wamama wafike mapema ili tuwape uangalizi wa karibu ili kuzuia wasiweze kujifungua watoto njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas.

Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ukaenda.

Na. 31

**Mradi wa Maji Dambiya - Mbulu Vijijini**

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Mradi wa Maji wa Dambiya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwepo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa heshima kabisa na unyenyekevu nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini ili niweze kumsaidia kazi kama Naibu Waziri wa maji kwa kipindi hiki cha Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Dambiya - Haydom uliopo Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya mashine, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 373, ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 2,575,000, ujenzi wa vituo 192 vya kuchotea maji vyenye dira za malipo ya kabla, sambamba na ujenzi wa mbauti nne za kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Dambiya - Haydom umefikia wastani wa 45% za utekelezaji na unatarajiwa kumalizika mwezi Novemba, 2027. Mradi huo unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi 133,737 waishio katika vijiji 21 kwa wilaya ya Mbulu utakapokamilika. Serikali itahakikisha inapeleka fedha za utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa chanzo hiki cha maji cha Dambiya kina maji ya kutosha na kitakwenda kuhudumia zaidi ya vijiji 21, tuna mji wa Dongobesh ambao ni Makao Makuu ya Halmashauri, una hospitali ya halmashauri, una kituo cha afya na vilevile una shule za sekondari mbili na shule za msingi tano. Mji huu sasa hivi hauna maji na unapata mgao wa maji angalau mara mbili....

**SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani kuweza kuvuta maji kutoka chanzo hiki ambacho ni chini ya kilometa saba na matanki yapo katika mji huu ili kuweza kuwasaidia wananchi hawa ambao wana tatizo la maji na huduma ziweze kuendelea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza. Tunao mradi katika Kijiji cha Qaloda Kata ya Dongobesh ambao sasa Kijiji hiki kina kaya 386 na mradi huu umekwama kwa zaidi ya miaka miwili, na una mabomba pale. Je, Serikali ina mpango gani kukamilisha mradi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Dkt. Emanuel, Mbunge wa Mbulu Vijijini. Ni kweli kabisa mradi huu ambao unatekelezwa wenye gharama ya shilingi bilioni 41.2 ambapo Serikali mpaka sasa imeshamlipa mkandarasi takribani shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Spika, mradi utakapokamilika utaweza kuhakikisha kwamba vijiji 76 vya Mbulu Vijijini vitakuwa vimepata huduma ya majisafi na salama. Vilevile, katika vijiji ambavyo vimebaki, ndani ya nchi yetu kati ya vijiji 12,318 ni vijiji 1,575 tu ambavyo vimeshabaki,

ambapo miradi zaidi ya 3,714 vyenye gharama ya shilingi trilioni 1.8 vimeshakamilika na miradi 878 inayoendelea yenye gharama ya shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika miradi inayoendelea pamoja na huu ambao amesema kwamba unasuasua, tunaenda kuhakikisha mradi huo unakamilika na wananchi wake wa Mbulu Vijijini wanapata huduma ya majisafi na salama.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 32

**Uhitaji wa Maji Kijiji cha Kapalala**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Maji ya mserereko katika Kijiji cha Kapalala Kata ya Kapalala - Nsimbo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa maji kwa wananchi wa Kijiji cha Kapalala Kata ya Kapalala kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Wilayani Mpanda. Kijiji hicho kwa sasa kinapata huduma ya maji kupitia visima vitatu vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita 23,742 kwa siku wakati mahitaji ya wananchi wa kijiji hicho ni lita 72,675 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa kutumia chanzo cha maji ya mserereko cha Ikolongo ambapo unatarajia kunufaisha vijiji tisa Wilayani Mpanda kikiwemo Kijiji cha Kapalala. Kwa sasa

Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo unaotarajia kugharimu takribani shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa visima viwili havifanyi kazi kabisa, kisima kimoja kinatoa maji ya kusuasua na wananchi wa Kapalala wana adha kubwa ya maji, ni nini mikakati ya Serikali kuhakikisha vile visima viwili vinatoa maji kwa dharura ili wananchi wa Kapalala waweze kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa maji ya mserereko mpaka sasa hivi kwenye bajeti mpango haupo, je, katika bajeti ijayo ya Serikali mpango huo utawekwa ili wananchi wa vijiji vyote saba waweze kupata manufaa ya majisafi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeza sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatetea wananchi wake wa Jimbo lake la Nsimbo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, kwanza upatikanaji wa huduma ya maji katika Jimbo la Nsimbo kwa sasa ni 74% na ninafahamu mradi huu utakapokamilika utaweza kusaidia kutoka vijiji 23 vinavyopata huduma ya maji, lakini katika vijiji tisa ambavyo vitahudumiwa na huu mradi, vijiji vitano vina huduma ambayo inasuasua, na ni vijiji vinne ndivyo ambavyo hawana huduma ya maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kuwa huu mradi tunaenda kuhakikisha kwamba unakamilika. Pia huu mradi wa mserereko tunaenda kuuingiza kwenye bajeti ya fedha ya

2026/2027 ili kuhakikisha wananchi wake wanaendelea kupata huduma ya majisafi na salama, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea. Mheshimiwa Profesa Lazaro Ndalichako.

Na. 33

**Mradi wa Maji Mwanga B**

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Mwanga B – Kasulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji Mwanga B uliopo Mji wa Kasulu mkoani Kigoma ambapo hadi sasa Mkandarasi ameshapeleka mabomba yote ya mradi yenye urefu wa jumla ya kilometa 52 eneo la mradi. Kazi nyingine zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kubadili mfumo wa nishati ya umeme wa jua kwenda umeme wa gridi kwa ajili ya uzalishaji maji sambamba na ujenzi wa chemba za ukaguzi wa mitambo ya mabomba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahakikisha inapeleka fedha za utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi waishio katika mitaa sita ya Mwanga B, Mganza, Msambala, Nyachidima, Kimombwa na Kigondo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Pia, ninaomba nitumie nafasi hii kuishukuru kwa dhati Wizara ya Maji kwa namna ambavyo inafuatilia miradi katika jimbo langu kwa sababu kule hali bado ni tete.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza. Kwa kuwa mabomba hayo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyazungumza yenye urefu wa kilometa 52 yalipokelewa tangu mwezi Mei, 2025, je, ni lini hasa Serikali itaendelea na utekelezaji wa awamu zinazofuata ili wananchi hawa wa Mwanga, Nyachidima, Kabanga, Nyalumanga, Kimombwa pamoja na Kidiama waweze kunufaika kwa sababu wanapata adha kubwa ya maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini, kwa kazi kubwa ambayo anatupatia ushirikiano mzuri sana tunapofanya ziara katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwahakikishia wananchi kutoka mitaa hii sita: Mwanga B, Mganza, Msambala, Nyachidima, Kimombwa na Kigondo, kuwa mradi huu wenye gharama ya shilingi bilioni 2.9, tayari mabomba yameshafikishwa eneo la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kupeleka fedha kwa ajili ya kwenda kumalizia mradi huu ili wananchi wa mitaa hii waweze kupata huduma ya majisafi na salama sambamba na kuongeza upatikanaji wa maji ambao kwa sasa kwa Kasulu Mjini ni 71%, na sambamba na mradi wa miji 28 ambao unaendelea pale Kasulu utafikisha huduma ya maji kufikia 95%.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

Na. 34

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Mwibara**

**MHE. KANGI A. LUGOLA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Mradi mkubwa wa Maji katika Jimbo la Mwibara utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda vijiji 30 vya Jimbo la Mwibara Wilayani Bunda. Miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* na mtambo wa kutibu maji *(treatment plant)* mwenye kuzalisha lita milioni 35.7, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(booster station),* ujenzi wa matanki 10 yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 19.3, ulazaji wa mtandao wa bomba zaidi ya umbali wa kilometa 500, ujenzi wa mbauti 30 za kunyweshea mifugo, ujenzi wa vituo 124 vya kuchotea maji sanjari na maunganisho kwa wateja 5,000 wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza utekelezaji wa mradi huo unaotarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 94 ambapo utanufaisha zaidi ya wananchi 200,000 wa Jimbo la Mwibara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niishukuru Serikali ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kuona umuhimu wa kuwapa maji Wanamwibara wapatao 200,000. Sasa kwa kuwa usanifu ulishakamilika zaidi ya miaka mitatu sasa, na kwa sababu usanifu ni chanzo cha kujenga matumaini kwa wananchi kupata

maji, kwa nini, sasa Serikali baada ya kuona utafutaji wa fedha kwa wafadhili unachukua muda mrefu, kwa nini, wasitenge bajeti kwenye fedha za Serikali ili waanze kujenga mradi huo awamu kwa awamu ili matumaini yaliyojaa kwa Wanamwibara yasije yakapotea?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa mradi huu umechelewa na wananchi wa Mji wa Kibara ambapo ni makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda Vijijini ni mradi ambao una changamoto nyingi mabomba kupasuka, wakati mwingine mitambo haiwaki.

Mheshimiwa Spika, je, uko Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari baada ya Bunge hili Tukufu litakapoahirishwa kuja Mwibara na ikiwezekana kwenda nami mguu kwa mguu ili akajionee changamoto za mradi huu ili wananchi wapate maji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nianze na swali la pili. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, daima imekuwa ikihakikisha kwamba inafika maeneo ya changamoto ili kujionea ukubwa wa namna ambavyo wananchi wanahangaika.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, niko tayari kwenda na Mheshimiwa Kangi Lugola, mguu kwa mguu kwenye Jimbo lake la Mwibara kuhakikisha kwamba tunatoa kauli ya Serikali baada ya kujiridhisha na changamoto za tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni ushauri ambapo Mheshimiwa Mbunge ameshauri tuweke katika bajeti ya Serikali. Ni kweli kabisa kwa sasa sekta ya maji tunakuja na kitu kinaitwa *alternative financing,* maana yake hatuwezi kutegemea fedha za wadau pekee yake, lakini pia hatuwezi kutegemea fedha za Serikali pekee yake. Tunatoa fursa kwa wadau wengine ambao wanaweza kuingia kwenye sekta ya maji tukashirikiana kwa mfumo wa *PPP*.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba kuna njia nyingi ambazo tunakwenda kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba mradi huu lazima uzingatie maslahi na uzingatie sera yetu ya Maji ya 2002 toleo la mwaka 2025 kwenye *security* ya maji ambao hatuwezi kwenda kichwa kichwa ku-*engage private sector* bila kuwa na tahadhari, lakini tutaendelea kuangalia namna gani tutafanya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kulikuwa na uhaba mkubwa sana wa maji Dar es Salaam kwa kipindi kirefu sana, lakini *bill* zinakuja kama kawaida. Shida ni nini? Kalifanyie kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jinsia, Mheshimiwa Tarimba.

Na. 35

**Sharti la Watoto Kutunza Wazazi Wasiojiweza**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka Sharti la Kisheria la Watoto wakubwa kutunza wazazi wao wasiojiweza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku ya leo, lakini pili ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoionesha juu yangu kwa kuendelea kuniteua kama Naibu Waziri, wakati huu kwa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wanawake na Makundi Maalum ili niweze kumsaidia *Field Marshal* wetu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nijielekeze kwenye swali. Serikali inatambua umuhimu wa familia na jamii kuchukua jukumu la kulea wazee, na huu ndiyo msingi wa mila na desturi zetu Watanzania. Jukumu hili ni msingi unaojengwa katika hatua za awali katika malezi na makuzi ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma na matunzo kwa wazee, Serikali imefanya mapitio na kutunga Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024. Sera hiyo inatoa wajibu kwa familia na jamii kusimamia matunzo ya wazazi. Sera hii imeweka msisitizo wa kuimarisha mfumo wa kisheria utakaolinda na kuendeleza wazee ambao pamoja na mambo mengine, utawezesha uwajibikaji wa jamii na watoto kuwatunza wazee wao. Kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua ya kuwashirikisha wadau ili kutoa maoni juu ya umuhimu na masuala muhimu ya kuzingatiwa katika sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa wito kwa wazazi kuwekeza kwenye malezi ya watoto na siyo matunzo peke yake, kwani inaendeleza ukaribu na muunganiko imara kati ya wazazi na watoto. Mzazi anapobeba jukumu la malezi na matunzo ya watoto wake kikamilifu, hujenga msingi imara kwa mtoto kumhudumia mzazi wake anapozeeka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Wajibu wa kisheria wa kuwalea wazazi kwa maana ya wazazi wasio na uwezo katika nchi nyingine wanaita *Filial Responsibility Laws,* maana yake ni kwamba hizi sheria siyo ngeni.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kwenda kupata uzoefu kwenye nchi ambazo zina sheria kama hizi ili kuzileta nchi zikatumika kwa minajili ya kusaidia wazazi wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, twende kwenye swali.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, swali la pili, sioni kama kuna mizania. Zipo sheria zinazolazimisha wazazi kulea watoto wao, lakini hakuna sheria zinazolazimisha watoto kuwalea wazazi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimwulize Waziri, haoni kwamba kuna uharaka sasa wa kuleta hiyo sheria Bungeni ili tuweze tukaijadili? Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Tarimba Abbas kwa maswali mazuri ya kujenga. Kama nilivyoweza kujielekeza kwenye jibu langu la msingi, nianze kujibu hapa umuhimu wa kwenda kujifunza, tuko tayari na tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu inatembea nchi mbalimbali kuendelea kujifunza. Vilevile hii sera ambayo tumeirekebisha mwaka 2024 tukiizingatia ina majibu sahihi kwa nchi yetu na jamii kuona umuhimu wa vijana wetu kulea wazee wao wasiojiweza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, uharaka wa kuleta jambo hili Bungeni, tutaendelea kuona mchakato uliopo wa wadau kukusanya maoni, na kuona namna njema ya kuhakikisha wazee hawa wanaendelea kupatiwa matunzo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye sera yetu tumeelekeza namna wazee hawa pia tunawashirikisha. Hivyo, nipende tu kusema tutaendelea kukusanya maoni kwa wadau pamoja na Bunge letu Tukufu. Tutaendelea kuomba ushirikiano wenu kuhakikisha wazee

wote wanapata matunzo kwa sababu wao ni tunu, wamefanya mengi kwenye nchi, wanastahili heshima na matunzo salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Getere.

Na. 36

**Kulipa Kifuta Jasho Vijiji vya Jimbo la Bunda Vijijini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Wananchi walioharibiwa mazao yao na Tembo katika Vijiji vya Jimbo la Bunda watalipwa kifuta jasho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ililipa kifuta jasho na machozi jumla ya shilingi 311,160,000 kwa wananchi 1,115 wa Wilaya ya Bunda. Aidha, Wizara imekamilisha uchambuzi wa madai ya kifuta jasho na machozi ambapo shilingi 524,122,500 kwa wananchi 1,603 wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda zitalipwa. Kwa sasa Wizara inakamilisha taratibu za malipo hayo ili wananchi husika walipwe stahiki zao kwa mujibu wa Kanuni kupitia mfumo wa kieletroniki ujulikanao kwa jina la *Problem Animal Information System – (PAIS)*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mfumo huu mpya kwa sasa, Serikali itaendelea kulipa wananchi ambao hawana *account* au namba za siku kwa kutumia utaratibu wa awali ambapo wataalamu hufika uwandani kufanya malipo hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta, Kyandege, Tingirima, Nyangere na Kambugo wameahidiwa kulipwa toka mwezi wa Novemba, je, Serikali kwa siku za karibuni sasa, ni lini watalipwa fedha zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Naibu Waziri amezungumza vizuri kwamba sasa wameleta mfumo mpya wa kuwalipa watu kupitia akaunti zao za benki na kwenye simu. Wanajua katika nchi yetu tuna matatizo ya *NIDA*? Mtu anaweza kusajili watu wawili, watatu. Sasa huo mfumo wa kwenda kuwalipa watu kwa kutumia mtindo wa zamani, wako tayari kwenda kuelimisha watu juu ya jambo hilo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, ninaomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati wowote kuanzia sasa, kwa sababu mchakato umeshakamilika, wananchi waliopata madhara hayo wataenda kulipwa stahiki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba pamoja na mfumo wetu mpya tulionao wa kisasa tunaenda kurejea mfumo ule wa zamani wa kufika uwandani kuwalipa wananchi stahiki zao na kabla ya kuwalipa tutaendelea kutoa elimu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amependekeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Surati.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameendelea kuyatoa. Pia nilikuwa ninaomba wananchi wa Jimbo la Seregenti wanaomba

kufahamu, ni lini Serikali itaanza kutoa fidia stahiki inayoendana na hasara wanazopata wananchi wanaoathirika na Wanyamapori? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa fidia stahiki kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi hawa wataendelea kupata fidia ambazo wanastahiki, na kwa sasa hakuna mtu yeyote ambaye atakosa haki yake ya msingi.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Madini, Mheshimiwa John Stephano Luhende.

Na. 37

**Usajili wa Bodi ya Wanajiolojia Nchini**

**MHE. JOHN S. LUHENDE** aliuliza:-

Je, lini usajili wa Bodi ya Wanajiolojia nchini utakamilika ili kulinda na kuongeza ufanisi katika shughuli za utafiti na uchimbaji madini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na hatua za uanzishwaji wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Jiosayansi Tanzania *(Tanzania Geoscientists Registration Board),* kwa kifupi itajulikana kama *(TGRB).*

Taratibu ambazo zimeshatekelezwa ni pamoja na uandaaji wa rasimu ya Waraka wa Mapendekezo ya Baraza la Mawaziri, kuhusu kuanzishwa kwa bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Wizara ya Madini ipo katika hatua ya ukusanyaji wa maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau kuhusu masuala mbalimbali likiwemo suala la kuainishwa kwa vyanzo vya mapato vitakavyohakikisha bodi pendekezwa inaweza kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa maoni kutoka kwa wadau kukamilika, Wizara itawasilisha waraka huo kwenye ngazi za maamuzi za Serikali ikiwa ni pamoja na ngazi ya kikao cha kitaalamu cha Makatibu Wakuu *(IMTC)* na kikao cha Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kujadiliwa na kupata ridhaa ya kuanzishwa rasmi kwa bodi hiyo kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhende.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya mara ya pili. Suala hili la usajili ya Bodi ya Wajiolojia limeanza kushughulikiwa na Wizara tangu mwaka 2017 na limekuwa ni tatizo sugu sana kwa muda mrefu na viongozi mbalimbali wa Serikali ikiwemo Waziri Mkuu, Mawaziri mbalimbali wameweza kuhudhuria makongamano ya taasisi hii tunayotarajia kuisajili ya hawa wataalamu wa kijiolojia.

Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi, sasa hivi kama Serikali tunaelekea kufanya utafiti nchi nzima kwa kurusha *drone* mbalimbali pamoja na njia nyingine za utafiti. Sasa Serikali imejipangaje kuhakikisha katika utafiti huo hatupati *data* za uongo kwa kuwa tunaenda kwenye utafiti tukiwa hatuna Bodi wa Wajiolojia ya kusimamia ubora wa taarifa hizo za kijiolojia pamoja na *policy*...

**SPIKA:** Mheshimiwa, twende kwenye swali.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na vishoka wengi sana mtaani wanaendelea kutapeli wachimbaji wadogo wakijiita wao ni wataalamu wa kijiolojia. Serikali imejipangaje kuthibiti hili tatizo kwa sababu tunaendelea na shughuli za madini, lakini hatuna bodi ambayo inasaidia kuondoa hili tatizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Luhende, Mbunge wa Bukene kwa sababu ya maswali yake kuhusu hii bodi ambayo imesubiriwa kwa muda mrefu. Pili, nitambue kwamba Jimbo lake la Bukene ni moja ya maeneo yetu ya madini ya dhahabu, kwani yanapatikana pia huko kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ubora wa *data* inayotafutwa katika tafiti zinazoendeshwa na Taifa hili kwa maelekezo ya mama, Mheshimiwa Dkt. Samia zinasimamiwa kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwajulisha Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba kati ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini kongwe na yenye uzoefu wa hali ya juu na wataalamu wanaojitosheleza ni Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ijulikanayo kama *GST*. *GST* imeanzisha mwaka 1925 ina miaka 101 sasa na ndiye msimamizi mkuu wa tafiti hizi zinazokwenda kufanyika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika tafiti yoyote kubwa inayokwenda kufanyika na inayofanyika, kunakuweko na mshauri mwelekezi mtaalamu anayetoka katika kampuni ya Kimataifa yenye uzoefu ambaye ndiye anayefanya kazi mbili za muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kwanza, anafanya kitu kinachoitwa *quality assurance* kuhakikisha kwamba *data* inayokusanywa ina vigezo vyote vya ubora wote unaotakiwa, lakini pia anafanya *quality control* kuhakikisha kwamba *data* inayokusanywa imesimamiwa itoe majibu yanayotarajiwa. Isitoshe katika kuhakiki

hiyo *data* na kuikamilisha Taasisi ya *GST* ndiye *custodian,* ndiye anayetunza *data* zote kwa ajili ya walaji wawekezaji wakubwa, na wawekezaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili la vishoka, ninaomba tena niseme hapa kwamba *GST* pamoja na *STAMICO* ambaye ndiye mlezi mkuu wa wachimbaji wadogo ambao ndio wanaumizwa sana na hawa vishoka, wana *mandate* na jukumu la kuwasimamia wachimbaji wadogo. Nitoe wito kwamba wasiwatumie wanajiolojia ambao hawajahakikiwa na *GST* kwa sasa wakati ambapo hatuna bodi.

Mheshimiwa Spika, kazi ya *GST* ni kutoa ushauri, ni kusaidia kupima sampuli, na pia ina watalaamu wanaoweza kutumiwa. Kwa hiyo, unapomchukua ambaye sio wa Serikali, pitia *GST* uliza kama huyu mtu anafaa?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kwa sababu hili suala lake ni la muhimu sana, ninaomba tu nitoe wito kwamba kwa kuwa bado bodi hii haijasajiliwa, na sisi pia tuko nyuma yao kuwasukuma wasajiliwe. Bodi hii itakaposajiliwa, kazi yao siyo kuhakiki *data,* wala ubora wa *data,* kazi yao ni kuwadhibiti wa jiosayansi ambao wamesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, hiyo bodi wanapokwenda kufanya kazi yao, wawe na sifa, na Watanzania watakwenda kuwatumia hao sasa katika tafiti zao. Wakishasajiliwa, usimchukue mtu ambaye hajasajiliwa na bodi hii ambayo inakwenda kuanzishwa siku za karibuni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo uliza swali.

Na. 38

**Kuongeza Maeneo ya Malisho ya Mifugo**

**MHE. YANNICK I. NDOINYO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza maeneo ya malisho kutoka hekta milioni 3 mpaka 6 kama Ilani ya CCM inavyosema?

**SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kutekeleza maelekezo yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025/2030 na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa kufungua rasmi Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe 14 Novemba, 2025 kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaongeza maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa shughuli za ufugaji kutoka hekta milioni 3.49 hadi hekta milioni sita.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi zenye majukumu ya kisheria ya kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi, tumeanza kuandaa mkakati wa miaka mitano wa kutenga hekta milioni 2.51 kwa ajili ya shughuli za ufugaji. Wakati wa utekelezaji wa mkakati huu, Waheshimiwa Wabunge wote watashirikishwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yannick.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sekta hii ya ufugaji inaathirika sana na mabadiliko ya tabianchi, je, Serikali inaweza kuchukua hatua zipi za dharura kuwaandaa wafugaji kabla na wakati wa nyakati za ukame ili wasipoteze mifugo yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, ni mikakati gani Wizara inaichukua kuwatembelea na kuwaandaa wadau pamoja na wafugaji kujiandaa na hiyo mikakati ya miaka mitano mnayoipanga kama Wizara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro, kwani tangu ameapishwa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana changamoto mbalimbali zinazowakumba wafugaji wake.

Mheshimiwa Spika, nikijielekeza katika kujibu maswali yake mawili ya nyongeza; moja linalohusika na hatua za dharura ambazo tunazichukua kuwaandaa wafugaji wetu. Kwanza kabisa ni kuendelea kutoa taarifa kupitia vyombo vyetu habari ambavyo vimekuwa vikitoa taarifa kila siku juu ya mabadiliko ya tabianchi na mipango ya hali ya hewa inavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili, kulingana na mipango ambayo tunayo kwa wafugaji wetu kwa kipindi hiki cha miaka mitano, ni kweli, Serikali inatambua kwamba nchi yetu ya Tanzania kama zilivyo nchi nyingine, zimekuwa zikikumbwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameleta ukame ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri wafugaji wetu. Kwa kulitambua hilo, sisi kama Serikali, tumechukua hatua zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja, ni pamoja na miradi mikubwa ya ujenzi wa mabwawa tunayoendelea nayo katika sehemu mbalimbali nchi nzima. Pia tunatambua kwamba miradi hii inachukua muda na fedha nyingi, hivyo tumekuja na mipango ya dharura. Kwanza, kuanza kufanya tathmini kwa ajili ya kuanza kujenga visima virefu katika maeneo mbalimbali ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeendelea kufanya mazungumzo na Wizara ya Kilimo ambayo kwa kiasi kikubwa inayo bajeti kubwa kupitia Tume yake ya Umwagiliaji ambayo inajenga mabwawa ya kumwagilia kwenye sekta ya kilimo sehemu mbalimbali nchi nzima ili kupitia mabwawa hayo, basi na wafugaji wetu waweze kutengenezewa majosho kwa ajili ya kunywesha mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara yetu kwa kutambua changamoto ya malisho tuliyonayo, tumeendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kupata majani ya malisho ya wanyama wetu. Majani haya tumeyafanyia tafiti, ni majani ambayo yanalimwa kwa kiasi kidogo na kupata mavuno mengi ambayo yanaweza kulisha wanyama wetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, pamoja na kuendeleza mashamba yetu yaliyo katika sehemu mbalimbali nchi nzima ikiwepo Shamba letu la Vikuge lililopo Pwani, lakini Shamba letu la Lagwira lililopo Mbeya na taasisi zetu mbalimbali kama *TARI* na *LITA* zinazozalisha malisho.

Mheshimiwa Spika, pia, tumeendelea kuhamasisha sekta binafsi na wafugaji wetu kuendelea kulima malisho mbalimbali. Kupitia hili, Serikali yetu kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeshatenga fedha, shilingi milioni 223 ambazo tutakwenda kuanzisha mashamba darasa ya malisho ya mifugo 300 nchi nzima katika halmashauri zote ili wafugaji wetu pale wanapohitaji mbegu, basi ziwafikie kwa ukaribu na kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kwa maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha wafugaji

wetu wanapata malisho haya kwa wepesi alituelekeza sisi tupunguze bei ya malisho haya ambayo tulikuwa tunauza hapo awali kwa shilingi 4,000 kwa kilo na kwa sasa kwa maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Rais, wafugaji wetu watapata malisho haya (mbegu hizi za malisho) kwa shilingi 1,000 tu kwa kilo ili waweze kuyapata kwa wepesi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa tunaendelea kuwahamasisha wafugaji wetu…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ameshakuelewa ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Upatikanaji wa Pembejeo Msimu wa Kilimo**

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbolea inapatikana kwa haraka wakati wa msimu wa kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati kwa wakulima. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa mahitaji kwa wakati, kuhusisha vyama vya ushirika kusambaza mbolea na kuhamasisha kampuni za mbolea na mawakala binafsi kufungua vituo vya mauzo ya mbolea kwenye maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizo, Kampuni za mbolea za *OCP, METL, ETG Inputs Limited, ITRACOM, MINJINGU, One Acre Fund, Premium Limited,* na *AFRISIAN* zimefungua ghala nane za mbolea katika Wilaya ya Mbozi na kusajili mawakala 174 ili kusambaza mbolea kwenye jumla ya vituo vya mauzo 85 katika wilaya hiyo. Lengo ni kuhakikisha mbolea zinapatikana kwa wakati ili wakulima waweze kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Onesmo.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza. Pamoja na kufunguliwa kwa maghala nane na kampuni nane, lakini pia kuwepo kwa vituo 85 na mawakala 174 Wilayani Mbozi, kwa nini msimu huu mbolea aina ya *DAP* imechelewa kufika kwenye jimbo langu na imefika wakati wa msimu wa kilimo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Jimboni kwangu mpaka hivi ninavyozungumza, wananchi wanalia sana, wanalalamika sana, *video* zao ninazo na nimewatumia Mawaziri. Wanalalamika aina ya mbolea ambayo wametumia mwaka huu, pengine kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kukosa uaminifu ama kutokana na kuchelewa kwa mbolea aina ya *DAP* ambayo wameizoea, wametumia mbolea mbadala na badala yake haijakidhi vigezo tulivyovizoea. Imepelekea mazao kudumaa, wananchi wameingia hasara, wananchi wanalia.

Mheshimiwa Spika, ipi kauli ya Serikali kwa wananchi hawa; na Serikali itafanya nini kuhakikisha msimu ujao wananchi hawa hawapati hasara ya aina hii na mnadhibitije hali hii isitokee kwa wakulima wangu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mnkondya kwa maswali madogo mawili mazuri na yenye kufuatilia maslahi ya wananchi wa Jimbo lake la Mbozi na Mkoa mzima wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza amezungumzia kwa nini mbolea ya *DAP* imechelewa mwaka huu. Niseme tu kwamba mbolea ya *DAP* sisi kama nchi tunaagiza kutoka nje ya nchi, na mahitaji ya *DAP* duniani sasa hivi yameongezeka hususan Brazil na nchi ya India.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji makubwa, maana yake sasa kumekuwa kama tunanyang'anyana katika ununuzi wa zile mbolea. Kwa hiyo, wale waagizaji wote waliopewa leseni za uagizaji waliweka *order,* na zilichelewa kutokana na mahitaji makubwa ambapo *order* zilikuwa zimefanyika kule nje ya nchi kwa maana ya India pamoja na Brazil

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na mahitaji yao kuwa makubwa, sisi tumeendelea kuzileta hizo mbolea hapa nchini na tumeendelea kuzisambaza japo zilichelewa kufika kwa wakati. Kwa hiyo, nikiri kwamba sisi kama Serikali tumeahidi katika msimu wa kilimo unaofuatia tutahakikisha waagizaji wa mbolea wanafanya hivyo kabla ya ule muda ambao msimu unakuwa umetarajia kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu kauli ya Serikali, sisi tunachokisema ni kwamba, moja, wananchi ama wakulima wote nchini wawe wananunua mbolea kupitia kwenye mfumo rasmi ambayo tumeuainisha, na tumetoa hiyo elimu kwa wananchi ili

inapotokea mwananchi amenunua mbolea haijaleta matokeo, sisi kama Wizara tumkamate yule msambazaji wa mbolea ama wakala.

Mheshimiwa Spika, tutamkamata, tutamfungia leseni yake na vilevile tutakuwa na nafasi sasa ya kumshurutisha ikiwemo kulipa fidia kwa wananchi ambao wameathirika. Sasa, hiyo ndiyo kauli ya Serikali na ninataka wananchi wasimamie hivyo kwa kununua mbolea katika mifumo rasmi ambayo tumeiainisha kote.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, yupo Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, Mbunge; na Ndugu Madaraka Nyerere kutoka Butiama Mkoani Mara, karibu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maelekezo ya Spika kuhusu uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge tarehe 28 Januari, 2026 Bungeni, Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyoonekana kwenye orodha ya shughuli za leo, kuna shughuli ya uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge Kanuni ya Saba ya Kanuni za Bunge ya mwaka 2025 imeeleza uwepo wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao huongoza vikao kwa utaratibu wa maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kuwapata wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge umewekwa katika Kanuni ya 13. Mchakato husika unaanza kwa Kamati ya Uongozi kupendekeza majina ya Wabunge wasiozidi sita kutoka miongoni mwa Wenyeviti

na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia jinsia, na pande za Muungano.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, majina hayo hupelekwa Bungeni ili Bunge lipigie kura majina hayo matatu. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 13 ya taratibu zetu, Jumanne tarehe 27 Januari, 2026 Kamati ya Uongozi ilikutana na kwa kauli moja ilipendekeza majina matatu ili yaweze kuwasilishwa Bungeni na Bunge liombwe kuyapitisha.

Waheshimiwa Wabunge, majina ya Wabunge waliopendekezwa na Kamati ya Uongozi ni kama ifuatavyo: -

(i) Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, (Mbunge wa Viti Maalum), ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;

(ii) Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini) ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo; na

(iii) Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mbunge wa Viti Maalum) ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 13(4) imetoa mwongozo wa endapo Kamati ya Uongozi itapendekeza majina sawa na nafasi zilizopo Bunge halitapiga kura, bali litathibitisha majina hayo kwa kura ya sauti chini ya Kanuni ya 95. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo basi, kwa kuwa, nafasi zilizopo za Wenyeviti wa Bunge ni tatu; na kwa kuwa, Kamati ya Uongozi imependekeza majina matatu; Bunge hili katika kikao chetu cha leo tarehe 28 Januari, 2026 linaomba kuwathibitisha Wabunge hao, kuwa Wenyeviti wa Bunge ili kupata uamuzi wa Bunge. *(Makofi)*

Sasa ninaomba wale Wenyeviti watatu waje mbele.

Msisimame kama mnaenda mpirani, watazameni Wabunge. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Wagombea wetu watatu ni hawa wawili walikuwepo tokea zamani, na mwingine ameingia, Mheshimiwa Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, wanaoafiki kwamba Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge, waseme ndiyo; na wasioafiki kwamba, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wasithibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge waseme siyo. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kumpitisha Mhe. Najma Murtaza Giga, Mhe. Deodatus Philip Mwanyika na Mhe. Cecilia Daniel Paresso kuwa Wenyeviti wa Bunge iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda.

Hongereni sana Wenyeviti wa Bunge, sasa ninakuomba Mheshimiwa Paresso uje utoe salamu za shukrani na useme mawili matatu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, nichukue fursa hii pia kutoa shukrani za dhati kwa Chama changu, Chama Cha Mapinduzi, kwa Kamati Kuu ya Chama ya Halmashauri Kuu chini ya Mwenyekiti wetu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa miongoni mwa wagombea wa nafasi hii ya Uenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwako pamoja na Kamati ya Uongozi, ninawashukuru sana kwa kunipendekeza na hatimaye kuleta jina langu mbele ya Bunge hili Tukufu kwa ajili ya kuthibitishwa. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa uthibitisho wao na kwa imani yao juu yangu.

Mheshimiwa Spika, ninaahidi ushirikiano kwako na kwa Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ninawashukuru. Ninawaahidi kutekeleza majukumu haya kwa uadilifu na uaminifu mkubwa ili kazi zetu za utekelezaji wa majukumu ya Kibunge yaweze kufanikiwa, ahsanteni sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paresso kajiandae kuvaa joho nitakupisha muda mfupi uje kukaa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali kuwa hapa na kwa kunikirimu zawadi ya uhai. Pili, ninakishukuru sana chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya jina langu kuletwa tena ili kuweza kuendelea na kazi hii ambayo niliifanya katika Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaishukuru sana Kamati ya Uongozi, lakini ninaishukuru sana Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Kilimo, Viwanda, Kilimo na Mifugo kwa kunichagua na mimi kuweza kuonekana tena niweze kuhudumu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana wewe kwa miongozo yako na malezi yako katika kipindi cha Bunge la Kumi na Tatu, lakini ninatoa ahadi kwa Wabunge wote ya kuendelea kushirikiana nao

kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge za 2025 Kanuni ya Nane ambayo zinatutaka tufanye kazi kwa weledi, kwa uadilifu na kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii fupi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Najma.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndio muweza wa kila jambo katika ulimwengu wetu. Pia nitumie fursa hii adhimu kuushukuru uongozi wa Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, pia, niushukuru uongozi wa Bunge kupitia wewe kwa kuridhia jina langu liwe miongoni mwa Wenyeviti wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni faraja kwangu kuhudumia tena katika Bunge hili kama Mwenyekiti kwa kushirikiana na wenzangu kwa kipindi hiki cha tatu, lakini pia, kwa mara hii ninaishukuru sana Kamati yangu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuridhia mimi niwe Mwenyekiti na hatimaye kuweza kupata fursa hii ya kuwa tena Mwenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu niseme tu, ninaamini kabisa Mwenyezi Mungu ataendelea kunisaidia ili tuweze kushirikiana vizuri.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025

*(Majadiiano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tujiandae. Kwanza, tutaanza na Mheshimiwa Margaret Simwanza, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Douglas Didas Massaburi.

Mheshimiwa Simwanza Margaret.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani, ambayo ni Hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Taifa letu. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, na wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru sana wananchi wa Urambo na familia kwa jinsi ambavyo wananipa ushirikiano mpaka napata nafasi ya kuendelea kuwa Mbunge katika jimbo hilo. Nawashukuru sana. Halikadhalika nimepata ushirikiano mkubwa wa Serikali ngazi zote za mkoa, wilaya na Chama chetu cha Mapinduzi katika kuhitimisha Ubunge wangu uliopita, lakini pia, katika kuanza awamu hii nyingine ambayo wamenipa heshima ya kuendelea kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Urambo tuna haki na wajibu wa kumshukuru Dkt. Samia kwa kazi kubwa ambayo ametufanyia kwa kupitia Serikali yake. Siyo rahisi kuyasema yote ambayo ametufanyia, lakini nitachukua machache ambayo kwa

kweli, ni ushahidi wa jinsi ambavyo wananchi wa Urambo tumenufaika na huduma kubwa tuliyopewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, shida yetu kubwa Urambo ni maji. Naishukuru sana Serikali, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia, imetupitishia mradi wa maji kutoka *Lake Victoria*. Tayari mabomba yameshafika, tenki kubwa limeshajengwa, tunachosubiri sasa hivi ni maji tu kuingia, halafu usambazaji uendelee. Tunaishukuru sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya pili tuliyokuwanayo, ilikuwa ni suala la umeme. Tulikuwa tunapata matatizo makubwa sana kupata umeme, ili tuweze kusaga mahindi, kukoboa mpunga na kadhalika, lakini Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia ilitupa shilingi bilioni 44, kituo cha kupoozea umeme tayari kinafanya kazi. Tunaiomba Serikali yetu, na hasa yeye mwenyewe, akipata nafasi, aje akizindue rasmi, lakini sasahivi umeme Urambo ni furaha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ametusaidia Mheshimiwa Dkt. Samia, ametupa shilingi bilioni 13 kwa suala la afya. Kwa hiyo, tumejenga vituo vya afya na zahanati, tunashukuru sana. Pia, kwa upande wa elimu, wote ninyi ni mashahidi pamoja na Urambo kwamba tumepata madarasa mapya na walimu wameajiriwa. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, elimu pia, imepewa kipaumbele sana kwetu. Halikadhalika barabara, ninyi mnafahamu, sisi Urambo ni wa vijijini, lakini tulipewa shilingi bilioni 12 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliomba pia, tuongezewe barabara nyingine, hasa kwa kupitia *TANROADS*. Nashukuru sana, majibu yameshatolewa humu Bungeni kila mara nilipokuwa ninauliza. Tumepata barabara ya kutuunganisha sisi Watu wa Urambo na Sikonge. Tumepata barabara inayotoka Usoke inakwenda Tutuo Sikonge, itakuwa ni ya lami. Kila wakati ninapouliza, Naibu Waziri,

Mheshimiwa Kasekenya, huwa anajibu kwamba tayari usanifu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunategemea wakati wowote wilaya zinazotuzunguka pia zitakuwa na lami kwa sababu, tumeshapeleka maombi mengine ili tuendelee kupata huduma za barabara nzuri. Kwa kweli, tuna haki ya kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa mambo mengi ambayo siyo rahisi kuyataja yote kama nilivyosema, lakini tunamshukuru sana na tunamwombea aendelee ili aweze kutuletea maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukichukua suala la maji, nimelizungumza hapa. Namshukuru sana Mheshimiwa Aweso, kila anaposimama huwa anataja kwamba, tutapata maji kutoka *Lake Victoria*. Kila ninapomwona yeye ananikumbusha na mimi ninamkumbusha kwamba, Mama Sitta maji ni lazima upate, utachekelea. Kwa kweli, nachukua nafasi hii kuiomba Serikali itusaidie maji yasambazwe. Yatatoka *Lake Viktoria* sawa, yatafika Urambo, yataingia kwenye tenki, lakini je, yanawafikiaje wananchi kule waliko?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachoiomba Serikali, tunajua itakuwa ni gharama kubwa, lakini itakuwaje faida sasa kama maji yatafika Urambo, yaingie kwenye tenki, halafu yasisambazwe?

Mheshimiwa Spika, sisi tunajua kwamba, miundombinu ya maji ni ya siku nyingi na tunaamini kabisa haya yatakuja kwa nguvu, kwa hiyo, kupita kwenye mabomba ya zamani itakuwa siyo rahisi. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima naiomba Serikali ituletee mpango mkubwa wa kusambaza maji yafike kwa wananchi, ndiyo ombi langu kubwa ambalo nalileta leo. Pamoja na shukrani, lakini tunaomba maji yasambazwe yawafikie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ukirudi kwenye maji hayo, Serikali hii imeona kwamba, kutegemea tu maji ya kutoka *Lake Viktoria,* hapana, tuongezee mabwawa. Wakatupatia shilingi bilioni sita, bwawa linajengwa eneo linaitwa Kalemela, halijakamilika. Nia ya Serikali ni nzuri, lakini tunachoomba sasa ni kwamba, lile bwawa

la shilingi bilioni sita likamilike ili lichangie watu wapate maji zaidi kwa ajili ya kilimo, mifugo na matumizi ya nyumbani, lakini pia na ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tunaendelea kuishukuru Serikali na kuomba ile mitambo iliyoletwa, yale malori makubwa yenye mitambo ya kuchimbia maji, yaani visima, yaendelee kukaa kwenye maeneo yetu ili tupate visima vingi zaidi visaidiane na bwawa na maji ya kutoka *Lake Victoria* kwa sababu, kilio chetu kwa muda mrefu kimekuwa ni maji, na kwa kuwa sasa Serikali tayari imeshaanza kutusaidia, basi ikamilishe.

Mheshimiwa Spika, humu Bungeni nimeongea sana mpaka nafikiria kuongea tena wakati wa bajeti sijui, Waziri atanistahimili kwa sababu, Mawaziri wengi wamepita katika Wizara ya Maliasili na Utalii na nimekuwa nikiwaambia hapa kwamba, wananchi wanapenda sana maendeleo yanapoletwa kwao, lakini kitu kikubwa ni ushirikishwaji na elimu. Sisi kwetu kuna kata tatu: Nsenda, Ukondamoyo na Ugala ambao eneo lao limechukuliwa, limekuwa Hifadhi ya Msitu wa Mto Ugala.

Mheshimiwa Spika, nimeongelea sana, Mawaziri wote wanajua na wao wanaahidi kwamba litafanyiwa kazi. Tunaomba sasa lifanyiwe kazi. Wananchi wanashukuru kwa hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali katika kuhifadhi misitu na kadhalika, lakini wanaomba maeneo.

Mheshimiwa Spika, tuliomba kilometa tano wapewe kwa ajili ya kuweka mizinga yao nimeenda mpaka kwenye kamati, wanajua, kamati ambayo nashukuru Mheshimiwa hapa amerudishwa kule. Nimekwenda kuwaona kwamba, wananchi hawakatai eneo lao kuwa hifadhi, lakini wanataka wapewe kilometa tano kwa ajili ya kufuga na kuweka mizinga ya nyuki. Wamezoea kupata asali na asali ni zao mojawapo ambalo tunalitegemea sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili suala Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii achukue hatua ambayo itaonesha kweli,

wamesikia kilio cha wananchi kwa sababu, kama nilivyosema, wanahitaji kuelimishwa, lakini pia, na wenyewe wanaomba waongezewe. Kwa hiyo, nitashukuru sana, kama suala hili litachukuliwa na kupewa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika jambo lingine ambalo nimeliomba na bado narudia kuliomba ni kwamba, sisi ni majirani wa Ulyankulu, Shinyanga. Hawa ni majirani zetu kwa sababu, ukifika Ulyankulu, mbele tu kidogo pale Kashishi, unakutana na Kahama.

Mheshimiwa Spika, tumeomba tuunganishwe na barabara ya lami ili watu wa Shinyanga wanapotaka kwenda Mbeya wasiwe na haja ya kwenda Tabora. Wanakwenda Tabora kufanya nini? Wakatishe tu pale Kahama, wanakwenda Ulyankulu, wanatoka Ulyankulu wanakuja Urambo, wanakwenda Sikonge, wanaendelea kwenda Mbeya, Katavi na kadhalika. Kwanini wazunguke tena waende kwingine?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi letu sisi majirani ni tuunganishwe na barabara ya lami, tutafurahi sana kwa sababu, barabara inafufua maeneo. Kama mnavyoona barabara hii ya zamani iliyokuwa ya Manyoni, miji imechipuka kutokana na barabara ya lami ilivyokuja. Sasa hivi ukipita tu unaona mji kabisa umechipuka na sisi tunataka miji ichipuke kutokea huku Kahama inapita Ulyankulu kwa lami inakuja mpaka huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kuiongoza Serikali yake na kujali mahitaji yetu. Kwa hiyo, tunaomba sana, kama nilivyosema hayo yaliyotangulia ya maji, Mwenyezi Mungu ambariki aendelee kutuhudumia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mary Chatanda, jiandae Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Jackson Kiswaga, na Mheshimiwa Massaburi.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge, tarehe 14 Novemba, 2025. Naanza kwa kusema kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana karama ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua kwamba, ana karama ya uongozi ni pale alipochukua nafasi ya Urais, katika kipindi cha miaka minne amehakikisha kwamba anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2025 kwa kiwango cha hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tumeshuhudia mambo ambayo yamefanyika ndani ya kipindi cha miaka minne. Tumeshuhudia ujenzi na ukamilishaji wa *SGR*. *SGR* hii siyo suala la usafiri tu, ni pamoja na usafirishaji. Tumeona faida kubwa ya *SGR,* hasa kwa wenzetu wa Mkoa wa Dodoma, wanawake wamepata faida kubwa ya kusafiri kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kufungasha biashara zao na hatimaye wanarudi kuja kufanya biashara Dodoma. Hiyo ni fursa kubwa ambayo wanawake wameipata na kuitumia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita Mheshimiwa Paresso aje kukalia Kiti.

Mheshimiwa Chatanda endelea tu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kukamilisha ujenzi wa *SGR*. Tunamwomba aendelee kukamilisha maeneo yaliyobakia ya kutoka hapa Dodoma kuelekea Mwanza ili

watani wangu wa Mwanza na wenyewe waweze kufaidi matunda ya *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza kwa kupata nafasi ya Uenyekiti. Hongera sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kushuhudia suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili la Mwalimu Nyerere limewezesha kuongeza umeme katika nchi yetu. Hapo mwanzoni umeme ulikuwa unakatikakatika, sasa hivi umeme unapatikana kwa muda wote. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kulisimamia kuhakikisha kwamba, Bwawa la Mwalimu Nyerere linakamilika na ndoto zile za Hayati Baba wa Taifa zinakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Rais wetu, na tunajua kabisa kwamba, suala la upatikanaji wa umeme linawasaidia sana wanawake wajasiriamali. Wanawake wale ambao wameanzisha saluni zao, na shughuli zao zinazohusiana na umeme, wananufaika kupitia mradi huu wa Bwawa hili la Mwalimu Nyerere ambapo umeme sasa unakuja bila kukatikakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia uzinduzi wa meli *ya MV. Mwanza,* Wananchi wa Mwanza, Kigoma na Kagera wamepata bahati ya uzinduzi wa meli hii ambayo itawanufaisha kiuchumi hasa ikizingatiwa kwamba, inakwenda hadi katika nchi za jirani. Kwa hiyo, wanawake watanufaika sana kupitia meli hii kwa ajili ya kwenda kutafuta na kufungasha mali kupitia kwenye nchi za jirani, hususan kule Uganda; watafungasha mali zao, watarudi kuja kuuza. Kwa hiyo, watajiinua kiuchumi kupitia hii Meli ya *MV. Mwanza. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka minne, ameweza kujenga shule za msingi kuanzia awali hadi sekondari, lakini kubwa zaidi alilolifanya ni kuhakikisha anajenga shule za sekondari za wasichana za mchepuo wa sayansi kwa kila mkoa, tunamshukuru sana. Tunajua lengo lake

anataka mabinti waweze kupata elimu ili kuendana na elimu kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru tena Mheshimiwa Rais, katika mpango wake amesema kwamba, atajenga shule kila Mkoa, za wavulana za vipaji. Kwa hiyo, nalo hilo tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais katika mipango yake hiyo na tunaomba basi kila mkoa uandae maeneo kwa sababu, Rais ameshasema kwa vyovyote vile atatoa fedha ili kusudi shule hizo ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, katika kipindi chake cha miaka minne ameweza kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya, za Mikoa, hadi za kanda. Hospitali hizi zimeweza kuwekewa mpaka na vifaatiba. Tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwarahisishia akinamama wa vijijini kwa kujenga hizi zahanati; walikuwa wanapata tabu kwenda mwendo mrefu kufuata huduma za zahanati kwa ajili ya kwenda kujifungua, lakini sasa wamekuwa na zahanati kwenye maeneo yao na vituo vya afya maeneo ya karibu na kuweza kujifungua karibu. Kwa hiyo, afya za akinamama na watoto zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kushukuru suala zima la maji, Mheshimiwa Rais alipokuwa Makamu wa Rais alisema kwamba, atahakikisha anamtua mwanamke ndoo kichwani. Jambo hilo hata alipoingia kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi chake cha miaka minne, ameliendeleza kwa kununua mitambo ya kuchimbia visima vya maji kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kwamba, changamoto hii bado ipo, lakini haina ukubwa kwa kiasi hicho. Tunatambua kwamba, Mheshimiwa Rais, kupitia Wizara ya Maji, hususan kwa kijana wangu Mheshimiwa Aweso, watalisimamia hili, ili ziweze kutimia ndoto za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kumtua mwanamke ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalau kwa wale ambao tayari wameshafanikiwa kupata maji, imesaidia sana kurekebisha ndoa za wanawake na waume zao huko vijijini. Nilipokuwa nafanya ziara, nimekwenda kuzindua mradi mmoja wa maji, wanawake wale wamemshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwapelekea ule mradi wa maji kwa sababu, walikuwa wanapata shida ya kuondoka nyumbani saa kumi usiku, akimuacha mmewe amelala kitandani anakwenda kwenye maji, akirudi bado anapata mkong'oto kwamba, kwanini amechelewa kurudi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amewasaidia kuimarisha ndoa zao kwa upatikanaji wa majisafi na salama huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wananchi wa Tanzania tuendelee kumwombea Rais wetu, tuendelee kumsaidia Rais wetu ili aweze kutekeleza mambo mengine mazuri ambayo amejiwekea katika Mpango wa Maendeleo ambao tumeupitisha kipindi kilichopita cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi ya kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mary Pius Chatanda. Sasa atafuata Mheshimiwa Japhet Hasunga, akifuatiwa na Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kipekee kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa kuniamini na kunichagua kuendelea kuwawakilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa na kwa heshima kubwa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Spika wa Bunge letu, Naibu Spika, na ninyi Wenyeviti ambao tumewachagua leo ambao ndio mtakuwa viongozi wetu wa kuliongoza Bunge hili na kutuongoza sisi. Ninawapa hongera sana, sana, sana ili muweze kutekeleza majukumu ya Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025. Hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni hotuba nzuri, hotuba yenye maono, hotuba yenye mtazamo mpana, hotuba yenye nia ya kuleta maisha mazuri kwa wananchi wa Tanzania. Hotuba ile ili-*cover* maeneo yote ya msingi ambayo kama tukiyawekea mikakati nchi yetu itapiga hatua kubwa katika kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kutumia *slogan* yake ya Kazi na Utu inaonyesha kwamba, anasema kwamba bila kufanya kazi, Taifa haliwezi kuendelea. Kwa hiyo, lazima Watanzania wote, tufanye kazi. Pia anasema, tunapofanya kazi tuheshimu na utu wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mungu alimuumba binadamu, akampa macho, lakini yale macho hakumpa, ajiangalie yeye, alimpa macho ili aangalie watu wengine, aangalie mambo mengine ndiyo ayaone. Sasa maana yake kiongozi yeyote unapopewa Madaraka, kazi yako ni kuangalia watu wengine wanahitaji nini uweze kuwasaidia, na haya yameonekana katika maono ya Mheshimiwa Rais. Ninampongeza sana kwa namna anavyoiona na kuitazama nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwangalia Mheshimiwa Rais anatamani Watanzania wawe na maisha mazuri, anatamani nchi yetu ipige hatua kubwa kiuchumi, kijamiii na kisiasa. Hayo yanajidhihirisha, kwenye hotuba yake, anasema: "Uchumi wa Tanzania ulikua kwa 5.6%," lakini matamanio yake ni kutaka kuona uchumi unafika zaidi ya asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi kama Wabunge kwa kushirikiana na Serikali yetu tunatakiwa tuweke mikakati ya kuhakikisha uchumi huu unakua zaidi ya asilimia saba ili kusudi maisha ya Watanzania yaweze kuwa mazuri, kwa sababu ukikua chini ya asilimia saba, wakati kuna mfumuko wa bei, wakati idadi ya watu inaongezeka

kwa 3.2% na mfumuko wa bei uko kwenye asilimia mbili, maana yake yale maisha mazuri tunaweza tusiyaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuyaone maisha mazuri, lazima uchumi huu tusaidiane, tufikirie kwa mapana, ukue kwa zaidi ya asilimia saba, ndipo maisha yetu yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, hilo kwa kweli ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anasema ili maisha yawe mazuri lazima tuangalie sekta za uzalishaji, sekta zile zinazohusu watu wengi. Sekta za uzalishaji anasema ni kilimo, na hii inaonekana hata katika kipindi kilichopita, tuliona bajeti ya kilimo imeongezeka mpaka kufika shilingi trilioni 1.2. Ni matumaini yangu huenda tena ikaongezeka mwaka huu. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wako kwenye kilimo. Kwa hiyo, ukiendeleza kilimo maana yake utakuwa umeyaboresha maisha yao. Ukiendeleza kilimo ajira zao zitakuwa ni nyingi, ukiendeleza kilimo Taifa litapata fedha za kigeni, na ukiendeleza kilimo, uchumi wa Taifa letu utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema ukichukua sekta ya uvuvi, sekta ya mifugo, hizi ni sekta ambazo zina watu wengi. Hizi ni sekta ambazo anasema ziongezewe bajeti na sisi kama Bunge lazima tuunge mkono kuongezea bajeti kwenye sekta hizi za uzalishaji. Pia anasema, sekta ya madini iendelee kutoa mchango mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi zilizobarikiwa kuwa na madini ya kila namna. Tuna madini mengi ambayo mpaka sasa hivi nina imani kama tumechimba hata 1/5 hatujafikia. Sasa ni lazima tuweke juhudi na maarifa kuhakikisha kwa kweli tunachimba haya madini, yanatunufaisha katika nchi yetu. Hiyo ni moja ya sekta muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nchi ya Tanzania imebarikiwa kuwa vivutio vingi vya utalii. Kwa hiyo, lazima tuweke mkazo kwenye

sekta ya utalii. Sekta ya Utalii ina uwezo wa kutuingizia fedha nyingi sana. Nchi za wenzetu tunaona, nchi nyingine watalii ni wengi sana. Sasa hivi sisi ndiyo tumefika watalii karibu milioni tatu na sisi angalau tunasema tumejitahidi, lakini kwa vivutio tulivyonavyo, kwa maliasili tulizonazo, bado tunahitaji kuwekeza zaidi katika kuboresha sekta ya utalii ili iweze kuwavutia watu wengi zaidi na tuweze kunufaika kupata mapato mengi yanayotokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zinapata watalii wanafika mpaka milioni 100 kwa mwaka. Nchi kama Ufaransa, Hispania na nchi nyingine zinapata watalii wengi sana. Katika Afrika nchi kama Morocco inapata zaidi ya watalii milioni 16. Nchi kama *Egypt* inapata watalii wengi. Tanzania ambayo ina vivutio, ni nchi ya pili duniani kwa vivutio, kwa hiyo, tunahitaji kuongeza mikakati ili kuvutia watalii zaidi, kujenga hoteli, kujenga vivutio mbalimbali ili tuweze kupanua wigo wa utalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweka mkazo, pia ametufundisha, anatuambia michezo siyo burudani tu, michezo pia ni Uchumi. Amewekeza nguvu kwenye michezo. Tumeona jinsi ambavyo amejitahidi sana ku-*sponsor* michezo yetu, ndiyo maana hata sasa hivi Tanzania kimichezo tumepanda. Tumeona hata timu zetu zimepanda. Anatuambia, michezo ni biashara kama biashara nyingine. Kwa hiyo, tunahitaji kuwekeza zaidi kwenye michezo, pia tutaimarisha afya zetu, na vile vile tutapata fedha nyingi zinazotokana na michezo. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sasa tunakuwa ndiyo *host* wa mashindano ya *AFCON* yanayofuata. Tanzania tunawekeza kwenye viwanja, kwa hiyo, ni lazima iende sanjari na kuwekeza kwenye vipaji vya vijana watakaoshiriki katika michezo hiyo waweze kutuletea faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo Mheshimiwa Rais ameleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu. Anasema lazima tuwe na *human development plan*. *Human development*

*plan* tunaiona ambavyo tumebadilisha kwenye elimu, tumeanza kwenye shule za msingi, shule za sekondari, tumekuja na mitaala mipya, na hii imekuwa *adopted* na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais anasema lazima twende zaidi ya hapo; vyuo vyetu vya kati, vyuo vikuu mitaala yao lazima ibadilishwe iendane na mahitaji ya leo ya kisasa ili tujue viwanda vyetu vinahitaji wataalam wa namna gani? Tunahitaji ujuzi wa namna gani ili hii nchi iwe na wataalam wa kujitosheleza na tuweze kupiga hatua kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, lazima tujenge miundombinu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kule Vwawa alitupatia fedha tukajenga kilometa kadhaa za lami, na sasa inajengwa kilometa 21 kutoka Njiapanda ya Iyula kwenda mpaka Idiwili. Tunamwomba azidi kutupatia fedha zaidi tujenge barabara ya lami kutoka Vwawa kwenda Isalalo kutoka maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani tukifanya haya, tutawafanya wananchi wa Tanzania waishi maisha mazuri na tuweze kufikia malengo tuwe na furaha na tuweze kuifurahia nchi yetu na utamaduni wetu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae na Mheshimiwa Dougras Massaburi pia ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia leo kwa mara ya kwanza. Kwa kuwa ndiyo tumeanza Bunge hili na mimi ni mchungaji wa timu ya mpira wa miguu ya Bunge na mshauri wa kiroho kwa baadhi ya Wabunge wenye ugonjwa wa kiroho, baadhi

siyo wote ambao wanapenda ushauri, nianze kwa kutamka maneno ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha 1Timotheo 2:1-2 inasema: "Basi kabla ya mambo yote nataka dua na sala na maombi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote. Tunaanza kwanza kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka tuishi kwa utulivu na amani katika utauwa wote na ustahivu." Neno lingine katika Warumi 13:1 linasema: "Na kila mtu na atii mamlaka iliyo kuu, maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu na ile iliyopo imewekwa na Mungu." Nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, tunamwombea Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo ya maandiko haya matakatifu, Mungu akampe hekima, maarifa, ulinzi na afya ili tuweze kuishi kwa amani, utulivu kama maandiko matakatifu yanavyosema. Andiko lingine Jeremiah 29:7 Inasema, "Kautakieni amani mji ule ambao nimeufanya mkachukuliwa mateka, mkauombee kwa Bwana kwa maana katika amani yake mji ule na ninyi mtapata amani."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie ndugu zangu, tunao wajibu wa kuliombea Taifa letu la Tanzania, kwa maana anasema katika amani yake katika Taifa la Tanzania, katika mafanikio yake, ndivyo na sisi tutakavyofanikiwa. Ndugu zangu haya ni maelekezo ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kutuongoza. Sisi watu wa Kalenga tulimpa kura za kutosha yeye mwenyewe alivyokuja kule aliona bashasha, na tulifanya hivyo tulikuwa na sababu. Jimbo la Kalenga limekuwa na maendeleo makubwa, lakini hapa tunajadili bajeti ya Kitaifa, lakini ni mfano, ndiyo maana alivyokuja tulimpokea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye hiki kitabu kuna mambo mengi mazuri, yaani muda hauwezi kutosha kueleza, lakini

nikianza na kwenye maji ambako mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bunge lililopita, nimeiona nia iliyowazi sana ya Mheshimiwa Rais ya kufanya mapinduzi kwenye sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaingia tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 640. Mpaka sasa tayari tumeshaweka kiasi cha shilingi trilioni moja kwenye sekta ya maji. Hiyo inaonyesha nia iliyonyooka, nia ya wazi ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba huduma hii ya maji inapatikana katika Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi karibu 1,000 ambayo inatekelezeka katika maeneo mbalimbali, miradi karibu 878 vijijini, miradi 217 ikitekelezeka mijini yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.3. Je, tumemaliza changamoto ya maji? Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotufurahisha ni kuona nia ya Mheshimiwa Rais hata kwenye hii hotuba yake katika ule ukurasa wa 17 ameonyesha kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameathiri upatikanaji wa maji katika maeneo mengi hata ya Dar es Salaam hapa mmekuwa mkizungumza, lakini tunafurahi tunavyoona Rais ameanza kutekeleza mipango mikubwa ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, bwawa lile la Kidunda ambalo lilikuwa ni mipango ya Mwalimu Nyerere, Mama ameanza kulijenga. Kwa hiyo, niwaambia ndugu zangu wa Dar es Salaam, ndugu zangu wa Pwani na ndugu zangu wa Morogoro kwamba, baada ya kukamilisha bwawa hili ukanda huo tutakuwa tumemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mipango ya kutumia maji kutoka katika Ziwa Nyasa, maana yake Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria katika mpango wake Rais wa kutengeneza ile gridi ya Taifa, maana yake hata ndugu zangu kule Kalenga, ndugu zangu kule Iringa tutawapelekea maji kwa mfumo wa gridi kama mnavyoona umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Watanzania wawe na matumaini makubwa na Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mipango yote imeonyesha kwenye hotuba yake na sisi tuko hapa kusimamia kuhakikisha kwamba inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwa sababu katika ahadi yake ya zile siku 100 alieleza kwamba ataajiri watumishi 12,000. Mimi nimpongeze na nimshukuru kwa sababu Jimbo langu la Kalenga katika Halmashauri yetu ya Iringa Vijijini mimi na Kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi tumeshaletewa wafanyakazi 194 kuonesha kwamba alichokisema anamaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye bima ya afya, tayari tumeshapewa kitita cha 150,000 kwenye familia hizo. Ni hatua kubwa ambazo Mama ameanza kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta za uzalishaji, tukienda pale hasa nikizungumzia uvuvi na mifugo, tumeona mapinduzi makubwa kwenye kununua boti mbalimbali na uzalishaji wa vifaranga ambavyo vimekuwa vikitolewa kwa watu katika vizimba, Rais amekuwa akiweka ruzuku huko. Kazi kubwa zinafanyika na sasa anaeleza katika ukurasa wa 22 wa hotuba yake kwamba, tunakwenda kuongeza maeneo ya malisho kutoka heka 3,900,000 kwenda 6,000,000. Sasa hapa ni ushauri tu kidogo kwa wanaomsaidia Rais, malengo yake mazuri ameshaonesha hapa mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tunaipata kwenye hili eneo la ufugaji pamoja na kuwa kwamba haya maeneo tunayatenga, lakini wafugaji wetu hawa wakina Chacha, kutoka kanda hizi za wafugaji, changamoto za kuhamisha hamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, hiyo ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotakiwa kukifanya sisi kama Serikali ni lazima tu-*commercialize* masuala ya mifugo, tufanye kuwa ufugaji wa kibiashara. Kwa maana hii, Serikali iwekeze fedha katika

maeneo haya ambayo tunayatenga, tuhakikishe tumeweka majosho, tuhakikishe tumejenga mabwawa ili tukiwatengea haya maeneo, wawe na maji, wawe na majosho katika maeneo haya. Tukifanya hivyo, hawa watu wataacha kuhamahama, kwa sababu mara nyingi wanahama kutafuta majosho pamoja na kutafuta maji. Hii pia itatusaidia kujua idadi ya mifugo halisi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo mingi hapa Tanzania haijulikani, watu wengi wafanyabiashara inawezekana baadhi ya Wabunge na wafanyabiashara nyingine wananunua hawa ng'ombe wengi wanawatupa tu huko porini. Hii ni biashara kubwa ya wafanyabiashara wengi kwa sababu wanapata faida, kwani kule hakuna kodi. Sasa tukiweza kuiratibu hii mifugo kwa namna hii, kwanza Serikali itaweka mfumo mzuri wa kupata fedha kutoka katika mifugo na tutakuwa tumewafanya wasiendelee kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi, lakini mwisho nisisitize tu kwenye hili suala kwenye mambo ya habari na utamaduni pale. Nimeona mipango ya kujenga ukumbi wa maonyesho, lakini nilikuwa nashauri, hapa Dodoma tungejenga ukumbi mkubwa kwa ajili ya masuala haya ya makumbusho ili mambo yote ya kimila na tamaduni za mikoa yetu mbalimbali ziweze kupatikana katika eneo moja, watu waendelee kusoma na kuendelea kutambua historia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. ninaona kengele ya pili imeshagonga. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Anafuata Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi na Mheshimiwa Sara Msafiri wajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaanza kuongea kwamba, mimi huwa kwenye ukweli ninazungumza ukweli, kwenye kona huko huwa siendi. Nitasema yale ya ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais katika Jimbo langu la Gairo kwa vitu ambavyo ametufanyia wananchi wa Gairo. Kwa mfano, tumepata madaraja ambayo yalikuwa yanaua watu kila siku. Nilimwomba mwaka juzi 2024 alipopita pale, tunashukuru madaraja yamekwisha ya shilingi bilioni 16, la mita 120 na la shilingi bilioni 11 la mita 80. Madaraja ya Chakwale na Nguyami yamekwisha. Ninamshkuru kwa kuweka barabara hiyo katika *feasibility study* kutoka Gairo hadi Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kwa Gairo kutupa barabara ya lami ya kilometa 57 kutoka Gairo mpaka Nongwe. Tunamshukuru kwa mradi wa maji wa shilingi bilioni 21 na shilingi bilioni 9.9, takribani shilingi bilioni kumi. Kwa hiyo, lazima niseme ukweli, tangu mwaka 2005 maana mimi nimeingia tangu mwaka 2005, na bado nipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kustaafu kwa heshima, hiyo hakuna, kwa sababu mimi nilimtoa mtu, na mimi mpaka nipate kura mbili ndipo najua hapa sasa unastaafu kwa heshima. Kwa hiyo, kwa wale wanaoviziavizia bado nipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tangu niingie mwaka 2005, nimekaa na Mheshimiwa Kikwete na kabla ya hapo nimekaa na Mheshimiwa Mkapa, kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kupitia viti 20. Nimekaa na Mheshimiwa Magufuli pamoja na yeye, lakini lazima niseme ukweli. Katika kipindi cha Awamu ya Sita, Gairo na Tanzania imepata vitu vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wakati wa nyuma wananchi walikuwa wanajenga wenyewe shule za msingi; wakati wa nyuma zahanati zote walikuwa wanajenga wananchi; wakati wa nyuma tulikuwa hatuna hospitali za wilaya, wengi wamezungumza, tangu Uhuru, watu walikuwa hawana hospitali za

wilaya. Sasa, wakati wake tuna sekondari zinajengwa na Serikali, tuna zahanati zinajengwa na Serikali, tuna *ambulance,* kama Gairo ina *ambulance* takribani saba ziko pale. Kwa hiyo ni lazima tushukuru. Tuseme ukweli, kwenye mahali pa ukweli tuzungumze ukweli, kwamba kazi aliyoifanya huyu mama yetu ni kazi nzuri. Hata kama kuna mtu ana kinyongo, hicho ni kinyongo cha binafsi. Kwa hiyo, huwezi kumlazimisha mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukweli huo huo katika ukurasa wa 37 katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, amezungumzia uwajibikaji na utawala wa sheria; na amezungumzia kwa baadhi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika nchi yetu, hapa amezungumzia habari ya watu wabadhirifu wa fedha ambazo zilikuwa ziende kwa wananchi, zinyanyue maisha ya wananchi, kama yeye lengo lake linavyotaka. Amezungumza kwamba kuna baadhi ya watu ambao ni mafisadi. Ninasema katika nchi hii sasa hivi mafisadi hawa siyo kwamba wanapiga kidogo, wanapiga kiuhakika. Ni walaji na ni walafi, na wanafanya vitu kama vile wananchi wa sasa hivi hawana elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tufahamu sasa hivi ukienda sehemu yoyote, hata kama kwenye kijiwe cha bodaboda utamkuta mtu wa chuo kikuu, utamkuta wa *Form Six,* utamkuta wa *Form Four* utamkuta wa Darasa la Saba na utamkuta na asiyesoma. Wakikaa pamoja pale wakianza kuongea wote wana kuwa wako *University*. Kwa hiyo, hawa watu siyo kwamba hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta mtu yuko Serikalini ana *GPA* labda ya 2.5 halafu yule ambaye yupo bodaboda ana *four*. Halafu huyu jambazi anamtuma bodaboda, yule wa *GPA 4,* nenda kapeleke misumari pale, peleka hapa, halafu huyu naye mjanja anajua mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tujue. Hizi sheria za TAKUKURU kama ziko kidogo zimelegea, walete basi tubadilishe.

Watu kila sehemu wanajengajenga majumba, nini. Watu wanaona. Tusizungumze sisi hapa kama Wabunge wa CCM ambao tuna uchungu, tuzungumze ya leo, kwamba, je, tunayozungumza leo tunajifurahisha leo? Je, ya mwaka 2030 nayo tunayasahau. Tukizungumza ya leo tujue kuna mbele huko, kuna mwaka 2030. Je tunakwendaje kwenye chaguzi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tulikuwa tunamwomba Mheshimiwa, na sio Mheshimiwa Rais, kwa sababu Urais ni taasisi. Hata kama Mheshimiwa Rais anajitahidi vipi, lakini hawa watu wa chini yake wanamsaidiaje? Wanayaona haya mambo yanayofanyika, hao watu wa chini na wamekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi mfanyabiashara sipendi ufisadi wala sipendi wezi, kwa sababu mimi ninafanya biashara kwa miaka mingi, ninahangaika, nanunua hiki, nafanya hiki halafu kinakuja kijitu kinaiba kinaingia kwenye biashara yako. Unakingoja kifilisike, kwa sababu kitafilisika tu, lakini tayari kimeshakudhuru ndani ya miaka mitano miaka sita kwenye ile biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu nimemwona kabisa kwamba anahangaika sana, na ameanza vizuri sana kwenye masuala haya. Sasa tunamwomba, kama ameanza vizuri kwenye masuala ya kuangalia watu wezi wa nchi, maana yake tusikae hapa tu tuna kazi ya kusema aah sisi, sisi, sisi, kwenye watu, wezi wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanza vizuri, na tumeona ameita wale watu wa maadili na watu wa sehemu nyingine. Watu wa maadili siyo wanakuja kwa Wabunge, Mbunge mimi nakutana na fedha ya Serikali wapi? Sikutani nayo mahali popote, lakini Mawaziri na watu wa chini yao ndio wanaokutana na fedha ya Serikali. Kwa hiyo, kama ni vibaka, basi ni huko kwenda huko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanza vizuri, nami ninampongeza, na aendelee hivyo hivyo, na

amerudisha angalau imani kwa wananchi. Wamsaidie Mheshimiwa Rais. Rais hawezi akawa anaangalia mwizi yuko Gairo Halmashauri, akaangalie sijui yuko Bukombe, akaangalie sijui yuko Rorya, haiwezekani kitu kama hicho, na wawe wanafuata ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vinahusika kwenye masuala ya ushauri, wachukue ushauri, waangalie. Maana wananchi wa sasa hivi sio wajinga, wanajua kabisa hili jengo ni la fulani, hiki kitu cha fulani, huyu yupo Serikalini ni mwizi aliyekubuhu. Wengine tena wanakwenda hata hawana aibu, utakuta wanawanunulia watu mishkaki, wanawanunulia nini. Kama hawana, wengine waje, mimi nitawaandikia wezi wote, maana na mimi ni Usalama wa Taifa wa kujitegemea, nipo hapa, wasiwe na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaambia, katika kitu kinachozungumza, na ndiyo maana mama amekizungumza hapa anataka usaidizi kutoka kwa wasaidizi wake. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais alikizungumza kwa uchungu sana. Je, wasaidizi wake wanafanya hizo kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mawaziri wasikae tu hapa wanangoja nani atakuwa Rais baada ya mwaka 2030. Hata sisi huku nyuma, mimi nilikuwa ninaongea na Mheshimiwa Maganga. Mheshimiwa Maganga atakuwa hapa, maana hata mimi nina-*trot,* maana lazima tujue, wasikae huko tu, kila huyu anataka hiki. Hata sisi huku nyuma tulikuwa tuna-*trot*. Nilikuwa ninaongea na ndugu yangu Mheshimiwa Jafari hapa, yupo mwingine hapa anataka Uwaziri Mkuu mwaka 2030. Msiwe na wasiwasi tutakuwenda huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi nzuri. Ninaomba pale pale, na timu yake wote, na ninajua katika timu yake ya Mawaziri waliopo sasa hivi wengi ni wazuri, ila waangalie huku chini. Hata hapa Wabunge

hawa wengine, usione hawapigi kelele, inawaingia kichwani, wanajua ninachokiongea na wanakielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda sehemu fulani, utakuta jumba la fulani, jumba la fulani. Kuna mmoja hapa alijenga nyumba akaandika kabisa na jina lake *fulani tower*. Jamani, sasa huko tunafanyaje? Sisi wanatupa kazi ya ziada. Mtu anayekupenda atakwambia ukweli, mtu mnafiki atatoka hapa atapiga debe akitoka huko nje, aah tunaenda vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi, nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shabiby, tunaendelea na Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, wajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Asya Sharif Omar, na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, leo kwa mara ya kwanza ninasimama ndani ya Bunge hili Tukufu kwa ridhaa ya wananchi ya Jimbo la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanadiplomasia nguli Afrika na dunia ambaye alichaguliwa na Watanzania kwa zaidi ya 97%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi ule ulitafsiriwa na kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miaka yake minne ya uongozi, lakini alionekana kwenye mikutano mbalimbali ya wananchi kwa namna ambavyo wananchi walifurika kadiri ambavyo alikuwa akitembea katika mikoa yote takribani 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzunguka kwake, ahadi zake zilisheheni matarajio ya Watanzania, na ahadi zake zilimgusa

Mtanzania mmoja mmoja. Wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani, alikuja na falsafa ya *4R*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika falsafa yake ya *4R* ilimfanya kutambulika duniani na Mataifa ya nje na kupelekea kuwa kinara kwenye masuala ya haki za binadamu, uhuru wa habari, uhuru wa dini na kadhalika. Kiongozi ni lazima uwe na ngozi ya mamba. Hata nyakati ambazo zilikuwa ngumu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alituvusha salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka tulipata fedha za *IMF* kwa ajili ya kuzuia na kujikinga kipindi kile cha *Covid*. Tunao Ushahidi wananchi wa Jimbo la Kivule tulipata takribani shilingi bilioni 4.6. Dkt. Samia Suluhu Hassan aligeuza kuwa fursa na tukapata zaidi ya madarasa 232, wananchi wa Jimbo la Kivule wanapata elimu iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukasema ya kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi kubwa aliyoifanya na mageuzi makubwa aliyoyaleta katika mashirika ya umma ilikuwa ni chachu ya kuwaletea maendeleo kwa wananchi wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma kwa haraka haraka mambo makubwa na mageuzi aliyoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka yake minne. Kwanza aliongeza *Government Investment Value* kukutoka shilingi trilioni 67 hadi shilingi trilioni 92, sawa na 36% ya ongezeko la mitaji katika mashirika ya umma. Kwa maarifa hayo ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilimpelekea kuvuna fedha nyingi za gawio la Serikali kutoka shilingi bilioni 637 hadi shilingi trilioni 1.028 mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika kwenye mageuzi. Tumeona namna ambavyo Serikali imewekeza katika mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Tumepata ongezeko kutoka shilingi bilioni 153 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 263 mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 72%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameendelea kuimarisha mashirika ya kimkakati. Shirika la *TANESCO* lilikuwa linajiendesha kwa hasara, lakini leo hii faida imeongezeka kutoka shilingi bilioni 8.9 hadi shilingi bilioni 21.9 yenye *capital* ya shilingi trilioni 2.4. Tumeona mashirika mengine kama *TPDC* ambao wametoka *profit* ya shilingi bilioni 159 hadi shilingi bilioni 306 kwenye mtaji wa shilingi trilioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mashirika ambayo yalikuwa hayatoi gawio, mfano *TAZAMA Pipeline* leo hii imeendelea na Serikali inapata faida kutoka kwenye magawio na maeneo hayo. Pia tumeona namna gani tumeendelea kuongeza hisa katika kampuni za madini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2017. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mageuzi makubwa, lakini hayakuishia tu kwenye Kitaifa, mageuzi haya yameshuka chini na kumgusa mwananchi mmoja mmoja. Hivi leo mimi ninavyozungumza hapa Jimbo letu jipya la Kivule halikuwa na maji, kwa maana maji yalikuwa ni asilimia sifuri. Leo tunapozungumza ndani ya miaka yake minne maji yamefika 48%. Amejenga tenki kubwa la maji la lita milioni tisa lenye thamani zaidi ya shilingi bilioni thelathini. Maji yale yanatembea Ilala nzima, kwa maana Jimbo la Segerea, Jimbo la Ukonga zamani, pamoja na Jimbo letu jipya la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mitambo ile ya maji aliyoinunua kwa kila mkoa takribani mwezi mmoja uliopita, kaka yangu Mheshimiwa Juma Aweso alikuja Jimbo la Kivule na watu wa Kivule tukapata mitambo ile, na sasa visima takribani 10 vinaendelea kuchimbwa ndani ya Jimbo letu Jipya la Kivule *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha masuala ya maji, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa katika sekta ya elimu. Leo hii sisi wananchi wa Kivule tulikuwa hatuna kidato cha tano na cha sita, lakini sasa zimejengwa shule za sekondari mpya za kutosha, tena nyingine zenye hadhi ya gorofa. Tunayo

Shule ya Sekondari ya Kitunda Relini, tunayo Shule ya Sekondari ya Kipunguni zenye hadhi ya ghorofa ndani ya Jimbo leu jipya la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye sekta ya afya, jimbo lile ni jipya, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani hakukuwa na kituo cha afya hata kimoja, leo tunapozungumza kwenye kata zetu zote sita tuna kituo cha afya kimoja kikubwa kwenye Kata ya Kivule chenye mfano wa hospitali ya Kiwilaya, na kingine kikubwa zaidi Kata ya Mzinga zenye thamani ya shilingi bilioni 4.9 chenye thamani hiyo, na vifaa vya kutosha. Wananchi wa Kata ya Mzinga na Jimbo la Kivule wanapata huduma ya afya kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa, kwenye mpango ambao tumeuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tarehe 14 Novemba, Mheshimiwa Rais ametoa dira lakini pia ametupatia hotuba. Hotuba yake ilisheheni mahitaji ya Watanzania hasa vijana na akina mama. Utaona namna gani alikuwa anajaribu kuunganisha ujenzi wa vyuo vya *VETA* pamoja na mikopo ya 10% ya akina mama na vijana ili kuweza kutengenza matajiri wa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuona *congestion* kubwa kwenye Chuo cha *VETA* cha pale Chang'ombe ambacho kipo Wilaya ya Temeke, nasi watu wa Ilala sasa tunakwenda kupata Chuo chetu cha *VETA* ndani ya Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumepata fedha kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kaka yangu Elihuruma, tumenunua eneo kubwa la hekari tisa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* ili kuweza kuwanyanyua na kuwasaidia vijana wanaoishi ndani ya Wilaya yetu ya Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tunaomsaidia Mheshimiwa Rais, tunapaswa *ku-walk the talk;* yaani kutembea mle ambapo Mheshimiwa Rais anatarajia. Hapa imetajwa sekta yetu ya ujenzi,

amesema anakwenda kuongeza bajeti *TARURA* na kuongeza bajeti kwenye Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu pale, Mheshimiwa Chaurembo aliuliza swali, Barabara ya Msongola kuelekea Mbande mpaka Chamazi, tukapata majibu ya Naibu Waziri kuwa ni kusuasua na uwezo wa mkandarasi. Sisi watendaji tunapaswa kupata wakandarasi watakaotusaidia kupata *value for money* na ku-*achieve* zile *5R of procurement* ili miradi yetu iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi Barabara yetu ya kutoka Banana – Kitunda – Kivule – Msongola tayari mkandarasi anaifanyia kazi, na tumeahidiwa kufikia mwezi wa Nne lami ile itakuwa imekamilika na wananchi watakuwa wanaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wetu wa Kiserikali, Waheshimiwa Mawaziri, waendelee kuliangalia kwa jicho la kipekee Jimbo letu Jipya la Kivule. Barabara ya kutoka Pugu kuelekea Majohe kuelekea mpaka Mbondole; Barabara ya kutokea pale Kitunda kuelekea Magole kupitia Nyangasa; Barabara hiyo hiyo kutokea Kitunda kuelekea Mwanagati ni takribani kilomita thelathini na nane, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameziorodhesha kwenye Ilani ya Chama cha mapinduzi. Kazi yetu sisi ni moja tu, kusimamaia mradi ule wa *DMDP* uweze kukamilika kwa wakati na barabara nyingine zilizobakia takribani kilomita 50 ndani ya Jimbo letu Jipya la Kivule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, itoshe kusema ya kwamba, sisi wananchi wa Kivule tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia jimbo letu jipya, na kutupatia mwakilishi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nasi tupo tayari kumsaidia Mheshimiwa Rais kuisimamaia Serikali kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, wajiandae Mheshimiwa Asya Sharif Omar, na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupata kura nyingi sana kwenye Uchaguzi Mkuu. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mvomero kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo la Mvomero kwa kura nyingi za kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, na niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kusema kwamba hotuba ile imeleta matumaini makubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninukuu maneno ya mwisho kabisa kwenye hotuba ile ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyazungumza hapa Bungeni, kwamba anatamani sana kipindi chake cha awamu ya pili anapokwenda kumalizia ngwe hii, basi akiondoka aache wananchi wa Tanzania wakiwa na tabasamu. Kwa kweli ukisoma ahadi zilizokuwa kwenye hotuba ile, hakika Watanzania wataachwa na tabasamu kubwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze sana Tume Huru ya Uchaguzi kwa kazi waliyoifanya hasa ya kuongeza vituo vya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tunaotoka kwenye majimbo ya vijijini, majimbo yenye changamoto za kijiografia, zenye milima na miinuko mikubwa, majimbo ambayo wananchi wake ni wakulima, wafugaji, (wafugaji wale ambao wanategemea asubuhi wafungue maboma, watoe mifugo wakachunge jioni warudishe), wananchi ambao ni wajasiriamali wadogo wadogo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu kitendo cha kuongeza vituo vya kupigia kura kimesaidia sana wananchi wengi wa makundi haya

ambao iliwalazimu hata kama siku ilikuwa ni ya mapumziko ya kupiga kura, lakini wao ambao wamejiajiri sekta binafsi kuweza kutoka mapema kwenda kupiga kura, kurudi kufungua maboma yao kwenda kufanya shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wajasiriamali wadogowadogo, wakina mama wanaouza mbogamboga sokoni, mama lishe, bodaboda na wafugaji wote waliweza kupiga kura kwenye majimbo yetu ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa tunashukuru, wale ambao tumetoka kwenye majimbo yenye miinuko mikubwa (milimani). Jimbo la Mvomero kata 15 tarafa mbili zipo kwenye milima; wananchi wengi hasa wa makundi maalum: wakinamama, wajawazito, walemavu, na wazee walikuwa wanatamani sana kufanya takwa lao la Kitaifa kipindi cha nyuma kwenye michakato mingine ya uchaguzi, lakini walikuwa wanashindwa kwenda kupiga kura kwa sababu ya changamoto za kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sasa vituo vya kupigia kura vilikuwa vya kutosha ndani ya Jimbo langu la Mvomero tulikuwa na vituo 711. Vituo vilikuwa kwenye maeneo ya makazi ya watu, maeneo yenye wafanyabiashara, na kwenye maeneo ya shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, wakinamama na makundi mengine waliweza kutumia fursa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kutokuwa na misongamano sehemu za kupigia kura kulihamasisha sana wananchi kujitokeza kupiga kura. Kipekee wamenituma wananchi wa Tarafa ya Mgeta, Tarafa ya Mvomero ambazo ni kata 15 na kata nyingine 10 za wafugaji kwamba Mheshimiwa Mbunge uende ukampongeze Mheshimiwa Rais na wananchi, nao wamefanya takwa lao la Kikatiba kwa mara ya kwanza kupiga kura nyingi. Kwa hiyo, tunashukuru sana Serikali kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ndani ya siku 100 mambo aliyokuwa ameahidi kuyafanya kwenye hotuba hasa kwenye umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha anakamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere. Amehakikisha vijiji vyote nchi hii vinapata umeme. Aliahidi kwamba vitongoji ambavyo havijapata umeme ataanza kutekeleza hiyo ahadi, na tunaona ndani ya siku 100 tumeenda kupata miradi ya vitongoji 9,000 ndani ya nchi hii na Jimbo la Mvomero tumepata vitongoji 93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua bado vitongoji 13,000 ambavyo bado havijapata lakini tunaamini kwa *speed* na kasi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchi yote na vitongoji vyote vinaenda kupata umeme. Kama ndani ya siku 100 ametuletea vitongoji 9,000, tunaamini kabisa kwamba vitongoji vyote vinakwenda kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwenye suala la maji wenzangu wameongea mambo mengi na tunatambua kazi kubwa aliyofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama vijijini na mijini. Huko nyuma tunaona kwamba 84% mpaka 91%, upatikanaji wa maji umeongezeka mijin, na 70% mpaka 85%, upatikanaji wa maji umeongezeka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba maji haya yanapatikana kipindi kile kukiwa na mvua tu, kukiwa na kiangazi hali ya upatikanaji wa maji nchini inakuwa ni changamoto. Sisi tunaotoka kwenye maeneo ya wakulima na wafugaji, migogoro ya wakulima na wafugaji inakuwa mingi kwa sababu wafugaji wanahamia kutafuta maji, kwa hiyo tumekuwa na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa kwenye Hotuba yake kwamba anakwenda kujenga ujenzi wa gridi ya Taifa ya maji, na

maji haya sasa yatatoka Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, na Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, hatutatumia tena na kutegemea maji ambayo yanatoka kwenye mito ambayo yanategemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Ni kwamba sasa kwa miaka mitano hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakulima wanaenda kupata maji ya kutosha, wafugaji watapata maji ya kutosha, viwanda vitapata maji ya kutosha, matumizi ya majumbani maji ya uhakika, safi na salama yatapatikana. Kwa hiyo, hata wananchi wangu ambao wengi ni wafugaji, tutaenda sasa kuwekeza ile ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba wafuge kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajenga majosho, tutaleta madume na mbegu bora za mifugo kwa sababu sasa tunaachana na biashara ya kuhamahama. Vilevile, wakulima nao watafanya kazi za kilimo na kujielekeza kwenye shughuli nyingine za uzalishaji mali kuliko ilivyokuwa sasa hivi wanashinda kwenye mashamba kufukuza mifugo. Kwa hiyo, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuiunge mkono Serikali yetu ili haya ambayo Mheshimiwa Rais anaenda kufanya mapinduzi makubwa kwenye masuala ya maji tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameahidi kuongeza maeneo ya wakulima hasa kilimo cha umwagiliaji kutoka ekari milioni tatu mpaka milioni tano, na kupima maeneo ya wafugaji kutoka ekari milioni tatu mpaka milioni sita. Tunaamini kabisa utekelezaji wa jambo hili unaenda kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sasa Serikali yangu na Wizara na taasisi za Serikali, Mheshimiwa Rais ameahidi kuweka kongani za viwanda kwenye wilaya. Tunajua kuna suala la kibajeti, lakini kuna mambo ambayo hayahitaji bajeti, basi Serikali na taasisi zinazohusika zikamalize migogoro ya ardhi kwenye maeneo ambayo tumetenga kwa ajili ya kongani za viwanda ili tukiyasubiri hayo ya kibajeti, basi maeneo haya yawe tayari ili tunapopata wawekezaji maeneo hayo wayakute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa Wilaya ya Mvomero eneo la Dakawa kutujengea mradi wa umeme wa kilovolti 220 kwa ajili ya viwanda vya Turiani na maeneo ya Gairo na Kilosa. Tunaiomba Serikali ifanye hivyo ili wananchi hawa waweze kufaidika na kupata ajira nyingi kupitia uwekezaji wa viwanda, kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuweza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze ku-*support* au kuchangia hotuba ambayo aliwasilisha Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 14 Novemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi Taifa, kuwashukuru jumuiya yangu ya UWT Taifa, kuwashukuru sana wapigakura wa Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba, Jumuiya ya UWT wanawake kwa kuendelea kuniheshimisha na kuendelea kuniamini kwa uadilifu mkubwa kuweza kunichagua na hatimaye leo nikasimama kuwa Mbunge. Sitawaangusha, na nitaendelea kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kuwatumikia wananchi kwa unyenyekevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo katika hotuba ile ya Mheshimiwa Rais utajikita kwenye Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Lazima wananchi tumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ametufanyia makubwa wananchi wa Tanzania tukiwemo wanawake. Ameweza kutoa shilingi bilioni 10.5, fedha hizi tayari zinapatikana *NMB Bank* na ni kwa malengo makubwa ya kutusaidia wanawake tukiwepo wafanyabiashara wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ile ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 14 Novemba, ilijaa maono ya kiuchumi ambayo imekwenda kumnyanyua mwanamke na mfanyabiashara mdogo kutokana na maisha tegemezi. Shilingi bilioni 10.5 zile ambazo tayari zimeanza kuwanufaisha kwa wale wananchi ambao wamesajiliwa na wapo sahihi katika kukopesheka na tayari wameanza kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hatuna cha kumlipa ila tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu atamvisha joho na huruma, lakini atampa malipo yake ya duniani na kesho tunapokwenda. Ametunyanyua wanawake, leo wanawake tumeondokana na maisha tegemezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 10 ile imeenda kunufaisha babalishe, mamalishe, wasusi, wafanyabiashara ndogo ndogo, na bodaboda. Vijana wetu wote hawa wameweza kunufaika na pesa hizo. Nani kama Mheshimiwa Mama Samia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme ukweli, Watanzania Mheshimiwa Dkt. Samia ametuheshimisha. Kufuatia mkopo huu ambao umenyanyua hali zetu wanawake wa Tanzania tena wanyonge, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ametujengea uwezo wanawake mjini na vijijini, tena wadogo wadogo, tumeweza kukopesheka bila ya masharti magumu. Masharti nafuu yametupa fursa ya kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hadi hapa ninazungumza, kulikuwa na kilio kikubwa kwa wanawake wenzetu huko chini walikuwa wanapitia magumu. Wamenyanyasika, lakini Mama Dkt. Samia kawa mkombozi wa

wanawake wa Tanzania na hasa wanyonge. Tunataka nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokitaka ni kuendelea kumwombea dua Mheshimiwa Rais wetu na tutamuenzi kwa nguvu zote kwa sababu ametuheshimisha wanawake. Kama tunavyofahamu, mwanamke ndio kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, lazima niseme ukweli, ninampenda sana Mama Samia. Ninasema kwa hisia, wanawake leo tuliopo chini tumeweza kumiliki kujenga majengo sisi wenyewe. Kama haitoshi, sasa hivi tunasomesha watoto wetu. Kama haitoshi tumekuwa wafanyabiashara wakubwa, tunakwenda mpaka nchi za Kiarabu. Sisi wanawake tunapanda ndege tukishuka tunapishana na wakina baba. Ukija masokoni tunaongoza; ukija kwenye *business* tunaongoza; ma-*pilot* tunaongoza. Wanawake wote tunaongoza kwa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeuri hii tumeipatia kutoka kwa Mama Samia, ameweza kutujengea nguvu ya uwezeshaji. Kwa nini tusiseme? Lazima tuseme, Mama Samia tunakushukuru umenyanyua hali zetu wanawake, tena wale wanyonge kabisa umetunyanyua. Leo ninavyozungumza, mimi ni Mbunge wa wanawake UWT, lazima nitetee wanawake wenzangu, lakini lazima nijenge heshima aliyotupa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani ilikuwa wanawake tunanyanyasika, ndoa zetu hazitulii, lakini shilingi bilioni 10.5 zimeenda kujenga heshima ya ndoa zetu. Ni kweli zimekwenda kujenga heshima ya ndoa zetu. Baba anahangaika na mambo mengine mpaka wanaogopa, maana yake akitoa fedha ya mboga, tunatoa fedha ya shule ya mtoto; akianza kujenga msingi, sisi tunanyanyua juu tunaezeka nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni shilingi bilioni 10.5, lakini imetujengea mazingira mazuri, tumekuwa na afya ndani ya majumba na ndoa zimeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa wanawake tunahangaika na kaushadamu. Kaushadamu ilituumiza wanawake hasa wa vijijini, tulikuwa tunatolewa magodoro nje, tunatolewa vikombe vyetu, hatuna amani. Mume unampenda lakini unamchukia, lakini Mama Samia kajenga heshima ya familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza mchango wangu huu ninaomba sasa niseme, fedha hizo zipo na zinaendelea kutolewa *NMB* mjini na vijijini na riba yake ni ndogo, asilimia saba. Kwa hiyo, hii utaona namna gani Mama amekusudia kumnyanyua mnyonge na siyo tu kutoa fedha na fedha zinapatikana *NMB. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, tuitumie fursa hii kuhakikisha wanawake hawa zinawafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, niseme ninashukuru sana. Ninaomba kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ajiandae Mheshimiwa Hamisi Taletale, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Johnston Johansen Mutasingwa.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie fursa hii adhimu sana kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uzima iliyotuwezesha sote kuweza kukutana kwenye jengo hili Tukufu kwa ajili ya kujadili mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu kipekee kabisa na kwa shukrani za unyenyekevu kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nachingwea kwanza kwa kukubali, kuridhia na kunichagua mimi kuwa Mbunge wa Jimbo la Nachingwea. Pili, kwa kumchagua kwa kura nyingi na za kishindo, na za heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tatu, kwa kushiriki na kuendesha vizuri zoezi la Uchaguzi Mkuu toka katika kipindi cha kampeni mpaka siku ya kupiga kura wakiwa wamejijengea utulivu wa kuchagua viongozi waliowapenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu moja kwa kuchaguliwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimeisoma na nimeipitia hotuba aliyoitoa Bungeni tarehe 14. Katika hotuba ile Mheshimiwa Rais amejielekeza katika vipaumbele, ameonyesha umadhubuti, ameonyesha nia na amefungua mwanga wa Tanzania kubwa tunayoitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweka vipaumbele mahususi na amejipambanua kutokana na mwelekeo wa nchi ya dunia ya sasa inavyotakiwa kwenda kwa kuzingatia masuala mtambuka mbalimbali yanayoijenga dunia ya leo katika masuala ya kimaendeleo katika maeneo ya teknolojia, huduma za jamii, hali za vijana na mambo ya usalama wa nchi. Mheshimiwa Rais kila kitu amekiweka vizuri. Naomba kutumia fursa hii kumpongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba hotuba hii aliyoitoa hapa Bungeni ndiyo itakuwa dira, itakuwa mwelekeo na ndiyo itakuwa tochi itakayotuangazia Watanzania kuyaelekea maendeleo ya kweli katika siku zote za kuitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba Mheshimiwa Rais amejipambanua wazi kabisa, lakini ninaomba uridhie niweke jambo moja kutoka katika kitabu kitakatifu. Kwa wale wasomaji wa Biblia watakubaliana na mimi kwamba baada ya Musa kuwachukua Wanaisraeli kutoka nchi ya utumwa alipowapeleka kwenye nchi yao ya utawala na kuishi, Musa ndiyo alikuwa kiongozi aliyetumainiwa,

aliyetegemewa na ambaye alionekana ndiyo mustakabali wa Taifa la Wanaisraeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biblia inaeleza na hadithi iko wazi kabisa Musa naye alikufa sambamba na kuwa alipendwa na alihitajika. Wakati Musa anawaacha Wanaisraeli ni kama Taifa ambalo liliulizana nani anakuja kuwa Musa wa pili atakayetuvusha na kutupeleka kwenye nchi ya asali iliyoahidiwa. Mungu akamwinua mtu anaitwa Joshua akamwambia wewe ninakupa kazi ya kuwachunga kondoo wa Israeli na wafike kwenye nchi ya asali na maziwa wakiwa salama na wenye furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimsoma vizuri Joshua katika maandiko matakatifu anasema wakati anapokea nafasi ya uongozi hata yeye mwenyewe alibaini kwamba wako watu wanaweza wasielewe na kuamini kuwa ni Joshua mwenye nguvu atakayevusha wana wa Israeli ndipo Mungu akamwambia Joshua uwe hodari na moyo wa ushujaa, usiogope wala usifadhaike kwa kuwa Bwana Mungu wako yuko pamoja nawe kila uendako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niyachukue maneno haya niyaweke katika fikra, mwelekeo, mtazamo na dhima ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba amepokea kijiti kutoka kwa Musa na wakati anapokea inawezekana yako mashaka lakini kwa kazi, huduma na mwelekeo aliouonesha katika kipindi cha miaka minne mpaka sasa inatosha kabisa kutupa matumaini ya kuvuka bila mashaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi na Watanzania wenzangu kama leo dunia itatuamsha na kuuliza Rais wa Tanzania anapenda nini? Jibu nitakalolitoa nikiwa nimeamka anaipenda nchi yake kuliko kitu chochote. Kama leo dunia itaniuliza unajivunia nini kwa Rais wako, nitawaambia nitajivunia kuwa na Rais aliyewatoa watoto wa kimaskini kutembea umbali mrefu kufuata elimu kwa kuwajengea mabweni na shule karibu na maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama dunia itaniuliza kwa nini unamsemea Rais wako nitawaambia ninamsemea Rais aliyeendeleza na kufufua miradi mipya ya kimkakati ambayo ingeweza kukatisha tamaa. Nitawapa ushuhuda wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Daraja la Kigongo Busisi, Miradi mikubwa ya Hospitali za Kanda, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Rufaa, Hospitali za Wilaya, Zahanati pamoja na Vituo vya Afya ambavyo Dkt. Samia Suluhu Hassan amevijenga kwa nguvu, uwezo na mapenzi makubwa kwa nchi yake ya Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. ZAINABU R. KAWAWA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza msemaji, mdogo wangu Fadhili Liwaka, lakini ninataka kumwongezea taarifa kwamba nami pia nitamsemea Mheshimiwa Rais kwa mradi mkubwa wa Bandari ya Uvuvi katika Wilaya ya Kilwa, hii ni bandari ya kimkakati ambayo iko katika 90% na zaidi, hivi karibuni inakaribia kumalizika, lakini ni Bandari kubwa katika ukanda huu wa Nchi za Afrika Mashariki ambayo haijawahi kujengwa popote pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, Mheshimiwa Fadhili unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti kwa dada yangu ninayemheshimu sana na bado ninamwongezea kwamba dunia ikiniamsha juu ya Uchumi wa Bluu nitawaambia ninamsemea Rais aliyethubutu kujenga Bandari za Uvuvi, kujenga meli za usafirishaji za watu na mizigo na aliye tayari kuhakikisha kwamba wavuvi kwenye Ukanda wa Maziwa na Bahari Kuu wanapata mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo na kuweka mwelekeo wangu na mtazamo ambao ninatamani kila Mbunge na Mtanzania auone kwa Rais wetu, ninaomba nijielekeze kwenye mambo matatu ambayo kwenye hotuba Mheshimiwa Rais ameyaweka vizuri na sisi tunahitaji msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nitumie fursa hii sasa kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia niwapongeze Mawaziri waliotoa huduma kwenye Wizara ya Madini. Moja kati ya jambo kubwa ambalo nchi yetu inaweza kujivunia ni uwepo wa rasilimali ya madini, tena madini yenye thamani kubwa sana hata pale nchi yetu inapotoa sauti duniani juu ya kwamba tunayo thamani ya madini ambayo inamezewa mate hatutoi kwa bahati mbaya au kujifurahisha, tunatoa kwa sababu mlio wa mgonjwa, anayeujua ni muuguzi na sisi ndio wauguzi wa nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo hili Serikali imeweka mikakati madhubuti; moja, kuhakikisha tunavutia uwekezaji katika eneo hili la madini na tumeona pato la Taifa limeongezeka kutoka kwenye Sekta ya Madini kutoka asilimia 6.8 mpaka 10.1%. Hii ni kazi kubwa sana na imefanywa na sekta pamoja na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mavunde na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya usimamizi na sisi sote tutakuwa mashahidi tumeona Wizara ikihangaika. Jambo la kwanza ni kuweka utaratibu mzuri wa uwekezaji kwenye eneo la madini, lakini eneo la pili, kuhakikisha Watanzania wanakuwa matajiri kwa kuwa wachimbaji wazuri kupitia maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niungane nao na kuwatia shime kwamba moja ya jambo litakalolitoa Taifa na kusogea mbele zaidi kwenye eneo la Sekta ya Madini pamoja na mikakati iliyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha tunaongeza thamani ya madini, tunafungua kituo cha uzalishaji wa madini *East Africa.* Hata hivyo, ni sharti letu la msingi na ni muhimu

kuwatambua, kuwaelekeza na kuwajenga wachimbaji wadogo nchini ili waweze kupata ngazi ya utajiri na kuwa wachimbaji wakubwa ili tuwe na Taifa lenye thamani ya mali zilizopo hapa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa uchimbaji wa madini nchini unakwenda vizuri kwa sababu tumeona leo tukihesabu idadi ya Watanzania waliopata uwezo wa kujisimamia na kuweza kufanya shughuli za uchimbaji haiwezi kulinganishwa na miaka 15 iliyopita, kwa sasa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaomba niweke maneno yangu kwenye jambo moja. Nimesoma vizuri hotuba Mheshimiwa Rais na nimeona mwelekeo katika suala la kupambana na kusaidia kuwaondoa wanyama waharibifu ambao ni ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka jimbo ambalo 75%, wakati ninaomba kura ya wananchi kila nilipokwenda moja ya hoja niliyokutana nayo ni wanyama waharibifu aina ya Ndovu. Ninafahamu ndovu hawa wanalindwa na sheria maalum ya kimataifa. Ziko nchi ambazo ziliwahi kupitia changamoto kubwa ya wanyama wengi wa aina hii kama vile *Sri-Lanka, India, Sierra Leone* na nchi zingine nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mahususi ambayo kama nchi tukiamua kuyaweka tunaweza kusaidia kuwaondoa wananchi wetu kwenye adha ya hawa wanyama ambao sio tu wanamaliza mazao ya watu bali wanahatarisha usalama na maisha ya Watanzania kwa sababu wanaua. La kwanza ziko njia ikiwemo zile ambazo zimeainishwa na Wizara. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kuwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamis Taletale, atafuata Mheshimiwa Johnston Johannes Mutasingwa na wajiandae Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu *Azza wa Jallah* kwa kunifanya nimerudi salama Bungeni, lakini pia ninakishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi na nimshukuru Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Vile vile niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa kunirudisha mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Morogoro Kusini Mashariki tuna neno letu tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia anatosha wengine watatuchosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wabunge wa mikoani, sisi ni Mkoa ambao ulipata nafasi ya kwanza ya kutembelewa na Mwenyekiti wa Chama chetu na Rais Wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania. Alifika nyumbani kwetu pale Ngerengere kwa mara ya kwanza, lakini yale ambayo aliyoyaongea Ngerengere na ndiyo ambayo ameyaongea ndani ya hili Bunge. Niseme kidogo, sisi Wanamorogoro Vijijini, Wanamorogoro Kusini Mashariki tuna mengi ya kujivunia, tuna mengi ya kusema juu ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na sekta ambayo ukiniona nimesimama ninaonekana *yes big* wa Kisaki amesimama, lakini Rais alipokuja jimboni akasema jina hili halikufai ninalichukua mwenyewe. Wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni ila kuna kauli imetoka Mheshimiwa Dkt. Samia si mnyonge tena. Kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia si mnyonge tena shughuli yetu kumpa haki yake, Mheshimiwa Dkt. Samia apewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, wakati amepita Morogoro Kusini Mashariki alielekeza Wizara ya Fedha, tayari

tumeletewa bilioni nne na Mkandarasi ameanza kazi. Tunasubiria mchele kidogo uendelee, kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Sekta ya Elimu. Ukitazama sisi watu wa vijijini tuna kila sababu na neno la kusema, nami niiombe Wizara ya Elimu kwa kuwa Rais ameyafanya makubwa shughuli yenu ni kwenda kuyatangaza yale ambayo Mheshimiwa Rais amefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mtaala wa Elimu tunasoma miaka 10, kwenye hii miaka 10 hii miaka minne kuna Mtaala wa Amali. Kwetu vijijini, mimi kwangu kwenye Kata yetu ya Tomondo Mheshimiwa Rais, ameleta Shule ya Amali maana unasoma Sekondari baada ya hapo unasoma ufundi kuanzia *form one* mpaka *form four*. Leo hii ukitoka hapo unakuwa una cheti cha *form four* na una cheti cha ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ameangalia dunia inataka nini? Dunia inataka utaalam ujuzi. Kwa hiyo, ujuzi unaanzia kuanzia *form one* mpaka *form four*. Leo hii Vyuo vya *VETA* vilivyojengwa nchini ndio maana kauli yangu ninairudia kwa kumwomba kaka yangu Profesa Mkenda na dada yangu Mheshimiwa Wanu kuongeza na kuwekeza kwenye matangazo kuitangaza Wizara ya Elimu ili kesho na kesho kutwa watu wajue nini kimepelekwa kule chini. Nina ushahidi, sisi sasa hivi hatuna changamoto ya kuchangisha changishana, Rais ameshusha hela za shule kule chini watu hawajui na ndiyo maana wanayasema wasiyoyajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nipende kusema kwamba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea vijana wawili machachali kwenye Wizara yetu ya Michezo. Maana kuna mmoja anafoka, mmoja anahubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ina Mchungaji na Mwanamziki; kwa hiyo kwa hili unaloliona tumeona sura nzuri na mwanzo mzuri wa *AFCON*. Tumwombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya michezo, sisi Wanamorogoro Mkoa kwa ujumla

ukiangalia soka la hii nchi hatusemi kwa sababu ninavutia ngoma kwangu, soka la hii nchi sura ya kubwa iko Mkoa wa Morogoro. Tuiombe, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kubwa sana kwenye kuwekeza michezo, viwanja vya michezo Morogoro sisi tia maji, tia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara ya Michezo Mheshimiwa Rais ametuletea SGR kama kuna treni inayojaa nchini ni treni ya Dar es Salaam – Morogoro, kama tunakwenda kwenye *AFCON* lazima tuwe na *parking* ya michezo pale, hata wachezaji wanaokuja mazoezi watacheza Morogoro Mjini, Mbugani watakwenda Mikumi. Ninajua hili suala ni dogo sana kwao Mawaziri hawa wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hajakosea kumweka Mchungaji, kumweka na mwana *Hip hop,* ana maana yake. Maana hii sisi tunatakiwa twende tukajivunie kwenye hii Sekta ya Michezo na kwa uenyeji wetu wa AFCON ya mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme jambo dogo hapa kama tunatazama wachezaji waliocheza juzi pale *Morocco* ni wachezaji wenye viwango vizuri, wachezaji wanacheza vizuri lakini kama sisi hatujaangalia utaratibu ambao wanafanya wenzetu kuchukua wachezaji wa nje ambao wenye uraia wa Tanzania, nani atafanya? Ninaamini Mheshimiwa Makonda anaweza, ninaamini Mwana *FA* anaweza. Waende wakamwombe Rais, mikono yake misafi, moyo wake mweupe kwenye michezo, ndiyo mwanamichezo namba moja nchini mwanamichezo ambaye ameonyesha sera yake ya kuinua michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunakuja kuwa wenyeji wa *AFCON*, sasa twende tukawachukue wale watoto wetu wengine ambao wako nchi za nje ambao ruhusa ya kisheria inawasumbua kurudi ndani. Naamini hilo linawezekana kwenu. Hakuna kitu kizuri kama kuchanganya ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwenye hili kama tunapata Rais mwenye maono haya ya Mama Samia wa leo hii, huyu Rais

anazaliwa mara moja tu anatoka mara moja tu, kama tumempata huyu tumtumie vizuri. Michezo ni ajira michezo ni pesa michezo ni utajiri na yeye ameweka mguu kati kwenye michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka kwenye michezo tunajua Mheshimiwa Rais ameleta pesa kwa ajili ya Mfuko wa Sanaa na anafanya vizuri. Utaratibu wa Mfuko wa Sanaa umekwenda kisheria sana. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya sanaa aende akamsaidie Rais kwenye hili. Wasanii wanategemea kupata pesa hapa, waende kama kuna utaratibu wa kisheria sisi ndiyo watunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Daktari Tale Tale, namshauri Mheshimiwa Waziri walete sheria hapa, tuwasaidie wasanii.  Kama kuna utaratibu wa kukopeshwa hizi pesa ambazo Mheshimiwa Rais amezileta wapewe.  Kama utaratibu huu ni mgumu tunauona ambao wameujenga, eti ninataka kukopa pesa ambayo ameileta Rais kwa furaha yangu ninataka niweke nyumba, si kila msanii ana nyumba. Hili neno nilisema huko nyuma na Mheshimiwa Rais juzi ametilia msumari kwenye hotuba yake amesema anataka wasanii vijana wawe na furaha: furaha sioy kukosa kile alichokileta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho ambacho ningependa kukisema na kupenda kukisifia kwa Mheshimiwa Rais wetu, mimi Hamis Shabani Taletale kwenye Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ametuletea Mradi wa Morong'anya wa zaidi ya bilioni 23, ule mradi unalisha maji vijiji zaidi ya 19. Kwenye Kata yetu ya Tomondo, tulikuwa tunakunywa maji ya Nzasa, leo hii tunakunywa maji baridi, nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? Halafu leo hii atoke mtu amseme Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakunywa maji baridi kutoka vijijini, leo hii ameleta Mradi wa bilioni nne kwenye Kata yetu ya Mkambarani.  Vile vile sisi tumekuwa hifadhi ya kupeleka maji mjini kutoka kwenye Bwawa la Kidunda. Leo hii tuna uhakika Watanzania wanaoishi Dar es Salaam wanakwenda kupata maji kutoka kwa sisi Wanamorogoro Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuyasema haya machache ninarudia tena Mheshimiwa Dkt. Samia siyo mnyonge na wala hatumnyongi, tunampa haki yake. Ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamis Taletale, ahsante sana. Mheshimiwa Johnston Johannes Mtasingwa, Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma ajiandae na tutamalizia na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia afya njema na tunaendelea na michango yetu sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini na kwa heshima kubwa sana niwashukuru kwa kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninapenda kuchangia katika hotuba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nimesoma kitabu kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa 40. Nimeitafakari sana Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ni hotuba ambayo inatoa maono na mwanga kwa Mheshimiwa Rais anataka nini na anataka nchi iendeje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya na katika Jimbo letu la Bukoba Mjini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenda mambo makubwa sana na ninaweza nikasema ni muujiza ambaye hajawahi kutokea katika jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ametuletea shilingi bilioni 9.016 katika barabara za *TARURA* ni jambo ambalo halijawahi kutokea katika jimbo letu la Bukoba Mjini na sasa anakwenda

kuongeza pesa katika barabara za *TARURA*. Sasa anapokwenda kuongeza pesa katika barabara za *TARURA* niwaombe, *TARURA* sasa zile kilometa 133.87 ambazo wilaya yangu ya *TARURA* pale Bukoba Mjini imeziomba ili iweze kuzihudumia, niombe sasa waende kuziangalia ili mwananchi anayeishi Bukoba ziweze kumsaidia na kupandisha uchumi wake na hii ndiyo sera ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara inayotoka Kahororo kwenda Makongo hadi Ntoro. Hii Barabara inakwenda kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema anakwenda kukuza sekta binafsi. Kule kuna watu ambao wanachimba kokoto wanapiga mawe na inaenda ziwani. Niombe sasa tuweze kuiangalia ili iweze kutengenezwa, ina urefu wa kilometa 4.73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuleta miradi mikubwa na ya kimkakati katika jimbo letu ambayo ina thamani ya shilingi bilioni 40.04 katika Miradi ya *TACTIC*. Tunakwenda na tunajenga soko kubwa la Bukoba Mjini pale. Tunajenga Stendi yetu ya Kyakairabwa na tunajenga barabara kilometa 10, lakini tunakwenda kuweka taa 412. Hili ni jambo la kihistoria ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelifanya katika Jimbo letu la Bukoba Mjini ninasema mama ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la miundombinu sasa anatujengea barabara ya njia nne ambayo inaingia katika mji wetu wa Bukoba Mjini. Ametutumia shilingi bilioni 12 kwa awamu ya kwanza ambapo anajenga kilometa 1.6 likiwemo na Daraja la Kanoni. Niseme ahsante sana Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika miradi hii, maana thamani ya pesa anayotoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi na kwa ajili ya kukuza uchumi wa Taifa letu sasa inaonekana wazi. Niombe miradi yote inayotekelezeka katika Wizara zetu, wanahabari watangaze mema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mama ametenda

mambo makubwa sana tumsemee, tuyaseme watu wajue Mama yuko *site*, Mama halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama ametuletea shilingi bilioni 2.513 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali yetu ya Wilaya, Kata ya Nshambya. Kwa sasa tunaomba pesa kumalizia majengo yaliyobaki, maana hii shilingi bilioni 2.513 zimejenga vyumba 11. Sasa tumeomba pesa nyingine kwa ajili ya kujenga jengo lingine la hospitali kumalizia ambalo ni la ghorofa. Apewe nini Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo mema anayoyafanya katika Jimbo letu la Bukoba Mjini? Tunasema ahsante sana Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ametuletea shilingi bilioni 2.8 shule za msingi na akaleta shilingi bilioni tisa sekondari. Tumejenga sekondari za kutosha, tumejenga shule za msingi za kutosha na sasa tunapoomba kuongezewa maabara na madarasa ni kutokana na uboreshaji wa huduma za elimu ambako wanafunzi wameongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema anakwenda kutujengea Uwanja wa Ndege wa Kyabajwa. Uwanja wa ndege katika Mkoa wetu wa Kagera ni uwanja muhimu na tunauhitaji sana na kwa kuanzia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatutengea shilingi bilioni 1.6. Niiombe Wizara ya Uchukuzi na Hazina watusaidie kupata hizi pesa za upembuzi yakinifu na kulipa *compensation* kwa wananchi wa eneo lile ili ujenzi huu uweze kuanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niyashukuru sana maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi yetu sisi ni moja kuyatafakari, kuyaishi na kutenda vile dhamira yake inataka. Niwaombe wasaidizi wake, Mama ana mambo mengi sana kwa ajili ya Watanzania, kwa mfano katika Jimbo langu la Bukoba Mjini ametutengea shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga kitega uchumi na jengo la machinga ili katika katika Jimbo letu la Bukoba Mjini ili machinga waache kuuza vitu wakitembea barabarani, wawe na sehemu yao na hapa ametenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya

ujenzi wa soko hilo. Hapa anaangalia watu wote wa hali ya chini, ya kati na ya juu. Kazi yetu ni moja kumsemea na kuunga mkono juhudi zake anazozifanya katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga Stendi ya Bukoba Mjini ya zamani sasa inakwenda kumalizika. Ametenga pale hela za kutosha zaidi ya shilingi bilioni 3.8 na sasa tunaomba atutengee pesa iliyobaki ya kumalizia jengo la kitega uchumi katika eneo lile ili wananchi wote wanaoishi maeneo yale waweze kupata maeneo yao ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika njia nne tunayojenga pale Bukoba Mjini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga shilingi bilioni 12, lakini ameongeza shilingi milioni 340 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, kwa ajili ya Barabara kutoka pale Rwamishenye *round about* kwenda Kyakairabwa na kutoka *Rwamishenye round about* kwenda Magoti ambayo jumla ni kilometa 7.5. Niiombe Wizara ya Ujenzi upembuzi yakinifu ukamilike ili tuweze kupata pesa hizi za kuanza ujenzi wa barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nipende kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na njema anayoifanya kwa Taifa letu, lakini niwapongeze sana Mawaziri wanafanya kazi nzuri chini ya Waziri Mkuu na Mungu awabariki sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi atakuwa Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma.

**MHE. JAMILA MAHMOUD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima kuweza kuwepo hapa sasa hivi. Pia, nitoe shukrani zangu za dhati kwa chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa au kuniteua kuwa Mbunge ili kuja kujumuika na Watanzania wenzangu katika kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa shukrani pia, kama sitatoa shukrani zangu za dhati kwako pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mjadala wa hotuba ya Mama, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan; hotuba ambayo aliitoa wakati wa kufungua Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli hotuba ilijaa maono, lakini pia ilikuwa inaonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu. Kama ilivyobainishwa kwenye ile hotuba yenyewe Mama mwenyewe aliweza kusema kwamba tunasonga mbele kujenga uchumi jumuishi unaogusa maisha ya kila Mtanzania. Kauli hii inaendana moja kwa moja na ilani ya uchaguzi inayolenga ustawi wa wananchi. Pia inaelezea dhima ya Taifa na maridhiano ya kitaifa ambayo hutoa huduma bora kwa jamii na uchumi wa uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba aliyoitoa Mheshimiwa haikuwa ya kawaida, ni hotuba ambayo ilijaribu kuunganisha siasa, uchumi, jamii na utu wa Mtanzania. Hivyo, mchango wangu utaangaza zaidi katika mambo tofauti ambayo Mheshimiwa Rais aliazimia wakati anatoa hotuba yake hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ninatokea kwenye Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI, mchango wangu nitaanza kuuelekezea kutokea huko. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais imeweka msisitizo mkubwa katika masuala ya ajira, lakini uboreshaji wa maslahi kwa wafanyakazi, madaktari, wauguzi na wahudumu katika vituo vya afya. Hili limedhihirishwa wazi kupitia ziara ambayo tuliifanya jana Kamati ya Kudumu ya Afya tulienda kutembelea Hospitali ya Dodoma na tuliona mazingira yalivyokuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji walisifia kwamba huduma ambazo wanazitoa zimetokana na sera pamoja na matakwa ya Mheshimiwa kwa sababu wamewezeshwa kwa vifaa vilivyo bora, maslahi yao yameongezeka, lakini pia na wao wameweza kutoa huduma kwa ufanisi kwa kuzingatia haki na bila upendeleo. Watu

wote wanapata huduma na tuliona kwamba wameweza kuokoa maisha ya watu wengi pale hospitali tuliona kuna wodi ya watoto njiti, kuna watoto karibu 40 wako pale. Hii inaonesha kwamba kwa namna gani wameweza kuokoa maisha ya hawa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji pia, walitueleza kwamba wameweza au wanaweza kufanya upasuaji kwa watu 60 kwa siku moja. Hii inaonesha kwamba ni namna gani huduma za afya zimeimarika na zimeongezeka kiasi cha kwamba inatoa fursa kwa kituo kimoja kuweza kuwahudumia watu 60 kwa wakati mmoja, kwa ajili ya kupata *operation* na huduma nyingine ambazo zinatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize kitu kimoja kwamba hatupaswi kupima mafanikio ya afya kwa majengo peke yake bali tunatakiwa tuangalie ubora wa huduma ambao tayari umeonekana kwa baadhi ya taasisi au hospitali ambazo tulizitembelea. Pia muda wa kusubiri wagonjwa, tumeona kwamba kwa sababu hospitali zimekuwa za kutosheleza kubwa na nyingi, kwa hiyo hata muda wa wagonjwa kusubiria umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa, tulijaribu kuongea na wagonjwa wawili, watatu ambao tuliwakuta pale wamesema kwamba wanashukuru kwamba dawa zinapatikana, lakini pia wagonjwa wamekuwa wakiheshimiwa. Yale malalamiko ambayo yaliyokuwepo huko nyuma, wakilalamika kwamba labda wagonjwa wanadharauliwa hawapati huduma vya kutosha, sasa hivi malalamiko hayo yameondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuishauri Serikali na watendaji ambao tunamsaidia mama katika utekelezaji wa ilani hii. Ili tuweze kuendelea katika kuwezesha si kwenye miundombinu tu, lakini tuna haja ya kufanya kazi na jitihada kubwa katika kutoa motisha, lakini kuhamasisha maadili na mazingira bora ya kazi kwa wahudumu wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililoliangazia ni suala la ilani ya chama. Tumeona kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais iliendana sambamba na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Katika utendaji wa Serikali kupitia utekelezaji wa ilani hiyo tunaona kwamba uwezeshaji wa wanawake na vijana kupitia mikopo; kwamba Serikali imeahidi kuendelea kutoa mikopo kwa ajili ya akinamama na vijana. Kama alivyotangulia msemaji mmoja huko nyuma kwamba wanawake sasa hivi wamewezeshwa na wanaweza hii yote inatokana na maono ya mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji mkubwa katika masuala ya reli, bandari, barabara na nishati; tumeona kwamba kwa kipindi cha uongozi wake mama masuala ya usafirishaji kupitia reli, bandari lakini pia anga umeongezeka na watu wengi wamekuwa wakinufaika na miundombinu hiyo. Vilevile, viwanda vya kati na vidogo vimeongezeka. Pia suala zima la elimu ya ufundi na *TEHAMA* ambayo imezungumziwa kwa mapana yake ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninapenda kusema kwamba utekelezaji wa ilani lazima uambatane na masuala ya uwazi, ufuatiliaji na upimaji wa matokeo halisi kwa wananchi. Pia, nichukue fursa hii kuishauri Serikali na Bunge kwa pamoja kuwa mfano wa kufuatilia kila ahadi iliyomo kwenye ilani, kwa sababu kwa namna ya kutoa ripoti kwa wale watendaji tukiwa tuna utaratibu wa kutoa ripoti kila baada ya muda basi tuhakikishe kwamba tunafanya hivyo ili kuweza kuona ule mwendelezo na yale matokeo ya zile ahadi ambazo zilitolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake na vijana kama tunavyojua ni nguvu ya Taifa na tumeambiwa kwamba vijana wako 60% ya Watanzania wote, lakini wanawake ni 52% kama sikosei. Mheshimiwa Rais anaamini na anajivunia kwamba nguvu ya Taifa letu ni nguvu kutoka kwa vijana na wanawake. Hivyo, niombe kwamba tusimwangushe, tumuunge mkono katika hili kwa sababu kama wanawake tutasimama imara lakini na vijana pia kwa pamoja tukashirikiana kusaidia maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa hotuba na ilani wanawake ni lazima washirikishwe katika kupanga na kusimamia *program* za Uchumi, lakini pia, Mifuko ya Uwezeshaji iwafikie wanawake na vijana hasa wanawake wa masokoni, mashambani na viwandani. Pia, vijana wa mijini na vijijini wapate fursa sawa katika hizi fursa za mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali haiwezi kufanya kazi peke yake, tumeona kwamba kuna hizi asasi za kiraia. Na-*declare* kwamba mimi ni Mbunge ambaye ninasimama kwa nafasi za *NGOs* na ushirikishwaji wa Serikali na *NGOs* kama utakuwa mzuri zaidi na tunaamini upo wa kutosha, lakini tunaomba, ushirikishwaji uwe wa karibu zaidi ili kuwafikia jamii za pembezoni. Kama tunavyojua kwamba hizi asasi za kiraia zinafanya kazi zaidi na watu au jamii ambayo ipo chini zaidi. Pia, hizi asasi za kiraia zitumike *in a positive way* katika kutoa elimu ya biashara, masuala ya afya ya jamii na masuala ya mazingira na pia kuwaunganisha wananchi kwa fursa za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianzishe mifumo rasmi ya ushirikiano na *NGOs* katika utekelezaji wa masuala ya afya, uwezeshaji wa wanawake, ajira kwa vijana na ulinzi wa mazingira. Tukiwashirikisha wadau hawa utekelezaji utakuwa wa haraka, haki na gharama nafuu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni bila utekelezaji ni ndoto, hivyo, ninaomba tuwe na ripoti za utekelezaji za robo mwaka kwa kila Wizara; miradi ipimwe kwa muda, gharama na matokeo; ajira zipimwe kwa idadi ya vijana wanaoajiriwa na waliojiajiri wenyewe; na huduma zipoimwe kwa kuridhika kwa wananchi hapo ndipo Bunge litaona nafasi ya kweli litapokuwa na nafasi ya kweli ya kuisimamia Serikali kwa maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. JAMILA MAHMOUD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru wachangiaji wote wa kipindi cha asubuhi kwa michango yao mizuri na ushirikiano waliotupatia.

Jioni tutaanza na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele na wachangiaji wengine wataendelea.

Sasa ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na uchangiaji jioni ya leo. Mchana wakati tunaahirisha niliwataja watakaoanza jioni hii;

tunaanza na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, ajiandae Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo aliitoa katika Bunge hili Tukufu. Kwa sababu, hii ni mara yangu ya kwanza kusimama rasmi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchangia hoja, ninaomba nitumie fursa hii kwanza kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini ambao kwa muda mrefu sana wamekuwa wakiniunga mkono kisiasa na leo ninasimama katika Bunge hili kama mwakilishi wao, ahsanteni sana Wanatunduru. Ahadi yangu kwa Wanatunduru, nitasimama imara, kwa ajili yao, kwa ajili ya kutetea maslahi yao bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kukishukuru Chama changu cha *ACT*-Wazalendo ambacho kimefanya uamuzi wa kuniruhusu mimi na Wabunge wenzangu nane wa *ACT*-Wazalendo, ili tuweze kushiriki katika Bunge hili la Kumi na Tatu. Kwa mazingira ya Uchaguzi wa Mwaka 2020 uamuzi huo haukuwa mwepesi, lakini kama inavyofahamika siasa ni hesabu na uwepo wetu ndani ya Bunge hili ni hesabu za kulitumikia Bunge hili, kama chombo cha mapambano ya kupaza hoja na kuwasilisha sera mbadala. Historia itatuhukumu kama uamuzi huo wa kimkakati ulikuwa ni uamuzi sahihi ama la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi yangu na wenzangu ni kwamba, sisi tutatekeleza wajibu huo ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila hofu wala kusita, lakini pia tutatoa michango yetu kwa hoja badala ya vioja. Hiyo ndiyo ahadi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amezungumzia mambo mengi katika hotuba yake, mimi nitajikita katika maeneo makubwa matatu, la kwanza nitazungumzia juu ya mwelekeo wa kisiasa wa nchi yetu. Tangu tulivyoanza kutoa mawazo yetu ndani ya Bunge hili, Wabunge wengi wamezungumza kwa haki kabisa juu

ya umuhimu wa amani na juu ya umuhimu wa vijana kupenda Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukta moja ambayo imeachwa katika mijadala yetu na mimi ninaisema ni juu ya umuhimu wa haki, ili kupata amani ya kweli. Amani ni zao la haki na demokrasia, bila demokrasia hakuna haki, bila haki hakuna amani, bila amani hakuna maendeleo. Hiyo ndiyo *principle*. Kwa hiyo, ukiwa unazungumza juu ya amani hata kama utakesha kusisitiza watu wapende amani na watu waipende nchi yao, kama husisitizi juu ya haki huwezi kupata amani ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefarijika ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukiacha zile hatua za kutibu majeraha ya uchaguzi wa 2025 amezungumza juu ya ahadi ya Serikali kufufua mchakato wa Katiba mpya. Hilo ni jambo jema kabisa, lakini nakisi ambayo sisi tunaiona, huwezi kuwa na mchakato bora wa Katiba mpya kwa kutaja ahadi ya Katiba mpya peke yake. Sisi tunaona kwamba, Katiba mpya inashughulikiwa kwa vipandevipande; kipande ambacho tumepewa sasa ni kwamba, kutakuwa na Tume ya Usuluhishi ndani ya siku 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yetu sisi ni mchakato huu ushughulikiwe *comprehensively.* Tunataka Serikali ije na ratiba kamili ndani ya Bunge hili ya namna mchakato wa Katiba mpya utakavyoendeshwa. Pia, tunataka Serikali itueleze juu ya *approach* au mtindo ambao itautumia kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujipatia katiba yake na sisi tumekuja na mapendekezo. Hatua ambazo tunazipendekeza ni za muhimu sana katika mchakato huo na ni vizuri mapema sana Serikali inapotoa ahadi itueleze, kama hiyo ndiyo *route* ambayo itaipitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tunahitaji kuzifanyia mapitio Sheria zinazosimamia mchakato wa Katiba mpya, kwa maana ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Mpya pamoja na Sheria ya Kura ya Maoni; hiyo ni hatua ya kwanza muhimu sana. Ya pili ni tunahitaji kuwa na Mkutano wa Kitaifa, kwa maana ya *National*

*Sovereign Conference,* kwa ajili ya kupata muafaka wa pamoja juu ya masuala ya Kikatiba, ambayo mpaka sasa hayajapata muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu ya muhimu ni lazima tuwe na timu ya wataalam, kwa maana ya *Committee of Experts,* ambao wataandaa Rasimu ya Katiba Mpya na hatua ya mwisho ni tunahitaji kuwa na kura ya maoni. Kwa hiyo, tunavyoitamka Katiba mpya tusiishie kuitaja kwa ujumla wake, tuwe na *road map* ambayo itawafanya wadau wote wa Katiba Mpya wajue mchakato utakwenda namna hii. Hilo ni la kwanza ninataka kulisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, jana limezungumzwa kidogo na ninaheshimu taratibu. Ninafahamu kwa mujibu wa Kanuni ya 81, Mwongozo wa Spika ni wa mwisho juu ya suala. Kwa hiyo, sitoliibua tena suala hilo, isipokuwa nina rai kwamba, ahadi ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa ya kuachiwa huru kwa wale ambao walikamatwa katika matukio ya tarehe 29 ni ahadi njema. Vyombo ambavyo vinahusika, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, zifanye uchunguzi wa kina, zijiridhishe kama watu wote wameachiwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapofungua ukurasa mpya wa kisiasa ukiwa na mtu mmoja umemwachia huru, siyo yeye peke yake, unakuwa umeigusa roho yake, familia yake na ukoo wake. Unawatoa kwenye masononeko, unaifanya nchi iwe na furaha na kinyume chake ukiwa na mtu mmoja amewekwa ndani, ametekwa au amepotezwa, siyo yeye peke yake bali ukoo mzima unakuwa kwenye masikitiko na unatengeneza Taifa lenye huzuni. Huo ni mchango wangu wa pili niliotaka kuusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho, ninawakumbusha mabosi wangu, wananchi wa Tunduru, kwanza imesemwa juu ya kuboresha huduma za maji; Tunduru tuna mradi mkubwa sana wa maji. Pale Tunduru Mjini usambazaji wa maji hivi sasa upo kwa wastani wa kilomita 3.3, hivi mtandao wake. Tuna mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 3.4 ambao ungeweza kusaidia mtandao wa usambazaji wa maji Tunduru ufikie kilomita 92,

lakini ule mradi mpaka sasa unasuasua. Tunaitaka Serikali ilitazame hili kwa sababu, tunaamini ni *game changer* katika kuboresha maisha ya Wanatunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalowahusu mabosi wangu, Wanatunduru, ni suala la umeme. Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Chilombe yupo hapa na tunashirikiana vizuri, ataendelea, ni mtaalam wa umeme, lakini niseme hivi kwamba, pale Tunduru tuna mradi mkubwa sana wa umeme ambao ukikamilika utatupa *megawatts* 120 wakati mahitaji yetu ni *megawatts* nne. Maana yake ni Tunduru tutakuwa na umeme mwingi sana wa ziada, tunasubiri kwa hamu mradi huo uweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ukitazama mradi unasuasua kwa sababu, mkandarasi hajapata fedha za kuendelea na mradi. Vifaa viko *site* amekwishapeleka vifaa vingi pale, lakini umeme wa uhakika hujapatikana, ndiyo maana hivi sasa ukienda Tunduru, mimi nina hakika, tutakuta eneo ambalo linaweza kuingia katika kitabu cha historia ya maajabu ya kukatikakatika kwa umeme. Tunduru inaweza ikawa namba moja kwa sababu, umeme unakatika mara 20 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wanatwambia ni kwa sababu, njia ya umeme inapita katika miji mingi. Haya ni maelezo ya kitaalam, mwananchi wa kawaida hayaelewi hayo, yeye anadhani Serikali imelala na imefeli. Kwa hiyo, tunaomba mkandarasi yule apewe fedha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ADO S. ADO:** ...ili mradi uendelee. Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninampongeza anayetoa hoja, lakini ninatokea Tunduru, umeme haukatiki mara 20 kwa siku. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Unaipokea hiyo Taarifa?

Muda wako pia, umeisha.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, muda wangu umeisha watakaotuhukumu kama umeme unakatika mara 20 ama la, siyo Bunge hili ni Wanatunduru, tukutane *site*. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Yustina Rahhi, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge. Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge hili la Kumi na Tatu, mnamo Tarehe 14 Novemba. Kwanza kabisa ninaomba nitoe shukrani kwa Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi pamoja na Kamati Kuu, amekuwa sababu ya kuwepo katika Bunge lako hili Tukufu, Bunge la Kumi na Tatu, kuendelea kuwawakilisha akinamama wa Manyara. Kwa dhati ya moyo wangu ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Watanzania wote kwa ushindi wa kisindindo na wa kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema ni ushindi wa kihistoria kwa sababu, toka tumeingia kwenye vyama vingi 1992 na uchaguzi wa kwanza 1995, hadi leo sijawahi kuona awamu iliyovunja rekodi kwa ushindi mkubwa namna hii na ninaomba Mungu kama rekodi hii itaendelea kuvunjwa katika chaguzi zinazokuja. Hongereni Watanzania na hongera Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawaambiwi tazama. Kulikuwa na sababu kubwa ya ushindi mkubwa kama huu. Watanzania hawawekewi maneno mdomoni, wanajua kazi kubwa kabisa aliyoifanya Mheshimiwa Rais katika kipindi chake alichokuwa madarakani. Kote amewekeza katika sekta za kijamii, kiuchuki, sekta binafsi na vichochea uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa mfano mdogo tu, tukisemea sekta ya kijamii. Ukienda afya kila mtu anaona uwekezaji mkubwa uliowekwa kwenye afya; zimejengwa zahanati nyingi, vituo vya afya vingi, ukiangalia 2020 vituo vya afya vilikuwepo 8,458, lakini mpaka Disemba 2024 vimekuwepo 9,826, lakini hospitali za halmashauri 50. Hospitali na vituo vya *emergence* vimekuwa vimefika 116 pamoja na ununuzi wa dawa, vifaa tiba na mambo kedekede pamoja na kuajiri watumishi wa afya. Hata majirani zetu sasa wanatamani kuja kutibiwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa sababu ya kupunguza vifo vya akinamama wakati wa uzazi. Kulikuwa na vifo 556 kwa vizazi 100,000 kwa mwaka 2020, lakini hadi kufikia Disemba, 2024 vimeshapungua mpaka 104 kwa vizazi 100,000. Hiyo ni kazi kubwa sana iliyofanyika na Dkt. Samia, lakini vifo vya watoto kutoka 67 kwa watoto 1,000 mpaka 43 ni kazi kubwa sana imefanyika. Hongera Dkt. Samia na hongereni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye sekta ya elimu hiki kitu kinachoitwa elimu bure watu wasione ni jambo dogo. Kumekuwa na Watanzania ambao wanashindwa kuendelea na elimu ya sekondari. Ninafahamu kuna wazazi wamekuwa wanaona ni adha kubwa sana. Mimi ni shahidi, wanafunzi wanavyofika darasa la saba, kuna wazazi wanawaambia wakaandike madudu ili wasifaulu na Serikali ikawasumbua wale wazazi kuwashinikiza walipe ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imeleta unafuu mkubwa, wanafunzi wanasoma na kwa kuona hivyo, ndiyo maana Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongeza fedha kwenye eneo hilo toka shilingi

bilioni 312 katika mwaka wa 2020 hadi shilingi bilioni 796 kufikia mwaka jana, 2024. Hiyo ni kazi kubwa sana, lakini kumekuwa na ongezeko la shule za msingi, shule za sekondari, madarasa na matundu ya choo kila sekta. Ninampongeza sana kwa kazi kubwa iliyofanyika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maono yake sasa ya kubadilisha mtaala wa elimu na kuleta hizi shule za amali. Huu unaweza ukawa muarobaini kwa vijana kupata *skills,* wanavyomaliza elimu warudi kule kuweza kujiajiri na kufanya kazi. Ninaomba Serikali katika eneo hili waweke miundombinu ili wanafunzi wanaokwenda huko wasiende kupotea. Pamoja na walimu na ma-*facilitator* ambao wakimpika mtoto kwenye amali atoke hapo ana *skills* na *knowledge* ya kuweza kujikwamua na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya umeme; kwanza ninaipongeza sana Tanzania, kwa sehemu kubwa kwa mapato ya ndani tumeweza kujenga mradi mkubwa sana wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambapo tunatarajia kupata *megawatts* 2,115 na umefika 99% ni kazi kubwa sana iliyofanyika ndani ya Serikali hii. Hii itaongeza upatikanaji wa umeme kwenye vyanzo vingine, ili zile ndoto za Samia Suluhu Hassan za kusema tufikie uzalishaji wa *megawatts* 8,000 zifikiwe kwa sababu, mahitaji ya Watanzania mpaka sasa hivi ni chini ya *megawatts* 2,000. Kwa hiyo, kumbe siku moja tutakuwa na ziada ya umeme, tutauza nje na hiki kitakuwa chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kupeleka umeme vijijini na kwenye vitongoji; kwanza ninapongeza kwa sababu, vijijini tayari tumefikia 99%, lakini huko kwenye vitongoji bado tuko kwenye 51% kutoka vitongoji 64,359, ambavyo vimekwishapata umeme ni vitongoji 32,827 ni hiyo 51%. Kupeleka umeme kwenye vitongoji hakika kumepunguza kazi kubwa kwa akinamama *(women workload),* wamekuwa wanahangaika na nafaka kwenda kusaga mjini, kutuma bodaboda, mara waende na punda. Sasa hivi mashine za kusaga zipo kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa sababu kubwa ya kupunguza kitu kinaitwa *rural urban immigration* kwa vijana. Vijana walikuwa wakimaliza la saba na vyuo vikuu ni lazima wakimbie kijijini waende mjini na ndiyo *Gen Z* wanaoongezeka. *Gen Z* ni wasomi, akikaa kule kijijini hana cha kufanya, umeme hakuna, hawezi kupata *exposure* ndiyo anakimbia huko, lakini imesaidia sana pia, vijana kujiajiri; wana ma-*salon* na ma-*grill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu sikivu, hivi vitongoji vilivyobaki waweze kuvi-*cover* kwa muda mfupi wapate umeme lakini pia wafungiwe kwa bei ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuona tabasamu kwenye nyuso za Watanzania lazima tuje tuwekeze kwenye sekta za kiuchumi ambazo Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, hizi zikiwa ni kilimo, mifugo na madini, kote huko ili hizi huduma za jamii ambazo zimekwishawekwa kama elimu, afya na maji Watanzania wawe na uwezo mkubwa wa kuvimudu ili Watanzania tusijigawe, tusiwe katika *cluster* kulingana na *wealth*. Kwa sababu sasa hivi kuna mtu anapata huduma ya afya kwa gharama kubwa, mwingine kwa gharama ndogo, wengine elimu wanachagua, siku moja Watanzania waweze kumudu hii huduma wakiwa tayari wana hali nzuri ya kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kilimo, kuna fursa nyingi sana huku kwenye kilimo, ni sehemu nzuri sana ya uwekezaji na ndiyo maana Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia kwenye kiti ameipaisha bajeti ya kilimo mara nne. Bajeti ilikuwa shilingi bilioni 294 hadi sasa hivi tunatekeleza bajeti ya shilingi trilioni 1.2 ni kazi kubwa sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *potentials* nyingi. Huku Tanzania siyo sehemu ya kusema tunakosa mashamba ya kulima. Kuna hekari zaidi ya milioni 44 zinazofaa kwa kilimo na tumeweza kutumia chini ya 40%. Kuna maeneo yanafaa kwa umwagiliaji, hekari milioni 29, zilizoendelezwa ni milioni moja, hizi zote ni fursa za uwekezaji katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bado kuna fursa ya kuzalisha pembejeo hususan mbegu. Zaidi ya nusu ya mbegu zinazotumika hasa za mahindi tunaziagiza kutoka nje, kwa hiyo, hapa kuna fursa kubwa, tunayo mashamba, tunazo *potentials* na *conducive climate* ya kuweza kuzalisha mbegu. Kwa mfano, kuna mashamba ya *ASA*, haya yanaweza wakapewa hata vijana wakatuzalishia mbegu na tukauza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa nyingine iliyoko kwenye kilimo *of course* tunajitosheleza kwa chakula, lakini kuna vyakula bado tunaingiza kwa fedha za kigeni, kwa mfano ngano. Watanzania tunatumia zaidi ya tani milioni moja ya ngano, lakini 90% ya hii ngano inatoka nje na tunanunua kwa fedha za kigeni. Sisi tunaweza kuzalisha kati ya tani 100,000 na tani 200,000. Tunayo mashamba Basutu, Ngano *Limited*, Serikali ione ni namna gani hii ni fursa tuwekeze tujitosheleze kwa uzalisaji wa ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mafuta mahitaji ya Watanzania ni tani 650,000 tunaweza kuzalisha tani 300,000, hizi ni fursa. Tunayo mazingira *very conducive* kuzalisha alizeti, michikichi na ufuta, tuwekeze maeneo hayo. Tunayo *sugar gap*, mahitaji yetu ya sukari ni zaidi ya tani 470,000 na sisi tunazaisha kwenye tani 360,000, haya ni maeneo kwenye kilimo yanafaa kuwekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la mifugo kuna maeneo mengi sana ambayo tuna fursa ya uwekezaji. Kwa sababu tukisema sisi ni wa pili Afrika kuwa na mifugo mingi lakini bado hatujaweza kui-*exploit* kutoka kwenye mifugo tukapata kipato.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, wajiandae Mheshimiwa Edibily Kazala na Mheshimiwa Paschal Inyasi.

Mheshimiwa Edibily Kazala.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa hii ya uhai. Pia, kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Rais kama Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kwa kuniteua ili niingie kwenye kinyang'anyiro cha Ubunge na hatimaye wananchi wa Kasulu Vijijini wakaamua mimi niwe Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kipindi chake cha miaka minne ambacho kimekuwa ni cha neema kwa Taifa letu la Tanzania. Kipindi ambacho tumeshuhudia safari ya kipekee, safari ambayo inafanana na ile safari ya wana wa Israel wanatoka Misri wanaelekea Kanaani. Sasa, Mheshimiwa Rais, ametukuta tuko jangwani hatimaye tunayo matumaini punde si punde tutafika Kanaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa hotuba nzuri, hotuba iliyojaa matumaini, hotuba ambayo ni dawa na hotuba ambayo imejaa dhamira ya dhati kama kiongozi, maana kama kiongozi wajibu wake wa kwanza anawaongoza wananchi wake, lakini pia atawasaidia wananchi kwa kupunguza changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kipindi chake cha miaka minne ameonyesha mwelekeo wa kiuongozi wa Taifa ambao nimetangulia kusema tunaelekea Kanaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kiongozi pia ametatua changamoto zetu zinazotukabili kama Watanzania ambazo zingine

zilikuwepo na zingine zimeibuka wakati tupo kwenye safari. Changamoto hizo Mheshimiwa Rais amepambana nazo kuhakikisha safari yetu inakuwa ni rahisi na nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kipindi chake cha miaka minne ametatua changamoto mbalimbali. Ukizungumzia nishati, umeme mpaka vijijini. Ukizungumzia afya, zahanati na vituo vya afya mpaka vijijini. Ukizungumzia elimu, shule zimejengwa, zikiwepo shule za kimkakati za wasichana. Pia, ukizungumzia kwa maana ya uchukuzi na ujenzi, barabara zimejengwa, pia kuna meli mpya zimejengwa. Kuna ndege mpya zimenunuliwa. Ukija kwenye kilimo utamkuta tena Mheshimiwa Rais pembejeo, wananchi wetu wanafurahia ni shangwe vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utazungumzia pia msukumo wa Serikali kuwekeza fedha nyingi kwenye kilimo ikiwemo kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. Katika haya hivi ndivyo vilikuwa vikwazo vikubwa ambavyo ukiangalia vingetukwamisha sisi kwenye safari yetu kama Taifa kufika Kanaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze pia kidogo kwenye baadhi ya vipaumbele vya Mheshimiwa Rais, lakini pia nishauri. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amezungumzia sekta ya uzalishaji. Kwenye hotuba yake amegusa kilimo, pia amezungumzia na viwanda. Ninamuunga mkono kwenye hili pia ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuziona sekta hizi mahsusi za uzalishaji kitaifa. Taifa letu na nchi yetu tunalo eneo kubwa la ardhi ambalo linakidhi kilimo, ufugaji, pia tuna maeneo ya kutosha ya kujenga viwanda vya kimkakati ambavyo vinaweza vikatutoa kama Taifa kutoka hatua moja kwenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisisitize kwenye kilimo. Ningeshauri kama Taifa tuwe na vitu vichache vya kimkakati. Kwa mfano, tunaweza tukasema tunapambana na kilimo na viwanda kama Taifa, tuhakikishe tunasukuma sekta hizi mbili kufika mahali kama Taifa katika kipindi cha miaka mitano kama Mheshimiwa Rais alivyoeleza kwenye hotuba yake. Kwenye kilimo tunaweza

tukaweka msukumo kwenye mazao ya kimkakati, tunaweza tukachagua mazao kadhaa ya biashara kwa mfano chai, pamba mkonge, lakini pia na tumbaku. Mazao haya yanaweza yakatupatia fedha nyingi ya kigeni kama Taifa, lakini pia itatusaidia kuongeza pato la mwananchi mmoja mmoja kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kwenye kilimo. Kuna changamoto nyingine kwenye *issue* ya masoko. Ninaomba niishauri Serikali ikiwezekana tujitahidi kuongeza nguvu kwenye matumizi ya TEHAMA ili kurahisha wananchi wetu ku-*access* masoko hata wakiwa vijijini. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo inaweza ikawa na *software application* ambayo uki-*click* kwa mfano mahindi au uki-*click* mchele, utaona mchele Dodoma unauzwa kiasi gani, kama ni maharage utaona Dar es Salaam yanauzwa kaisi gani, utaona kama ni Kongwa au wapi maeneo mengine ili mwananchi atofautishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye Jimbo langu mimi ilifika sehemu maharage yanauzwa mpaka shilingi 1,000, lakini wakati huo huo ukija Dar es Salaam ni shilingi 3,500 na ukija Dodoma shilingi 3,000. Kwa hiyo, mwananchi aki-*click* mambo yanakwenda vizuri anaweza akajua kitu gani cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza ninaomba nishauri pia kwenye suala la ajira na upotevu wa mapato. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, ajiandae Mheshimiwa Thomas Kampala, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na mimi binafsi ninashukuru kwa mara ya kwanza kusimama katika Bunge hili kutoa hoja. Pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, watu wa Dodoma tumepata mvua nzuri

tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. Ninamshukuru vile vile Mheshimiwa Rais kwa kunikubali mimi kugombea katika Jimbo la Dodoma Mjini, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia wakazi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi mimi pamoja na Mheshimiwa Rais na Madiwani. Wamekiheshimisha sana Chama Cha Mapinduzi na mimi binafsi ninaahidi kutumia nguvu zangu zote kuhakikisha kwamba matarajio yao yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya mambo mengi katika Jimbo la Dodoma Mjini, lakini kwa haraka haraka tu niseme, tumejengewa *SGR*, sasa hivi watu wa Dodoma tunapata usafiri kwa urahisi zaidi kwenda Morogoro na Dar es Salaam, hospitali pamoja na vituo vya afya kadhaa vimejengwa, miradi ya maji na umeme, barabara hii ya mzunguko pia tumejengewa kiwanda kikubwa cha mbolea katika eneo la Nala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni baadhi, yapo mengi kwa sababu ya muda nitajikita katika maeneo matatu na niseme tu ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri iliyosheheni matumaini makubwa wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo na mimi ningependa nijadili ni suala la uchukuzi ambalo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ameliweka suala hili vizuri katika ukurasa wa 32 na ninaomba nisome kwa jinsi lilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameeleza kuhusiana na kufungamanisha sekta za uchukuzi, sekta hizi zinapofungamanishwa zinaleta tija kubwa sana kwa uchumi wa nchi. Ninaomba niseme tu, katika Jimbo la Dodoma Mjini tumepata bahati ya kupitiwa na barabara ya mzunguko *(ring road),* katika eneo la Zuzu barabara hii inakutana na *SGR*, reli ya mwendokasi. Hata hivyo, katika kituo hiki hakuna kituo cha *SGR* ni ombi la wakazi wa Dodoma Mjini kwamba eneo hili la Zuzu lipate stesheni ya *SGR* kwa kuwa tayari kuna *access road* ambayo ni *ring road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo kadhaa ambavyo *SGR* inapita kwenda Dar es Salaam, maeneo ya Soga na Gulwe, Serikali ya Dkt. Samia inajitahidi sana kujenga *access roads* lakini hapa Zuzu tayari ipo *access road* ambayo inakwenda katika maeneo mbalimbali, hii barabara inashika maeneo ya Nala, Mbalawala, Bihawana, Matumbulu mpaka Mpunguzi, kote huko inafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani kabisa na hiki kituo ambacho tunapenda kijengwe cha Zuzu kuna kongani ya viwanda inatarajiwa kujengwa katika eneo la Zuzu, ambapo ni maombi ya wananchi kwamba litoke tawi la reli ya *SGR* kutoka hapa Zuzu kuelekea Nala ili mizigo itakayokuwa inakwenda kwa ajili ya ujenzi wa viwanda hivi ipite kwenye reli badala ya kupita kwenye barabara zetu ambazo zinajengwa kwa gharama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ambao ningependa nichangie ni sekta ya ujenzi ambayo katika ukurasa wa 28 imewekwa vizuri na ninaomba ninukuu. Mheshimiwa Rais amesema hivi; "eneo lingine tutakalolipa uzito mkubwa ni sekta ya ujenzi. Kipaumbele kitakuwa ni kukamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ambazo tayari zimeanza na zinaendelea. Tutaendelea na kasi ya utekelezaji wa miradi ya barabara pia *TANROADS* ili kufikia lengo la kuunganisha barabara za Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kujenga barabara za nchi hii, ningependa nitoe wito kwa vijana wetu katika nchi hii na niseme tu kwamba nchi hii imetoka mbali sana katika sekta ya barabara. Miaka ya kabla ya 2000 wakazi wa Dar es Salaam na maeneo mengine kama Morogoro na Dodoma walikuwa wanakwenda katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa kutumia treni peke yake. Hakukuwa na usafiri mwingine zaidi ya treni, ilikuwa inachukua hata siku tatu na hiyo ni katika hali ya kawaida, lakini ikitokea reli imekwama katika maeneo ya Kidete kwa mfano, ambapo kila mara huwa kuna shida wakati wa mvua, basi abiria walikuwa wanaweza kukaa njiani hata kwa wiki nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mbali katika ujenzi wa barabara ambapo kwa sasa Mheshimiwa Rais amefanikiwa kujenga kilomita 11,900 hadi 12,197 za barabara nchi nzima. Tuko mbali katika barabara na suala hili Watanzania tunapaswa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake hizo. Nitatoa mfano mdogo wa hii Barabara ya *Ring Road*, barabara hii ni barabara ambayo ni ya mfano. Nilikuwa najaribu kupitia nchi mbalimbali kuona ni nchi zipi ambazo zina barabara zenye urefu kama huu, tunaambiwa kwamba barabara hii ya *ring road* ambayo ina kilomita 112 .3 ni barabara kubwa kuliko zote katika Nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeenda mbali zaidi nikaangalia Morocco pamoja na South Africa, lakini nimekuta wote wana barabara za *ring road* ambazo zina urefu mdogo. South Africa wana kilomita 83, Morocco wana kilomita 41 ni Misri peke yake ina kilometa 400 ambayo ndiyo inatuzidi, sisi ni wa pili tunayo barabara ambayo kwa kweli ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta wote wana barabara za *ring road* ambazo zina urefu mdogo. *South Africa* wana kilometa 83, Morocco wana kilometa 41; lakini ni Misri peke yake ina kilometa 400, ndiyo inayotuzidi. Sisi ndiyo wa pili na tuna barabara ambayo kwa kweli ni kubwa. Barabara hii ya *ring road* inasaidia sana ufikaji katika Jiji la Dodoma. Ninasema tu, ndugu zangu wanaotoka Iringa na wanakwenda labda mji wa Serikali, hawana haja tena ya kwenda mjini, wanafika Matumbulu wanaingia moja kwa moja Mji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu pia wanaotoka Mwanza, Shinyanga na kadhalika, wakifika maeneo ya Nala hawana haja tena ya kuja mjini, wanaingia kushoto, wanapita Veyula wanakwenda Mji wa Serikali wanakuwa wameshamaliza. Kwa hiyo barabara hii ni msaada mkubwa sana kwa sisi Watanzania hasa ndugu zangu tunapoingia katika Mkoa wa Dodoma, kwa hiyo barabara hii ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** …barabara katika mkoa wetu, tuna Barabara kutoka Mjini Dodoma kuelekea Mvumi. Barabara hii ni ya muhimu na wananchi wetu ambao wanapitiwa na hii barabara hawajalipwa fidia. Ninapendekeza walipwe fidia zao kwa sababu ni haki yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na sasa namwita Mheshimiwa Thomas Kampala, ajiandae Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mungu wa Mbinguni kwa kunipa kibali cha kusimama siku ya leo ili nichangie kwenye hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa msingi mkubwa inatupa mwelekeo wa tulipotoka na wapi tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; lakini kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, ninaomba kuwapongeza sana na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Katavi kwa kura nyingi za kishindo walizonipa ambazo zimeniwezesha mimi leo kuwa mbele yako hapa kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anakuja kwenye Jimbo la Katavi tulimwambia Mheshimiwa Rais kakae kwa kutulia sisi Jimbo la Katavi tutakupigia kura kama tumechanganyikiwa, tulikuwa tunazo sababu. Katika kipindi cha miaka minne tangu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameingia kwenye nafasi 2021 – 2025, Jimbo la Katavi tulipokea fedha shilingi bilioni 27.665 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia, katika nafasi yake ya urais, Jimbo la Katavi fedha hizi nyingi tuliziwekeza kwenye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu, wakati Mheshimiwa Rais anaingia, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele tulikuwa na shule za msingi 13. Katika kipindi cha miaka minne tumetoka shule 13 hadi 29. Tunaposimama hapa tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hatuji kufanya mbwembwe, tunapongeza yale ambayo mama huyu amyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda upande wa elimu hapohapo, elimu ya sekondari amekuta shule za sekondari tano. Hadi mwaka 2021 – 2025, tumetoka kwenye shule za sekondari tano mpaka 11 katika kipindi cha miaka minne. Hizi tano ninazoziongea ni tangu uhuru, hizi sita ni katika kipindi cha miaka minne; kwa nini tusimpongeze mama huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya, wakati mama huyu anaingia 2021 – 2025 tulikuwa na vituo vinavyotoa huduma za afya tisa; leo katika kipindi cha miaka minne vituo vya afya vinavyotoa huduma za afya viko 17. Kwa ongezeko la zahanati sita, kituo cha afya kimoja, hospitali ya wilaya moja, magari ya kubebea wagongwa manne ndani ya miaka minne. Kila anayefanya kazi anastahili kupongezwa. Tunaposimama kumpongeza mama huyu, hatusimami kumsifia, tunampa moyo kwa kazi alizofanya ili aendelee kufanya zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo, kulikuwa kuna changamoto nyingi sana. Hivi leo tunavyoongea wakulima wa Jimbo la Katavi wanapata mbolea ya ruzuku. Nikija kwenye kitabu

hiki cha Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ninaomba ninukuu; ukijikita kwenye sekta ya uzalishaji ukurasa wa 20, Mheshimiwa Rais; hapa ninataka kuweka msisitizo; Mheshimiwa Rais amesema:

"Katika miaka mitano ijayo tunakwenda kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta za uzalishaji tukianza na kilimo. Tutaongozwa na dhana ya kilimo ni biashara ni mwekezaji. Lengo letu ni kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hii kutoka asilimia nne ya sasa hadi kufikia 10% ifikapo 2030. Kwa kufanya hivyo tunalenga si tu kujihakikishia utoshelevu wa chakula bali pia tunawekeza kwenye mnyororo wa thamani ili kuwanufaisha Watanzania wengi walioajiriwa kwenye sekta hii. Tunakusudia kufanya Watanzania wengi kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya mahindi, mchele na mbogamboga *(horticulture)* Barani Afrika. Tutafanya hivyo kwa kujielekeza kwenye kilimo cha kisasa kwa kuongeza pembejeo kama mbegu bora, mbolea, viatilifu kwa ruzuku. Tutaongeza upatikanaji wa maji kuhakikisha kuongezeka eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka ekari milioni 3.4 hadi milioni tano".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka kusisitiza; kwenye upande wa kilimo cha umwagiliaji, sisi Jimbo la Katavi tuna maeneo mengi yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji si tu kinakwenda kutuongezea mazao ya chakula na ya biashara, kinakwenda kutoa suluhu ya ajira kwa vijana na kuwazuia vijana wanaotoka vijijini kukimbilia mijini. Serikali ikifanya *proper investment* kwenye *irrigation scheme* vijana watavutika kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji na badala yake hawatatoka vijijini kuja mjini. Tunaiomba sana Serikali kufanyia mkazo maneno haya ya Mheshimiwa Rais. Maneno haya yakifanyiwa kazi vizuri, hata wimbi la vijana kwende mjini hawatakuja kuwaona tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea mafanikio ya eneo lolote lile na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wapo viongozi kwenye maeneo yetu wanafanya kazi vizuri sana. Kwenye eneo langu la Jimbo la Katavi kwa mahsusi ninaomba kuchukua fursa hii kuwapongeza viongozi wafuatao, Alhaj DC Majid Mwangala na Mkurugenzi dada yangu Singlida Mndema.

Ninawapongeza hawa makusudi. Haya yote tunayoyaona yamefanyika kwenye eneo letu, wamesimamia vizuri fedha zilizokuja kwenye Jimbo la Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari bado ni ndefu; mama huyu anayo dhamira ya dhati ya kuwatumika Watanzania. Tusimame tumsemee, hakuna kiongozi anaweza kusimama akasema mwenyewe, twende tukamsaidie mama huyu kusema yale yaliyofanyika. Ninataka niwaambie, katika kipindi cha hii miaka mitano tunayoianza na kwa hotuba hii tunakwenda kuona matokeo makubwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninataka pia kuwashukuru sana viongozi wenzangu na ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kumtia moyo. Mama aendelee kufanya kazi, sisi viongozi na Waheshimiwa Wabunge tuko nyuma yake na tutamlinda kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kamonga, wajiandae Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Isack Joseph na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa mwezi Novemba wakati anazindua Bunge. Ninashukuru sana kwa kupata hii nafasi na ninaanza kwa kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Ludewa kwa kunipa heshima kubwa na kunichagua kwa kipindi cha pili ili niweze kurejea Bungeni ili niendelee kuwatumikia. Kwa kitendo hicho ninawaahidi wananchi wa Ludewa kwamba nitaendelea kuwa sauti yao, nitawasemea na nitaendelea kuwa karibu nao wakati wote. Mwenyezi Mungu tu anijalie uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Ludewa si wepesi sana kumwamini Mbunge kumpa vipindi viwili. Mara ya mwisho mwaka 1995 Mbunge aliyetoka ndiye aliyekuwa amekaa awamu tatu. Tangu wakati huo, miaka 30, hakuna Mbunge amepata awamu mbili. Kwa hiyo lazima niwashukuru sana wananchi wa Ludewa kwa heshima kubwa na ya kipekee waliyonipa mimi kuwatumikia. Ninawafahamu watu wa Ludewa, kwamba wao wanapenda matendo matamu, hawapendi maneno matamu. Niwaahidi kwamba watashuhudia vitendo ili waendelee kuniamini na kunipa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma Hotuba ya Mheshimiwa Rais kurasa zote 44. Nimepitia kipengele kwa kipengele, nimeona ameonesha sasa kwa kipindi hiki cha miaka mitano ni mambo yapi anakwenda kuyapa kipaumbele katika kuwatumikia Watanzania. Kwa hiyo na sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tunampa ahadi kwamba tutampa ushirikiano. kwa yale ambayo yako kwenye nafasi yetu tutatoa ushirikiano wote ili yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeon, ukisoma ukurasa wa 11, amezungumzia, alitoa ahadi ya ajira kwa vijana, alitoa ahadi ya ajira 7,000 kwenye sekta ya elimu na ajira 5,000 kwenye sekta ya afya. Kwa hiyo ninashukuru sisi Ludewa tumepokea watumishi 108, tunasubiri wa idara ya elimu msingi. Elimu sekondari tumepokea watumishi 45, afya 47 na wengine wanaendelea kuripoti. Kwa hiyo ninamshukuru sana kwa kutekeleza ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vilevile ukurasa wa 13, Mheshimiwa Rais amezungumzia jambo la vijana. Amezungumzia na ametoa takwimu kwamba 60% ya Watanzania ni vijana. Tumpongeze sana kwa kuunda Wizara Maalum ya kushughulikia masuala ya vijana na kumteua Waziri kijana ambaye ameanza vizuri, ameanza na mguu mzuri. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia kundi la vijana lina changamoto nyingi. Hawa ndiyo wana changamoto ya

kukosa mitaji kwa ajili ya kuendeshea biashara na shughuli mbalimbali; ndilo kundi ambalo hatimiliki zile fursa za vyanzo vya uchumi, ni kundi la vijana. Pia ndiyo walio kwenye changamoto ya madawa ya kulevya na msongo wa mawazo. Vijana wanakabiliwa na matatizo mengi na wengine wanakuwa na ujuzi ambao wakati mwingine si hitaji kwenye soko. Kwa hiyo natoa wito kwa Serikali hasa Wizara ya Elimu, Serikali imefanya *reforms* nyingi sana kwenye elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye elimu ya juu twende sasa tukaangalie kule tuweze kufanya *reforms*, tupitie kozi zote zinazotolewa na vyuo vikuu, tuangalie mahitaji ya soko yanakwenda vipi. Wizara ya Elimu ianzishe kitengo maalum cha *Information Center* ili wale vijana ambao wanakusudia kwenda kusoma elimu za juu wawe na ufahamu ni nini kinachohitajika kwenye soko. Hii itakuwa muhimu katika kusaidia vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile na kule kwenye soko la ajira kuwe na *fairness*. Wale ambao wanafaulu usaili waweze kupewa nafasi kulingana na uwezo wao ili hata kusiwe na watu wanapiga simu bwana Mheshimiwa Mbunge nimefanya usaili nisaidie *connection*. Kwa hiyo *connection* tuzipunguze ili haki iweze kutendekea kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nimeona amelizungumzia ni eneo la Dira ya Taifa. Amezungumzia na ameonesha pale umuhimu wa miradi ile mikubwa ya kimkakati ambayo inaweza kupaisha uchumi huu. Vilevile dira hii ameonesha wazi kwamba utekelezaji wake unahitaji rasilimali fedha nyingi. Kwa hiyo nitoe wito kwa wasaidizi wake wote upande wa Serikalini waweze kubuni vyanzo vingi vipya vya mapato ili tuweze kuongeza bajeti za *TARURA* na bajeti za *TANROADS* kwa sababu kule vijijini Watanzania wengi, zaidi ya 70% ni wakulima. Wana mazao yao, wawe na urahisi wa kutoa kule kwenye shamba maeneo ya uzalishaji kuyapeleka kwenye soko. Kutakuwa na faida kubwa na wengi wataingia kwenye sekta hiyo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hata kule jimboni Ludewa tukaanza na zile barabara ambazo zinaunganisha tarafa. Kwa mfano Madope pale kwenda Madilu mpaka ukaingia kule Mundindi, ile barabara ni muhimu sana. wenzetu wa *TARURA* waje na mbinu mpya na teknolojia mpya ya kuboresha hizi barabara ili ziweze kuhimili magari yenye uzito wote. Barabara ile ni barabara yenye uchumi mkubwa, magari yanapita hadi tani 30. Kwa hiyo ni muhimu sana tukaangalia eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija vilevile kuangalia Mheshimiwa Rais amezungumzia masuala ya viwanda, ukurasa wa 23, kuongeza uzalishaji kwenye viwanda. Sisi kule Ludewa kuna mwekezaji anaitwa HWTZ, anakusudia kujenga kiwanda cha kuchenjua chuma kutenganisha chuma na *titanium,* lakini vilevile kujenga kiwanda cha kuzalisha bidhaa zinazotokana na chuma ambazo zimekamilika. Kwa hiyo ni viwanda vikubwa vina ajira zaidi ya 1,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu anakabiliwa na changamoto kubwa sana, kwanza barabara upande ule wa Itoni Lusitu Serikali imeanza na iliweka mkandarasi. Tunaomba sasa pale paweze kukamilishwa ili mwekezaji huyu aweze kupitisha vifaa vyake na kuanza kwenda kujenga viwanda vyake. Pia akikamilisha viwanda aweze vilevile kusafirisha bidhaa. Ni mwekezaji mkubwa sana ambaye ameshatwaa eneo la ekari zaidi ya 711, ameshalipa fidia zaidi ya shilingi bilioni 2.5. Uwekezaji wake una thamani ya shilingi 3,000,000,000,000, dola bilioni 1.5, kwa hiyo ni uwekezaji mkubwa, atajenga bandari Ziwa Nyasa ili aweze kwenda kuchukua malighafi za viwanda vyake Malawi na Msumbiji pamoja na kupeleka bidha kwenye nchi hizo. Huko tayari alishapewa maeneo, ameshaanza utekelezaji. Kwa hiyo, ninaomba upande wa Serikali mwekezaji huyu aweze kupewa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii ya umeme hasa kwenye kituo cha kupoozea umeme, kwa sababu kwa sasa kipo Madaba na hii inasababisha kukatika sana kwa umeme hata wananchi wanapata kero kubwa sana; ile *transmission line* kutoka Madaba kuja Ludewa ina uwezo wa kusafirisha *megawatts* na ilihali

viwanda vinahitaji *megawatts* 30. Kwa hiyo ninaomba sana hii ya Barabara Itoni – Lusitu ikamilike na Kituo cha Kupoozea Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapongeza sana Hotuba na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa; na sasa ninamwita Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kwanza ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwingi wa utukufu. Katika kipindi changu hiki cha awamu ya tatu ya Ubunge ninasimama hapa leo kwa mara ya kwanza. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini vilevile ninawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa kunipa fursa hii. Ninataka kuwaahidi mbele ya Kiti chako kwamba yajayo yanafurahisha zaidi na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hotuba nzuri ya mfano. Sambamba na yeye Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi Makamu wa Rais, pamoja na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninawapongeza sana kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ile ukiisoma kwa kweli inaleta raha kwa sababu imesheheni Wizara zote na kila mahali ambapo unasoma na kulinganisha hali halisi ya utekelezaji uliofanyika kwa kweli unasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais ambaye ni tunu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama Rais mwanamke kwa kweli ametuvisha nguo sisi wanawake wa Tanzania. Ametuheshimisha kwa sababu alipokuwa anapokea kijiti hiki wengi walipata mashaka Rais mwanamke

ataweza? Ni kwa sababu ya desturi tuliokuwa nayo toka awali kwamba marais wote waliopita ni marais wanaume. Sasa leo hii tunaye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametuvusha na anaendelea kuikimbiza nchi katika sekta mbalimbali kufuatia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia katika hotuba yake maeneo mbalimbali ambayo ameyazungumza na kuendelea kutoa maelekezo mbele zaidi kwamba, tunatarajia kwenda mbele zaidi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya barabara, hakika unamwona Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuunganisha wilaya na wilaya, katika kuunganisha mikoa na mikoa katika miundombinu ya barabara na katika kuunganisha nchi yetu na nchi jirani. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona vilevile katika nchi yetu miradi mingi imeendelea kutekelezwa. Hata sasa tunapozungumza wakandarasi wako kazini wameshapewa pesa na kazi zinaendelea kila mahali; hongera nyingi sana kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu ya barabara vilevile ninataka nizungumzie katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2025-2030, tayari katika Mkoa wa Ruvuma imeshajieleza katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba, Barabara ya Likuyufusi - Mkenda yenye urefu wa kilometa 124 inakwenda kuanza kujengwa kwa lami msimu huu. Katika urefu huo, tayari pesa imeshapelekwa ya ujenzi wa lami kwa kilometa 60; nani kama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la barabara ninaona kabisa, ninamwona Samia katika Barabara yenye urefu wa kilometa 305 inayotoka Mtwara - Pachani inapita Luchili inakwenda Lingusenguse inapita Lusewa hadi kule Narasi na hatimaye kufika Tunduru. Hii ni barabara ya kimkakati ambayo ni barabara itakayobeba zaidi ya vijiji 37 - 70 ambayo kimsingi wananchi wanaozunguka barabara hiyo ni wananchi wanaojishughulisha na masuala ya kilimo, lakini ni wananchi ambao wanajishughulisha zaidi na masuala ya uzalishaji. Kwa hiyo, ninaiona nchi ya Tanzania

ikifunguka katika nyanda za juu kusini kwa kasi kubwa sana. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie suala la maji. Ndugu zangu ukisoma katika kitabu hiki cha hotuba yake kuna maeneo unakwenda kukuta kwamba nchi yetu ya Tanzania katika sekta ya maji imekua kutoka 84.1% mpaka 96.1% kwa maeneo ya mijini. Vilevile, unatazama katika eneo la vijijini unakuta imekuwa katika eneo hilo kutoka 70% mpaka 86%. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu tuna kila sababu ya kuwa na wivu na Rais wetu. Rais wetu anafanya mambo makubwa. Kwa sisi ambao tumetembea nchi mbalimbali tunataka tuseme walioko nje na wengine ambao wako humu ndani wanaweza wasijue kwamba, kwa nini tunasema Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumekwenda kwenye nchi mbalimbali unaangalia unakuta mpaka unajiuliza hii nchi toka imepata uhuru mpaka hapo ilipofikia hivi itapambazuka lini? Hali ni mbaya. Ukiangalia kwenye miundombinu ya barabara, miundombinu ya usafirishaji wa anga unakuta hali ni mbaya, lakini sisi tunacho chanda chema mkononi lakini hatukioni, hatukioni ndugu zangu. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya vitu vikubwa na anastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika sekta ya afya vilevile tunaangalia kila mmoja hapa kwenye maeneo yake aliyotoka kuna zahanati, kuna vituo vya afya, kuna hospitali za wilaya, kuna hospitali za kanda; jamani tumpe nini Samia? Nani kama Samia? Ni Rais wa mfano na tunatakiwa tumtie moyo ili Rais wetu aende kufanya vizuri zaidi ya hapa alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kuzungumzia masuala ya kilimo. Ukienda kwenye kilimo sasa sisi watu wa Nyanda za juu Kusini ndiyo wabobevu katika sekta ya kilimo na ndiyo tunalisha nchi hii. Hakika katika sekta ya kilimo, mama ametutendea haki. Amepeleka ruzuku kuanzia kwenye mbegu, amepeleka ruzuku

kwenye viuatilifu na amepeleka ruzuku kwenye mbolea. Tumpe nini Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma mbolea ilikuwa bei juu, mnakaa vikao vya ukoo kujadili namna gani tutapata mbolea, lakini sasa hivi ukienda kwenye eneo hilo ni raha mustarehe. Watu wanavuna mazao yao, wanayauza mapema anaondoka ameuza mazao, anaingia dukani anachukua pembejeo za kilimo, anaenda zake shambani. Hapo vipi? Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamtanielewa lakini ninachokieleza maana yake ninachechemua. Ndugu zangu suala ambalo pengine ningelishauri Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi Serikali sikivu, ni kuendelea kutafuta masoko ya mazao ya wakulima wetu ili wakulima wetu waweze kwenda kuwekeza kwenye eneo hilo uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwa kipindi ambacho Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani bei ya mazao imezidi kusonga mbele. Yako baadhi ya mazao bado yana changamoto, lakini ninaamini kwa sababu jina lake ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaendelea kutafuta suluhu ya namna ya bei ili wananchi wake na wakulima wake waweze kufanya uwekezaji kwenye eneo hilo uwekezaji wenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninataka nizungumzie zao la kahawa. Mwaka jana watu wa Wilaya ya Mbinga wamenufaika kwa bei kubwa sana ya kahawa kutoka kwenye bei ya gunia shilingi 250,000, wameuza mpaka shilingi 900,000. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wako imara, wanaendelea kuhangaika na kilimo kwa sababu tayari wameona kwamba kahawa sasa ni mkombozi. Wametoka kwenye nyumba za nyasi sasa hivi wanaezua na wanakwenda kubandika bati. Nani kama Samia? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nani kama Samia?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umeisha

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Astaghfirullah! (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Isack Joseph, wajiandae Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo ujiandae.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kuniona ili niwe sehemu ya kuchangia hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Rais. Kwanza, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuwa ndani ya Bunge hili Tukufu, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na mimi kuwepo mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndio Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Halmashauri Kuu kwa kuniona na mimi mtoto wa mfugaji niwe sehemu ya Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wananchi wa Monduli kwa kunipa heshima ya kunipa kura za kutosha na kumpa Mheshimiwa Rais Samia kura za kutosha ambayo zimeniwezesha mimi kufika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajikita kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo kimsingi imejitafsiri yenyewe vizuri na imejielekeza vizuri haina jambo ambalo linaweza likamshinda mtu yeyote kuitafsiri kwa sababu hotuba imejitafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanamonduli tuna sababu ya kusimama kifua mbele na kumsemea Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya miaka minne ndani ya Jimbo la Monduli. Kwanza kuna wengine ambao hawafahamu miaka ya nyuma kabla ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kushika nafasi ya Urais tulikuwa inapofika kila mwaka Januari tunaanza kuwachangisha wananchi shilingi 10,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakuta wanafunzi tunawapeleka shule kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili ili tutengeneze madarasa, lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani mwaka wa kwanza tu akatupelekea madarasa ya kutosha kwenye shule zetu za sekondari na hatukuwa na mchango tena kwenye mwaka huo wa kuchangisha wananchi. Kwa hiyo, unaona ni jinsi gani alivyoanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea kila mwaka na ndani ya miaka minne ya utangulizi wa Mheshimiwa Rais tukajengewa zaidi ya madarasa 109, tukajengewa mabweni zaidi ya tisa, tukajengewa vyoo vya kutosha 64, tukajengewa nyumba za walimu 30. Hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Rais alipoingia tu ndani ya miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi tu; mnakumbuka miaka ya nyuma tulikuwa tunajenga sekondari zetu kwa kuchangishana, kukimbizana, kushikana, lakini Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani akatujengea shule za kisasa tano kwenye Kata ya Meserani, Lepurko, Mswakini na Mto wa Mbu kwenye Kata ya Migungani. Shule za kisasa yenye zaidi ya shilingi milioni 600. Hiyo ni kazi nzuri iliyofanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndiyo maana ninasema hotuba ya Mheshimiwa Rais

imejitafsiri vizuri na haina kazi ngumu ya kuitafsiri kwa sababu kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu; ninataka niseme mafanikio kwa sababu nilipata fursa ya kuwa sehemu ya kusimamia hayo mafanikio nikiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kwa zaidi ya miaka 10. Kwa hiyo, haya ninayoyazungumza, atakayezungumza huko pembeni akasema hayana ukweli aende kwenye Jimbo la Monduli aangalie matunda na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu; Mheshimiwa Rais alipoingia alikuta vituo vya afya zaidi ya viwili ambavyo ni Mto wa Mbu na Makuyuni havikukamilika, lakini ndani ya muda mchache akakamilisha akaweka na *ambulance;* vile vituo vya afya vile vikakamilika. Hatujakaa sawa akatujengea kituo cha afya cha kisasa kilichoko *NAFCO,* kilometa 54 kutoka Monduli Mjini mpaka eneo hilo ambayo kimsingi wananchi wengi wa maeneo ya Lokisale, Naalarami na Lemooti walikuwa wanapata changamoto ya kuja kwenye hospitali ya wilaya, lakini tunavyozungumza sasa tuna kituo kizuri cha kisasa cha afya kilichokamilika kilichokuwa na kila aina ya vifaatiba vilivyopo ndani ya hospitali ile na *ambulance* mpya ya kisasa ipo kwenye kituo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu; hospitali ya wilaya ukifika sasa hivi, niliwaambia watu wengine, wananchi wetu walipokaa kwenye foleni kumpigia Mama Samia kura walikuwa wana sababu za msingi za kumpigia kura kwa sababu hospitali yetu ya wilaya sasa utadhani ni hospitali ya mkoa. Ilikuwa asubuhi nasikia hapa watu wakizungumza juu ya kuhifadhi watoto njiti, hospitali yangu ya wilaya ina vile vitanda vya kuhifadhi watoto njiti 11. Kwa hiyo, kwenye Wilaya ya Monduli tume-*advance* kwa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale ukikuta maabara ya kisasa ambayo ukiilinganisha na mkoa havina tofauti. Hiyo yote ni kazi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye upande wa afya. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani tulikuwa

tuna uhitaji wa watumishi wa afya 341, lakini ndani ya kipindi hiki kichache cha Mheshimiwa Rais, tumeshaletewa watumishi wa afya 221. Unaona ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anafanya kazi yake. Unapokuta mtu tukizungumza haya anaona kama tunajifurahisha; hatujifurahishi. Nenda Monduli uone kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo; ukienda kwenye shule za msingi unaona ni jinsi gani tulikuwa tunapata wakati mgumu. Unakuta tuna madarasa hayajapauliwa, Mheshimiwa Rais alipaua yote na bado akatuletea fedha Monduli Juu tukajengewa shule ya kisasa ya zaidi ya shilingi milioni 480 ambayo watoto wa Wanamonduli, watoto wa wapigakura wa Monduli walikuwa wanapata wakati mgumu kwenda shule panapotokea mvua, kuruka korongo, lakini sasa watoto wale wanapata furaha kwa sababu Mheshimiwa Rais amewajengea shule nzuri ya kisasa pale Monduli Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, twende kwenye maji. Kuna mradi mzuri; niipongeze sana Wizara ya Maji, iliitafsiri mapema sana hotuba ya Mheshimiwa Rais. Unaona ni jinsi gani mradi kutoka kwenye miinuko yale ya Mto wa Mbu kushuka mpaka Vijiji vya Esilalei na sasa inaelekea mpaka kwenda Otukai mradi ambao uligharimu shilingi bilioni 1.9. Leo ukifika pale Esilalei na wengi wa viongozi wanapokuja wanapoingia kwenye ule mradi; umeshaanza kufanya kazi, umekamilika karibu 95% na wananchi kwenye vile vijiji wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu; tuna miradi miwili mikubwa ambayo ninataka niisemee kidogo. Kuna Mradi wa Vijiji Saba ulioko Makuyuni ambao mradi huo ulisainiwa mwaka 2024. Niiombe Wizara ya Maji, mradi ule umeshaanza na mkandarasi yuko *site*. Ningefurahi kwa kuwa wananchi wangu wanatamani kutumia au kunywa maji ambayo Mheshimiwa Rais aliwaahidi na ambao umeanza. Niombe mradi ule kwa sababu ukienda hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ameelezea kwamba, anatamani miradi mikubwa yote iliyoanzishwa ikamilike mpaka itakapofika 2030.

Ninaamini kwa sababu mradi umeshafikia hatua nzuri utakwenda kukamilika kabla ya kufika 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu; Mradi wa Vijiji 18 uliosainiwa 2014 wenye gharama ya karibu shilingi bilioni 20, niiombe Wizara hiyo kwa sababu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais na yenyewe imetafsiriwa vizuri kuhakikisha mradi unakamilishwa. Mradi ule na wenyewe ukamilike kwa wakati ili wananchi wa Monduli waendelee kufurahia matunda ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu, Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara hiyo iangalie kwa makini na ninashukuru Wizara hiyo yuko mtu makini, yuko mtu mchapakazi atahakikisha kwamba, tafsiri ya hotuba ya Mheshimiwa Rais anakwenda kuisimamia vizuri na kuhakikisha tunakwenda kupata hayo maji kwa wakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa ninasoma hii hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukijaribu kuangalia kila eneo alilolitaja, mimi nitajikita kwanza kwenye eneo moja hili la mifugo. Umeona Mheshimiwa Rais pale ameelekeza kwenda kutengeneza maeneo ya malisho kutoka hekta milioni 3.6 kwenda hekta milioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaamini kabisa kwamba Waziri mwenye dhamana na Mifugo atakwenda kutafsiri na kueleza kiundani juu ya maeneo ambayo tunakwenda kuongezewa kwa ajili ya ufugaji ili kuondoa zile tofauti kati ya wakulima na wafugaji kuhakikisha kwamba, hili tatizo linaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye hilo eneo Mheshimiwa Rais ameelekeza vilevile, kuhakikisha kwamba kunajengwa mabwawa, kuhakikisha kwamba migogoro baina ya wananchi na baadhi ya maeneo, (na Waziri anajua fika Monduli ina mgogoro fulani ambao kimsingi siyo mzuri) ninaamini tunakwenda kuumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme neno moja tu la mwisho. Tumbo lililomzaa Mama Samia Suluhu Hassan limebarikiwa, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kadogo kwa mchango wako mzuri. Kwa kweli Mama Samia amebarikiwa sana. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu ambaye amenijalia mimi kuwa miongoni mwa wale ambao wamepata kibali cha kurudia Bunge hili kwa awamu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninawashukuru sana ndugu zangu, wananchi wenzangu, wanawake wa Mkoa wa Tanga kwa kujitendea haki kwa kunichagua mimi mchapakazi jembe ambaye hakika sitaitweza thamani waliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii pia kuchangia hotuba hii tukufu ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 akilihutubia Bunge hili Tukufu, akitekeleza matakwa ya Kikatiba kama yaliyotajwa katika Ibara ya 91(1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa hotuba, hotuba nzito yenye mwelekeo chanya kwa mustakabali mpana wa Taifa letu la Tanzania. Ametoa hotuba nzito yenye kutuweka pamoja, yenye kutengeneza umoja wa Kitaifa, yenye kusisitiza amani na utulivu wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakika ameweka kiwango na rekodi ya juu sana. Hotuba

yake aliyoitoa tarehe 14 Novemba nimeifananisha na hotuba iliyowahi kutolewa na Margaret Thatcher, aliyekuwa Waziri Mkuu mwanamke wa Uingereza mwaka 1979 baada ya kushinda uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Margaret Thatcher na yeye katika hotuba yake ile alihimiza umoja na mshikamano. Ninaomba nirekodi kwamba Margaret Thatcher alisema: *"Where there is discord may we bring harmony, where there is error may we bring truth, where there is doubt may we bring faith, and where there is despair may we bring hope"*. Maneno haya ni sawa sawa na maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akitutaka kama Taifa tujirekebishe, tujielimishe na tuboreshe demokrasia yetu kwa kufuata misingi na tamaduni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa hakika ameweka rekodi kama mwanamke kiongozi bora katika dunia hii. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ametekeleza majukumu yake, hapana shaka kiwango cha Margaret Thatcher ameshakipita. Hakika mwanamama huyu amefanya mambo makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtia moyo kwa maneno ya kitabu kitakatifu, kitabu cha *Quran*. Kuna mahali panasema *"Falaa yahzunka qawluhum; innaa na'lamu maa yusirruna wa maa yu'linuun."* kwamba, "Yasikuhuzunishe maneno yao, hakika sisi tunajua yaliyojificha na yaliyo wazi". Mungu wa Mbinguni ambaye anaiona kazi kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nina hakika yuko pamoja naye na ataendelea kumlinda na Tanzania itaendelea kusimama katika viwango vya juu kabisa ndani ya dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa na sisi Mkoa wa Tanga tulikuwa na kila sababu ya kumjazia kura nyingi za kishindo. Hakika mama huyu kwanza kabisa ametutoa kimasomaso

wanawake wa Taifa hili. Kila aliyekuwa aki-*doubt* sasa hivi anaona haya kwa namna ambavyo amewa-*outshine* kwa kazi nzuri na kubwa ndani ya Taifa letu. Nani kama Mama Samia? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hamna.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia hakika jamani sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga ambao tulikuwa na viwanda, viwanda kadhaa ambavyo vilikuwa vimekufa, nami mwaka 2024 hapa niliomba katika Bunge hili Tukufu viwanda vile viweze kufufuliwa, lakini ndani ya siku 100 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari Tanga viwanda vitatu vimekwishakufufuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi vijana na wananchi wa Mkoa wa Tanga tunaona fahari kubwa sana kwamba hatukukosea sisi kumpa kura nyingi kwa namna ambavyo tumempa, 98% Mama Samia zinamstahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga Kiwanda cha *African Harmony* kimetoa ajira za kudumu kwa vijana 218. Kiwanda ambacho kimekufa muda mrefu sana tangu enzi za Nyerere, leo Mheshimiwa Mama Dkt. Samia amekuja kuirudisha rekodi ya Nyerere na kuirudisha ramani ya Mkoa wa Tanga. Tuna kila sababu ya kumwombea heri na baraka nyingi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama yetu huyu, kiwanda kingine cha *Rolling Steel* ambacho kinatengeneza nondo, kiwanda ambacho kinazalisha nondo takribani tani 30 mpaka tani 40 kwa wiki, leo Tanga kimeanza kufanya kazi ndani ya siku 100 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nani aseme kwamba eti Mhehsimiwa Dkt. Samia sijui ajiuzuru? Tutamjibu kwa hotuba ya Margaret Thatcher alisema: "*There is no turning back. The lady should go on; the lady is not weak; the lady is capable enough.*" Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda kingine cha *Plywood* kinachotengeneza *marine board* na *Plywood Tanga* tayari kinaanza kufanya kazi ndani ya siku 100 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mioyo yetu imejawa na unyenyekevu, imejawa na shukrani dhidi ya Mama huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hakika ametusaidia wanawake wa Mkoa wa Tanga, leo hii tunabeba maji majumbani kwetu kwa kiwango kikubwa sana. Ametuletea shilingi trilioni tatu katika miaka yake minne ya uongozi wake. Shilingi trilioni tatu hizo hazijawahi kutokea tangu Tanga imeumbwa. Tuna kila sababu ya kumwagia kura nyingi, kura nyingi za kishindo na hakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan bado dhamira yake ya kuleta ufanisi kwa wanawake wa Mkoa wa Tanga imeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ndani ya Wilaya ya Mkinga ametuletea juzi tu vifaa mwa! mwa! kwa ajili ya maji, shilingi bilioni 35 zimeshuka ndani ya Wilaya ya Mkinga. Nani kama Mama Samia Suluhu Hassan? Hakika tuna kila sababu ya kuuona mwelekeo wake chanya alioutoa katika hotuba yake hii kwa mustakabali mpana wa Taifa letu. Sisi Wabunge kama alivyotuusia kwamba tuibebe dhamana tuliyopewa na wananchi ili tuweze kushauri ipasavyo, nasi tutamshauri Mama bila hiyana kwa sababu ni Mama msikivu, anayoyatekeleza mambo yote tunayoyaweka katika matendo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan vilevile katika hotuba yake upande wa elimu ameonesha umuhimu wa kuunganisha mikoa na wilaya kidijiti ili kubadilishana uzoefu na wanafunzi kuweza kupata maarifa endelevu. Sisi tunamshauri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, jambo hili ni jema sana kuunganisha wanafunzi wa vijijini na mjini kidijiti kuweza ku-*share* uzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ionekane haja ya kuitumia TEHAMA kupunguza wimbi la upungufu wa walimu wa masomo ya

sayansi. Kwa kutumia TEHAMA tunaweza kumfanya Mwalimu mmoja akafundisha madarasa matatu kwa wakati mmoja na hapo tutakuwa tumetatua changamoto ya walimu wa masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga tunathamini sana kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunaahidi kwamba tutaendelea kuchapa kazi kumuunga mkono, kumsemea kwa dhati ya mioyo yetu. Tunaiona kazi njema, kazi anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomba, kupitia yeye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaamini msamiati hauwezekani, haupo ndani kwa Mama Samia. Mambo yake yote yanawezekana na amefanya makubwa katika Taifa hili. Tuendelee kumwomba atuwezeshe Barabara yetu ya Kiomoni – Mlingano kilometa 35.9 ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara ile imeshikilia uchumi wa Mkoa wa Tanga. Siyo Tanga Jiji, bali uchumi wa Mkoa wa Tanga unashikiliwa na barabara ile kwa sababu ya *the best limestone in Sub-Saharan African Countries* ambayo inazalisha viwanda vile vya saruji vilivyopo Tanga. Tunaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuvutia wawekezaji zaidi katika ukanda ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushukuru, nimekuona umeshika *mic* yako sawasawa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri na sasa ninamwita Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, wakati huo wajiandae Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera, Mheshimiwa Asha Baraka na Mheshimiwa Dotto Bahemu.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii tena. Awali ya yote nitoe shukrani kwa Mwenyezi Mungu aliyenijaalia afya njema na leo nipo hapa. Pia nitoe shukrani kwa wananchi wangu wa Jimbo la Ukonga kwa maamuzi sahihi ya kunichagua kuwa mwakilishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais, ni hotuba nzuri ya kiutu uzima yenye kujali yenye kuthamini watu wake. Hakika ni hotuba ambayo inatoka kwa mama mwenye kuwa na sifa ya kuwa mzazi na mzazi ana sifa ya ulezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais siyo mtendaji wa kila eneo. Ili Mheshimiwa Rais vazi ambalo amelivaa kwenye hotuba hii, vazi ambalo limempendeza liweze kuendelea kuwa vazi zuri mbele ya macho ya Watanzania, ninawaomba wasaidizi hasa Mawaziri, Manaibu wao, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wengine waweze kuendelea kumvisha vazi hili Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza haya ambayo Mheshimiwa Rais amewaahidi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa watachukua vyeo hivyo kama sehemu ya *show*, maana halisi ya hotuba ya Mheshimiwa Rais haitaonekana na tutajikuta na mwaka kesho tunakuja tukiwa tunarudi kwenye changamoto hizi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatoa wito sana huo na ninampongeza tena Mheshimiwa Rais. Nimeona Mawaziri wengi ni vijana; pia Mawaziri wengine wengi ni akinamama. Ninaomba watambue Mawaziri na Manaibu wao kwamba huko mitaani kuna wananchi wengi wamekaa wanaishi kwa matumaini kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais.  Kwa hiyo, ninaomba wanapokaa kwenye vikao wafikirie kwamba huko watu wanasubiri matarajio ya Mheshimiwa Rais, wakiishi kwa imani. Kwa hiyo, ni vizuri waangalie hapo. Vinginevyo tutarudi hapa kuulizana mara mbili mbili wapi wametekeleza kama Mheshimiwa Rais alivyotuletea wito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kuwaomba ndugu zangu hao Mawaziri na Manaibu na Makatibu Wakuu, ninaomba nijikite kwenye sehemu mbili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ni katika kitabu hiki cha hotuba ya Rais ukurasa ule wa 23 unaozungumzia habari ya urasimishaji maeneo ya makazi. Katika Jimbo langu la Ukonga, hasa Kata ya Zingiziwa, Chanika, Buyuni, Pugu na Pugu Stesheni, kumekuwa na changamoto zisizoisha zinazotokana na mkwamo wa Mradi wa Urasimishaji Ardhi, mradi ambao ukiongea na baadhi ya wazabuni wanazungumza kwamba unatokana na migogoro ya mipaka baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa ni kama watu tunagombea fito moja na huu mradi unavyochelewa pia Serikali inachelewa kupata mapato kutokana na urasimishaji ardhi. Ninaomba kwa sababu Kisarawe ni Tanzania, Ilala ni Tanzania, mamlaka inayotawala ni moja hebu watuondolee huu mvutano usiokuwa wa lazima kwetu ili wananchi waweze kupata hii huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili liwezekane, ni viongozi niliowataja miongoni mwao wenye dhamana ya hii kitu waweze kukaa kumaliza hili tatizo ambalo ni la muda mrefu. Nami pia ni mhanga wa matatizo haya ya mipaka kati ya Kisarawe na Ilala. Eneo ninaloishi Pugu Kajiungeni mguu mmoja upo Ilala mguu mwingine upo Kisarawe, lakini unapofika kwenye utendaji wa Kiserikali wao kwa wao wanavutana, Kisarawe wanavuta, Ilala wanavuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tuangalie namna ya kuondokana na hiyo hali ili kweli tuweze kuishi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais nina hakika Rais wote tunampenda ni Rais wetu wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayofuata ni Kifungu ukurasa wa tisa: ukurasa wa tisa unazungumzia Sheria ya Uchaguzi wa Wabunge inayoeleza kuwa mashauri yote ya uchaguzi yatafunguliwa kwenye Masjala ya Mahakama Kuu ambapo jimbo husika la uchaguzi lilipo. Kwa maana ya kwamba ukiwa unapinga

matokeo, basi utachagua unafungua kwenye Masjala ya Mahakama Kuu katika Jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa upande wa Zanzibar Mahakama Kuu ya Tanzania haina Masjala. Hivyo basi, hali hiyo hutoona kuwa hilo nalo ni sehemu ya kero ya Muungano na inafifisha upatikanaji wa haki hasa suala zima la uchaguzi, ukizingatia kwamba sheria ama miongozo inasema tufungue kesi mahali ambapo Masjala Kuu ilipo na kule Zanzibar Mahakama yetu ya Tanzania haina masjala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachofuatia hapo ni kwamba wananchi ambao wanakuwa na haki ya Kikatiba ya kukata rufaa kwenye vyombo vyetu vya kisheria wanashindwa kuitekeleza kwa sababu huo mlango wako umefungwa. Hivyo basi, ninavyoona kwa maslahi mapana ya Taifa letu na tumeona habari ya Muungano unavyosifiwa na kadhalika. Hili nalo tulione ni sehemu ya kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba pia watu wenye dhamana ya jambo hili waliangalie kwa mapana yake, kwamba kuna mlango watu wanakosa sehemu ya kupumulia. Kama unavyojua Waswahili wanavyosema, paka ni mnyama dhaifu sana, lakini ukimfungia kwenye chumba na wewe ukajifungia humo ndani ukafunga mlango, paka anageuka kuwa adui mkubwa sana wa mwanadamu. Ninaomba tufungue milango ili hiyo ahadi iweze kukaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo ninashauri kwa umuhimu wa pekee wakati tunasubiri mchakato wa Katiba Mpya kama Mheshimiwa Katibu Mkuu wetu alivyosema hapa, ni vizuri hili jambo liingizwe makusudi kwenye mchakato wa Katiba marekebisho madogo ili tuweze kuwapa haki Wazanzibari ambao imenyimwa ama imefungwa kwa mujibu wa miongozo ya makao makuu yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeweka nia ya kuleta hoja binafsi juu ya jambo hili ili tufikie mustakabli mzuri wa Taifa letu, kwa nia ile ile ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais juu ya uendeshaji wetu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze pia sehemu ndogo. Hapa nilipokuwa nimekaa wananchi wangu wamenikumbusha na nilikuwa ninaongea na Naibu Waziri wa Ujenzi, lakini nimeongea na Naibu Waziri upande wa *DAWASA* na kadhalika, suala la Barabara yetu moja ya kutoka Pugu Kajiungeni – Pugu Kirumba – *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile ni ya vumbi japo Naibu Waziri ametwambia kwamba ina mpango wa kutengenezwa kwa lami. Katika kipindi hiki ambacho tunasubiri barabra hiyo ya lami, pale yanapita magari makubwa malori, yanapita na mizigo na ile barabara ni ya vumbi na ni katikati ya makazi. Tumekuwa na shida ya vumbi, nyumba za pale zimechoka. Wakazi wa pale wako hatarini kupata *TB*. Hali yao si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa makusudi kabisa, wakati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wanaendelea kuchakata mpango wa kupitisha lami, basi upatikane mpango mahsusi wa makusudi. Aidha, pawe panamwagiwa maji kila siku ili vumbi liwe halipo, ama malori yale ya mradi yahamishwe badala ya kupita njia ile basi yazungukie *Kilitex* kutokea kwenye barabara ya lami ya Nyerere kuja huku yanakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, lakini mwisho wa yote nifunge kwa kusema Taifa letu amani yetu. Ninaomba wote kwa pamoja tuishi katika maneno kama hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kukushukuru kwa kunipatia fursa nami kuweza kuchangia katika mjadala huu wa leo. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa Bungeni ili kuweza kuchangia, ninaomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa baraka nyingi alizonipatia hadi kunifanya niwe Mbunge katika Jimbo la Butiama na kuwa Mbunge katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi pamoja na vikao vya juu kuniamini na kuniteua kwenda kugombea Ubunge katika Jimbo la Butiama na ninapenda pia wananchi wa Butiama kwa kura nyingi za kishindo ambazo walipatia CCM katika ngazi ya Urais. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipata 98% katika Jimbo la Butiama nami nilifuatia kwa kupata 97%, lakini kata zote 18 ziko kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Butiama walikuwa wana sababu za kufanya hivyo. Butiama imeanzishwa mwaka 2013, lakini kwa muda mrefu kumekuwepo na changamoto kwenye baadhi ya miradi, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia kwa muda wa miaka minne ameweza kutupatia zaidi ya shilingi bilioni 345. Haikuwa jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya mambo mengi makubwa katika Sekta ya Afya. Tuna kata 18, lakini wakati anaingia tulikuwa na kata tatu na yeye katika kipindi chake pia tumepata kata tatu zenye vituo vya afya, lakini sasa hivi tumeongeza katika kipindi chake vituo sita vya afya, hilo siyo jambo dogo. Katika kipindi chake pia ameweza kujenga zahanati 14, shule nyingi za msingi mpya na za sekondari na madarasa, matundu ya vyoo na mabweni yamejengwa katika kipindi chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya maji; tulikuwa tuna shida ya maji katika kata zote 18, kata mbili tu ndiyo zilikuwa zina

uhakika wa kupata maji safi na salama, lakini katika kipindi chake kuna mradi wa maji wa shilingi bilioni 70.5 ambao tayari umeshakamilisha miundombinu ya msingi na unaenda kutupatia maji katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, kilichosalia sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuweka mtandao wa maji. Ninadhani hili Mheshimiwa Rais ameshaahidi. Tayari nimeongea na Waziri wa Maji; ameahidi kuna mradi wa usambazaji maji ambao ni wa thamani ya shilingi bilioni 4.8, ukipatikana huo wananchi wataweza kupata maji kwenye maeneo kama ya Kata ya Mirwa, Buhemba, Muliaza na Busegwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Butiama pia tumepata Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere chenye thamani ya shilingi bilioni 102. Hiki chuo kitaongeza thamani sana katika maisha ya wananchi wa Butiama katika masuala ya ajira za muda mfupi na ajira za muda mref,u lakini pia wananchi wa Butiama na hasa kanda ya ziwa wataweza kusoma kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake hicho vilevile tumepata fedha shilingi bilioni 10.7 kwa ajili ya *TARURA*, shilingi bilioni 14.9 kwa ajili ya masuala ya *TASAF*. Hizo zote ni sababu za msingi ambazo zimepelekea Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupata kura 98% kwenye Jimbo la Butiama. Katika siku zake 100 tayari Wilaya ya Butiama tumepata watumishi 80 wapya kati ya hao 80, 50 ni walimu wa shule za sekondari. Vilevile, tumepata watumishi 27 wa sekta ya afya, watumishi wawili kwenye Kilimo na Mifugo na mmoja upande wa Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya nishati tuna vitongoji 160 ambavyo havina umeme, lakini katika siku zake 100 tayari vitongoji 51 vinakwenda kupata umeme, kwa hiyo vitongoji 119 vilivvyosalia maana yake ni kwamba kabla ya mwaka 2030 vitongoji vyote vitakuwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa, ninaomba sasa nijikite kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hotuba ambayo imesheheni matumaini

makubwa na mipango madhubuti ya kwenda kuibadilisha nchi yetu ya Tanzania. Ili uweze kuwa na maendeleo ni lazima wananchi wa nchi husika wapate elimu ya kutosha na hasa upande wa sayansi, teknolojia na uvumbuzi. Kwa hiyo, ukiangalia Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliielekeza Wizara ya Elimu kufanya mabadiliko ya kuboresha sera pamoja na mitaala ili kuweza kuweka mkazo zaidi katika elimu ya ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakwenda kujibu hoja ya watu kumaliza elimu ya msingi au sekondari wanakuwa hawana ajira na hii katika sera na mitaala pia ilivyobadilishwa maana yake elimu ya lazima sasa ni miaka 10. Kwa hiyo, ina maana vijana wetu itakapofika mwaka 2030, tutakuwa na *graduates* wengi sana wa *form four* na *form six*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelekeza pia katika masuala ya elimu ujuzi ukiangalia kwenye hotuba yake ukurasa wa 19 anasema: katika kipindi cha miaka mitano anakwenda kuweka msisitizo zaidi katika utekelezaji wa elimu ujuzi. Pia, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujenga *VETA* nyingi nchini Tanzania. Tunachokiomba kwa sasa ni kuhakikisha kwamba Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha zile *VETA* 65 ambazo zinajengwa, lakini pia tupate fedha za kununua vifaa kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia, ambapo sasa hivi kwa mtaala mpya ni kwamba elimu ni nyumbufu baadhi ya wanafunzi wanakwenda kwenye mikondo ya amali na wengine wanakwenda kwenye mikondo ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuonesha kwamba sasa anakwenda kutatua tatizo la ajira nchini ameamua kujenga shule za sekondari 830 katika kipindi cha miaka minne iliyopita na kati ya hizo shule, shule 103 ni shule za amali na shule 29 ni shule za amali za kihandisi (*technical schools)* kama ulivyokuwa unasikia *Moshi Technical School*. Sababu tunakwenda kuwa nazo shule 29, hilo siyo jambo dogo. Kuna shule 74 za amali zisizo za kihandisi na shule 694 ni shule za sekondari za kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hotuba hapa alisema anakwenda kuweka msisitizo zaidi katika masuala ya sayansi na hisabati na hasa kwa wasichana. Tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshajenga shule 26 za wasichana katika mikoa yote 26. Hilo siyo jambo dogo, lakini na tayari shule za kikanda saba kwa ajili ya wavulana zinajengwa na anataka kujenga shule katika kila mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote ukiyaangalia kwenye elimu ya ngazi ya awali, madarasa mengi ya awali, sekondari, msingi pamoja na vyuo vya kati yanajengwa kwenye nchi yetu. Sasa kwenye elimu ya juu napo amefanya mambo mengi makubwa ambayo kwa kweli watu wengi hawayafahamu, lakini ni makubwa sana. Kila mkoa kwa sasa unakwenda kuwa na kampasi za vyuo vikuu maarufu hapa nchini, hilo siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni kampasi za vyuo kama vile vya Mzumbe, *SUA*, *University of Dar es Salaam* na *Arusha Institute of Accounts* kwenye mikoa 15. Hivi vyuo vitaongeza fursa kwa vijana wetu ambao watakwenda kusoma kwenye hivi vyuo lakini pia ni fursa kwa ajili ya ajira ndogondogo na zitatumika pia kuandaa vijana ambao watakwenda kuwa walimu katika shule zetu za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu anasisitiza elimu ya ujuzi kuna mradi mkubwa wa *US Dollar* milioni 90 kwa ajili ya kukuza ujuzi katika nchi za Afrika Mashariki. Hapa vinajengwa vituo vinne vya umahiri ambavyo kwa Kiingereza inaitwa *centre of excellence*. Ukiangalia pale Dar es Salaam, *Institute of Technology* kuna kituo cha umahiri kwa ajili ya mafunzo ya TEHAMA na hii maana yake ni maandalizi kwa ajili ya kwenda, watu wetu kwenda kujifunza masuala ya akili unde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo kwenye kampasi hiyo, kwenye Taasisi ya Dar es Salaam kuna chuo kipo Mwanza ambapo watu watafundishwa mafunzo ya umahiri kwa ajili ya uchakataji wa ngozi. Pale *Arusha Technical College* kuna Kituo cha Umahiri kule Kikuletwa ambacho hiki kina *focus* katika masuala ya utafiti wa

nishati jadididifu, ambavyo vyote hivi vinakwenda kuandaa vijana wetu ambao watasoma kwenye shule za amali kuweza kubobea katika masuala ya ujuzi ili kuweza kuibadilisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kifupi ninataka kusema haya anayoyafanya Dkt. Samaia Suluhu Hassan, kwa sababau kama nchi ili kuweza kuendelea lazima tujiulize tulikuwa wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi? Mwanzoni kabisa tulitangaza kwamba tuna maadui watatu: maradhi, ujinga na umaskini na njia ya kupambana na umaskini ni kuwasomesha vijana. Kwa hiyo, ukiangalia fursa zote hizi maana yake vijana wetu wa Kitanzania wengi sasa hivi wakae mkao wa kusoma na mkao wa kupata ujuzi mbalimbali wa kuweza kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili haya yaweze kufanikiwa tunatakiwa kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu. Hayo mageuzi makubwa ambayo yamefanyika sasa hivi katika utekelezaji wa sera na miataala mipya yanahitaji fedha nyingi sana, ndiyo maana kwa muda mrefu tangu mwaka 1974 tulipokuwa tuna falsafa ya elimu ya kujitegemea wengi tulishindwa kutekeleza hilo kwa sababu ya gharama kuwa kubwa sana, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alithubutu na amedhamiria kuibadilisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa niunge mkono hoja ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Baraka.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuweza kwa mara ya kwanza kunifikisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Chama changu

Cha Mapinduzi kwa kuweza kuniteua leo Asha Baraka mnayemjua kila siku yupo katika mziki wa *dance* Twanga pepeta leo nimekuwa Mbunge, ninawatetea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamsifia sana Rais wetu kupitia hotuba yake, Rais wetu ameweza kupita sehemu tofautitofauti na hakuweza kubagua, ameweza kubadilisha watu tofauti na ukiangalia hii hotuba yake hakuna mahali alipoacha. Kwanza kabisa nizungumze tu kwa upande wa akinamama; ameweza kumtua mama ndoo kichwani na pia ameweza kumtua mama kuni kichwani kwa kupitia nishati safi na salama ya gesi. Leo akinamama wengi majumbani wanatumia gesi ambayo ni nishati safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu pia amekuwa mstari wa mbele sana kuhakikisha anaunganisha biashara kubwa. Leo sisi wanawake unaweza ukatoka Dar es Salaam kwenda Tabora, kwenda Kigoma na kadhalika mpaka Mbeya kwa kutumia barabara na unaweza kuendesha gari yako bila ya kuwa na matatizo yoyote, kwa sababu njia zote zipo ni lami tupu tunakwenda salama na zinaunganisha wafanyabiashara. Wafanyabiashara wa nchi za nje; kwa sisi tunaotoka mipakani, wanaweza kuleta biashara kufikisha Dar es Salaam au kutoa Dar es Salaam kufikisha Burundi, Rwanda na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichambua hii hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, ukurasa wa 35, Rais wetu ameweza kuchangia kiasi kikubwa sana katika njia za sanaa, utamaduni na michezo. Mheshimiwa Rais, ni mwanamichezo, yeye amekuwa mstari wa mbele sana. Kwa mfano, ukiangalia aliweza kucheza *film*, kacheza sinema ambayo wote tumeiona na imesababisha kuingiza watalii wengi sana hapa nchini kupitia *Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba anatoa motisha kwa wanamichezo. Wanamichezo mbalimbali wa hizi timu zetu kubwa na hususan timu ya Taifa, amekuwa mstari wa mbele kwa kutoa motisha, tunaita sisi wanamichezo goli la mama ambalo limesababisha watoto wetu au

vijana wetu kupata ajira na kupambana kuhakikisha anapambana katika mpira ili aweze kucheza katika timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan amepambana katika riadha, kama mnavyoona mwaka jana mmeona tumekuwa na mwanariadha ambaye amechukua tuzo ya medali ya dhahabu. Kwa hiyo, hizo zote ni juhudi za Mama Samia Suluhu Hassan. Vilevile, hakuacha wanawake katika mpira, kuna michezo mbalimbali hasa mchezo wa mpira wa miguu sasa hivi vijana wetu wa kike pia wanaweza kucheza mpira nchi za nje na wanapata ajira na wanaingiza kipato kwa kupitia hela za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu pia ameweza kuinua mpira wa ngumi ambao ulikuwa umesahaulika, sasa hivi ngumi nayo imekuwa ni ajira kubwa watu wanapigana huko wanapata pesa. Kwa hiyo, katika hii michezo yote, michezo ni pesa, michezo imekuwa ni pesa imekuwa na thamani kubwa hapa Tanzania. Pia, hakuacha kurudi nyuma kwa watu wenye uhitaji maalum, kuna michezo ambayo inapitia *Olympic*; michezo ya *Olympic* ambayo wanakwenda watu wenye uhitaji maalum kupitia *TOC* ambayo ni *Tanzania Olympic,* pia, Rais wetu hakuweza kuiacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa wale wanaocheza *basketball* kuna timu ambayo imekuja juu sana, inacheza mashindano ya kimataifa inaitwa *Dar City* imeweza kumfanya Hashimu Thabiti ambaye alikuwa anacheza *basketball* nje ya nchi naye anacheza katika hiyo timu kuhakikisha kwamba Tanzania nayo inaingia katika mashindano ya kimataifa ya *basketball*. Huyo ndiyo Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa huohuo wa 35 Rais, amesema kwamba tunaendeleza maandalizi ya ujenzi wa studio za kisasa ambazo tutatengeneza *film* bora na kama umeona mwaka jana Mheshimiwa Rais aliambatana na wasanii wa *film* kwenda Korea kuhakikisha kwamba wanapata mafunzo ya jinsi ya

utengenezaji wa *film* ili na wao waje kutengeneza *film* zenye ubora hapa Tanzania. Hilo amelifanya kwa dhati katika njia za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia anatutengenezea ukumbi wa kisasa, kumbi ambazo zitakuwa zinapiga burudani, tukiachana na mambo ya kwenda kupiga burudani kwenye kumbi kubwa ambayo tunalipa sisi wasanii kama shilingi milioni 30 mpaka milioni 12 kwa ukumbi lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye anatujengea kumbi ambazo wasanii watakuwa wanafanya matamasha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia, Samia Suluhu Hassan, ninaipongeza sana hii hotuba yake na ninaiunga mkono mia kwa mia. Tunakwenda kwenye *AFCON,* sisi Tanzania kwa mara ya kwanza, mashindano ya *AFCON* 2027 japo wengine walizungumzia, lakini nitaizungumzia kwa mapana zaidi. Juzi kama mmeona kwenye *TV* Mheshimiwa Rais alikuwa Arusha na Mheshimiwa Makonda mwenye Jimbo lake la Arusha Mjini na Rais mwenye dhamana ya utamaduni, kuna viwanja vinajengwa vya kuingiza watu takribani 30,000 ambavyo vitaingiza watazamaji, lakini hapohapo sisi akinamama, watu wa bajaji na watu wa bodaboda watafanya biashara kutumia michezo ya *AFCON* na kama unavyomjua pia Mheshimiwa Makonda huwa harudi nyuma unaweza kusikia pale nyama bure, leo tunachoma nyama tu Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpongeze pia Naibu Waziri Mwana FA na Katibu Mkuu kuhamasisha michezo ya *AFCON;* na yeye hakurudi nyuma mwaka jana wote ulikuwa unamwona kwenye goli la mama Mwana FA yupo, safari za timu ya Taifa yupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa mara ya kwanza kwa kutuma ndege ya *Air Tanzania* kwenda kuwapokea vijana wetu waliofanya kazi nzuri katika mashindano. Vilevile, ameweza kuwaalika pale Ikulu akakaa nao pamoja wakabadilishana mawazo na vijana wametuhakikisha kwamba

*AFCON* 2027 watafanya kazi ya ziada na kama mnaona pia juzi, Mheshimiwa Makonda alikwenda kupokea bendera ya *AFCON* akiongozana na Rais wa *TFF* pamoja na Waziri mwenye dhamana yake. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Makonda kwa kazi hiyo pamoja na watu wa Wizara wote kwa ujumla akiwepo Katibu Mkuu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu, nina mengi ya kusema lakini watu wengi wameshazungumza, mengine nitakuwa ninarudia zilezile *point* zao lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tusiache kumsemea, tunaomsemea ni sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo tunatakiwa tumseme na watu wajue Rais amefanya nini, wengine hawajui, wengine hawatembei. Tuwaombe pia wananchi waweze kutembea kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine kwa biashara na waangalie vitu ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, ajiandae Mheshimiwa Asha Omar na tutamalizia na Mheshimiwa Mabula Magangila.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata fursa hii ya kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu. Kwanza ninapenda kushukuru kwa kupata baraka ya uhai lakini pia, ninapenda kuwashukuru akinamama na wananchi wa Morogoro kwa kunipa dhamana hii kubwa. Kipekee, ninapenda kuishukuru Kamati Kuu kwa kunipendekeza na kuniona ninafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende moja kwa moja kwa maslahi ya muda, lakini pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu na ninaomba nikueleze, hotuba hii inasomwa na kila mtu na kama

unavyojua kitu kilicho kibaya hakiwezi kusomwa na mtu, lakini inasomwa na hiyo inaonesha ni kiasi gani hotuba hii imeshiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia alikuwa anasoma hotuba hii Watanzania wote macho yao yalikuwa hapa. Ni hotuba ambayo inaeleweka na inaweza ikasomwa na kueleweka hata na mtoto mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme machache. Nimebahatika kufanya ziara ya kikazi kabla sijawa Mbunge katika mikoa 11 ya Tanzania, nimefanikiwa kutembea kwa siku sita tu nikiwa ninaendesha. Katika mikoa 11 hii, barabara ambazo zilikuwa hazijakamilika hazikuzidi kilometa 60; hii inaonesha ni kiasi gani tumepiga hatua kubwa katika miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebahatika kwenda kwa ndugu zangu Kigoma, nimepita Kasulu, Kibondo, nimeishi kule mwaka 2018, lakini mwaka jana, 2025, nimepita pale nimekuta mpaka wana hoteli ambazo zina *presidential suit,* lakini nikikumbuka miaka ya 2018, 2016 kama kulikuwa kuna *guest* ya bei kubwa, basi ilikuwa ni shilingi 30,000. Nimewatembelea ndugu zangu wa Geita na Runzewe, kule ni kama umelala Abu Dhabi, Dubai, hii inaonesha kabisa ni kiasi gani kama nchi tumepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, maendeleo hayapimwi kwa macho, lakini kwa kuona. Katika sehemu nyingi hizo, kama nilizozitaja za Kanda ya Ziwa, Geita, Runzewe, nimebahatika kuona kumbi za starehe na za sherehe kubwa. Hii inaonesha ni kiasi gani tunaendelea kufunga harusi na kufanya sherehe kubwa kubwa kwa sababu uchumi umekaa mahali pake. Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, anatosha na anatosha tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nirudi katika Mkoa wangu wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, hatuna deni naye na kama mnavyojua Mkoa wa Morogoro ni katika mikoa ya kimkakati, mama aliahidi kwamba, Mkoa wa

Morogoro tutafufua viwanda. Toka mama ameingia, Mheshimiwa Dkt. Samia, tumefanikiwa kufufua kiwanda cha tumbaku cha Mkwawa Recce. Mwaka 2022, kwa takwimu za haraka, Mkwawa imeweza kuajiri wafanyakazi zaidi ya maelfu na kinaendelea kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe sasa hivi kimejengwa Kiwanda kikubwa cha Sigara cha Serengeti ambacho kinategemewa kwenye kuajiri wafanyakazi wengi. Kwa manufaa haya ya ufufuaji wa viwanda hivi ni kwamba, dhahiri zao la tumbaku linaenda kuongezeka. Historia inaonesha msimu wa 2025 tumeweza kuzalisha zao la tumbaku kwa zaidi ya kilo milioni 1.85, haya ni mafanikio makubwa na hii inaonesha kwamba, tunakoenda ni kuzuri zaidi ya tunakotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo tumefanikiwa kujenga Kiwanda cha Mkulazi cha Sukari, pale Mvomero. Kiwanda hiki kinatoaa zaidi ya ajira 5,000 na kwa mustakabali huu, maana yake ni tutaenda kuongeza kilimo cha miwa.  Siyo hivyo tu, kuna upanuzi ambao umefanyika wa Kiwanda cha Sukari kule Kilombero, hii pia, itachochea kilimo cha miwa na ajira. Hii yote inaonesha ni kiasi gani Tanzania ya jana siyo Tanzania ya leo. Kipekee, kama Mwanamorogoro, ninasema Mheshimiwa Rais ameahidi kuacha tabasamu kwa Watanzania, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, Wanamorogoro tabasamu tayari tunalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe kusema ukija kwenye mikopo ya 10%, mwaka 2021 kwa *record,* Morogoro tulifanikiwa kutoa mikopo ya shilingi bilioni 3.5, lakini kufikia mwaka 2025 tumefanikiwa kutoa mikopo ya 10% ya kiasi cha shilingi bilioni nane na wanawake zaidi ya 14,000 wanufanika. Hii inaonesha kwamba, uchumi wa mtu mmojammoja na uchumi wa watu kwa pamoja ni kiasi gani unaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, ninaishukuru pia, Serikali yetu kwa kutuona Wanamorogoro. Ninajua wote ni mashahidi, wiki iliyopita kaka yangu, Mheshimiwa Aweso, alikuwa Morogoro pale, tumepata fedha nyingi sana, kwa ajili ya maji Mji wa Morogoro, zaidi

ya shilingi bilioni 81. Kwa pesa hii Morogoro tutakuwa na maji mengi mpaka tutagawia majirani zetu Dodoma na Dar es Salaam. Hii yote ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu anatekeleza kwa vitendo, sisi Wanamorogoro tunamuahidi ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Waziri Mkuu jana, Mama ameonesha dira, sisi kama watendaji tuna kazi kubwa ya kwenda kusimamia maono haya makubwa ambayo Mama ametuletea. Mimi kama Josephine Kapoma ninatamani mwaka 2030 Bunge hili tusije kujadili changamoto, lakini tuje kujadili pesa nyingi tuliyonayo ni nchi gani tunatakiwa kuwakopesha. Ninajua hiyo inawezekana, kama tukitembea na maono ambayo yapo katika hotuba hii iliyosheheni kesho iliyo njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, ninaomba kuunga hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Omar na tutamalizia na Mheshimiwa Mabula.

**MHE. ASHA OMAR RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama katika Bunge hili Tukufu. Ikiwa leo ni mara yangu ya mwanzo, ninachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kipekee nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua na leo hii ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba na leo nimesimama hapa ndani ya Bunge Tukufu. Nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kubwa ndani ya moyo wangu, Wapiga kura wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, akinamama, kwa kuniamini na kuthubutu kunisimamisha hapa leo katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwa moyo wa dhati ninampongeza Mheshimiwa mama yangu kipenzi cha Watanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hotuba yake nzuri

iliyojaa maono, iliyojaa fikra. Hotuba hii imemaliza kila kitu, mama kwa kweli, hapa amefanya kazi na anatekeleza; kweli mama ni mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na wanawake wa UWT Mkoa wa Kaskazini Pemba wanampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake iliyotaradadi na iliyojaa muono wote wa Watanzania. Ninachukua nafasi hii kuchangia yale niliyoyaona katika hotuba ya Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Rais ni mwanamke pekee aliyeweza na mwenye muono wa mbali. Vilevile amejikita kama mama katika uongozi huu, lakini hakukaa kama Rais tu, ameona kama ni mama ambaye anathubutu kubeba, kuwasilisha na kusimamia majukumu yote ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naenda kwenye sekta ya afya. Mheshimiwa Rais alipozungumzia suala la afya hapa alitumaliza sote wananchi na hadi ikafika siku ya uchaguzi kila kitu kikakaa sawa. Mheshimiwa Rais ameboresha huduma za afya katika mikoa yetu, tukiangalia sasa hivi katika mikoa yetu tuna hospitali za wilaya ambapo tunapata huduma tofauti na huko nyuma tulivyokuwa na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameboresha huduma iliyo bora na sahihi mpaka kusababisha sasa hivi vifo vya akinamama na watoto wachanga vimepungua kwa asilimia kubwa, jamani hakuna kama mama. Huyu mama tumpongeze na lazima ukweli wake usemwe, jamani, mama tumzungumzie vizuri na apewe maua yake. Mama amethubutu kama mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha huduma ya afya tukapata huduma nzuri akinamama na watoto, amehakikisha mnyonge maskini wa chini akienda katika vituo vya afya anapata huduma iliyo sahihi sawasawa na mtu aliye na kipato cha juu, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Imefika hadi sasa hivi kwenye sekta ya afya akifika mgonjwa pale, kama kalazwa siku mbili

anatamani aongeze siku kwa huduma nzuri anayoipata. Jamani mama anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye sekta ya maji ni kila kitu. Maji ni afya na mama ndiyo kalizungumza kwenye kitabu chake hiki cha hotuba na ameboresha miradi na kuisimamia. Ameweka muda iweze kufanya kazi na watu wote wapate maji kwa sababu, bila maji hakuna lolote, maji ni uhai, maji ni kila kitu. Maji haya haya ni kwamba, Mheshimiwa Rais ametugusia sisi akinamama wakati tunapokwenda kwenye huduma zetu, ama kikazi ama kiafya, mama unakwenda pale ukiwa na matumaini, ukiwa na imani kwamba, huduma pale unayoipata ni bora na sahihi, lakini huku nyumbani ukirudi huduma ya maji inapatikana muda wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Mawaziri wanaoshughulikia sekta hii ya maji, wasimamie vizuri, wamkamate mama mkono. Hili suala, kama alivyolisema mama, lifanyike kwa uadilifu na wananchi wapate maji kwa wakati sahihi, wa mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika huyu ni mama, amejitoa kwa Watanzania. Huyu mama anaweza na ni wa kumpigia mfano. Tutake tusitake tumzungumze mama kwa utekelezaji wake mzuri, tutake tusitake, tusimame tumsemee mama kwa muono wake wote wa kuwaona Watanzania, kuwajali wanawake na kuwajali vijana na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya mengi tena ya kupigiwa mfano, anastahiki kupewa tuzo. Ni mwanamke bora, ni mwanamke shupavu aliyejitolea, halali usiku, halali mchana, muda wote anatafakari nchi yake inakwenda vipi? Iende vipi? Wananchi wake watakaa vipi? Ilimradi wananchi hawa anaowasimamia wawe katika hali ya salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi na wanawake Mkoa wa Kaskazini Pemba wanasema, mcheza kwao

hutunzwa, huyu mama ni lazima atunzwe. Vilevile, wamenituma nimpe salamu mama, wanamwombea dua, wanamwombea kwa Mwenyezi Mungu mama huyu kila anapokaa Mungu amlinde, amsimamie, ampe maisha marefu, ampe maisha mazuri na awe na uthubutu wa hali ya juu kabisa kusimamia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninamalizia kwa kusema muungwana ni vitendo na vitendo vya mama tumeviona. Ninaomba kuunga hoja ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Mabula Magangila.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi ya kuongeza pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba nikusaidie kidogo, jina langu ni Mabula Magangila kutoka Jimbo la Msalala, Mkoani Shinyanga, Wilaya ya Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kwetu sisi Wanamsalala kwanza kabisa, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi njema kabisa ambazo anafanya kwa Taifa letu. Kwetu sisi siyo tu hotuba, kwetu sisi Mheshimiwa Rais amegusa maisha ya Wanamsalala, lakini kabla ya Wanamsalala ninaomba nisemee sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ni Rais ambaye amekusudia kuleta mageuzi makubwa kwa sekta binafsi. Ni Mheshimiwa Rais huyu ambaye ameingia madarakani nchi yetu ikiwa inakusanya shilingi trilioni 18, leo hii tunakusanya shilingi trilioni 32, mapato haya hayatoki nje ya wafanyabiashara ni Rais huyu ndiye aliyeboresha mazingira na kuweka mazingira wezeshi ya wafanyabiashara. Rais huyu ndiye aliyekataa kamatakamata ya wafanyabiashara, ni Rais huyu ndiye aliyeweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa vibali katika sekta yoyote unayotaka kufanya

biashara, ni Rais huyu ndiye aliyethubutu kutunga sera nzuri kabisa, hasa katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza hapa Awamu ya Sita ndiyo ambayo migodi mingi mipya imeanzishwa. Wachimbaji wadogowadogo na wanaojifunza kuchimba wamechimba, wanaojua kuchimba wanachimba, wenye leseni wanachimba, wanaotaka kushirikiana na wenye leseni wanachimba, awe ni mtu ambaye anataka kwenda kuokota ukwale, wale akinamama wanapata dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu hii ya Sita umeanzishwa mgodi pale Sengerema, Mgodi wa Nyanzaga. Ni katika Awamu hii ya Sita umeanzishwa mgodi kule Kabanga *Nickel* ambao unamilikiwa na Tembo *Nickel,* katika Awamu hii ya Sita. Leo hii tayari *pilot plant* ya madini ya *uranium* imekamilika, Awamu hii ya Sita, lakini kwenye *graphite* tayari tuna Faru *Graphite*, tuna Lindi Jumbo tayari uzalishaji umekwishaanza. Ni Rais huyu ndiye ambaye ameruhusu haya yote yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya yote kufanyika katika sekta hii binafsi naomba Wizara ya Fedha, haya mambo yote aliyoyafanya Mheshimiwa Rais kwa utashi wake Bunge hili tukubaliane yawekewe sasa Sheria kali, ili yasije tena yakabadilika na kupeleka huzuni kubwa kwa wafanyabiashara. Tungependa kusudio hili la Mheshimiwa Rais la kuboresha sekta hii binafsi na kuifanya Serikali yake kuwa ni sekta wezeshi na siyo sekta inayo-*control* na kuzuia maendeleo ya Watanzania. Tukatunge sera nzuri, tuweke Sheria nzuri za kuendelea kuweka hali hii ambayo Mheshimiwa Rais amekusudia isichezewe na mtu yeyote atakayekuja hata baada ya yeye kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya madini, tumeweza kuanzisha migodi mipya, lakini ni migodi ambayo ilifanyiwa utafiti miaka mingi nyuma, twendeni sasa kupitia Wizara yetu ya Madini, Mheshimiwa Rais amekusudia kuweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi, ili kukuza sekta binafsi. Twendeni tukaweke vivutio hivyo,

tukaongeze utafiti. Kampuni nyingi za utafiti, hasa zinazomiliki leseni kubwa za utafiti ziliacha kutafiti. Tunapoacha kutafiti tunaua matarajio ya kuwa na migodi mingine mikubwa kama Geita, kama Barrick, North Mara na Bulyanhulu, ambayo ilitafitiwa miaka mingi nyuma. Twendeni tukae na hawa wawekezaji, tuangalie ni kwa namna gani tutawavutia watafiti migodi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii sisi Msalala tunanufaika na mwekezaji mmoja tu, Bulyanhulu, ambaye ameweza kutuchangia *CSR* ya kujenga barabara ya lami kutoka Kahama kwenda mpaka kule Kakola, kilometa 71, shilingi bilioni 101. Hivi leo hawa wawekezaji wetu tukiwavutia zaidi, wakatafiti migodi mingine, wakaanzisha migodi mingine, tukafungua migodi mingine mikubwa zaidi kwa kushirikiana na wachimbaji wetu wadogowadogo tutapata *CSR* kiasi gani; hata hizi pesa tunazohangaika kutafuta, kwa ajili ya miradi yetu ya *TARURA* inawezekana *TARURA* na wenyewe wakajenga barabara nyingi za lami kuliko za moramu. Twendeni tukaimarishe sekta binafsi tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, ili tuhakikishe tunapa pesa nyingi zaidi, kwa ajili ya ku-*finance* miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Msalala kwa kumchagua Mheshimiwa Rais kwa kishindo. Mimi Mbunge wao ninawaahidi sitawaangusha, sisi kule tunasema jambo moja tu, Msalala moja, maendeleo kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza orodha ya wachangiaji wa siku ya leo. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano, ninawatakia jioni njema. Sasa ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho asubuhi, saa tatu kamili.

*(Saa 1.24 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 29 Januari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*